

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 4 Julai, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, karibuni tena kwenye kipindi chetu cha asubuhi katika ratiba ya siku yetu ya leo. Lakini kabla sijamwita Katibu atupe utaratibu, ninaomba leo kwa nafasi nyingine maalum kabisa nitambue uwepo wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri Mbunge huyu baada ya kuona leo ni Wizara ya Afrika Mashariki inayofanana kabisa na Mambo ya Urambo Mashariki, basi naona amejiandaa hasa leo kuja kufanya kazi yake kwa dhati humu na nafikiri attachangia hii Bajeti leo. Kwa hiyo, tunamkaribisha sana. (*Makofî*)

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:-

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:-

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2008/2009.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY- MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:-

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 157

Tatizo la Maji Nchini

MHE. MWAKA ABDULRAHMAN RAMADHAN aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la maji limekuwa sugu nchini na Serikali hajapata ufumbuzi wa tatizo hilo Vijijini na Mijini hasa kwenye Jiji la Dar es Salaam:-

(a)Je, kwa nini *DAWASCO* inapeleka *bill* za maji kwa wateja wakati hawajapata huduma hiyo?

(b)Je, Serikali haioni kuwa, wananchi hao hawatendewi haki?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abdurahaman Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, *DAWASCO* inatoa ankara kwa kwa wateja wake ambao wako kwenye makundi mawili: Kundi la kwanza ni la wale waliofungiwa dira za maji ambao hulipa ankara zao kulingana na jinsi wanavyotumia maji. Kundi la pili ni la watu ambao hulipa ankara zao kwa kukadiria (*flat rate*) kulingana na upatikanaji wa maji katika maeneo husika baada ya kufanyiwa uhakiki (*assessment*). Kwa mfano, huduma katika maeneo ya Mlandizi, Kibaha, Kibamba, Mbezi, Kimara, Ubungo na Kisukuru inatolewa kwa mgao ambao mara nyingi unavurugika baada ya kuwa na

hitilafu kwenye mitambo. Kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna wateja wachache wanapelekewa ankara bila kupata huduma.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maji ya 2002 inaeleza wazi kwamba kwa kipindi kirefu wananchi wamekuwa wanapewa huduma ya maji safi na uondoaji wa maji taka kwa bei ya chini isiyokidhi gharama halisi.

Hali hii imefanya kazi ya kukusanya maduhuli kuwa ngumu. Baadhi ya wananchi bado wanaona vigumu kuunganisha maji kihalali na wale wenye akaunti wanachelewa kulipa ankara zao.

Aidha, Mamlaka za maji nazo bado zina udhaifu katika utayarishaji wa ankara za maji na ufungaji wa dira za maji kutokana na uwezo wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa siyo halali kabisa kwa *DAWASCO* na Mamlaka nyingine za maji nchini kuwapelekeea ankarra wateja ambao hawajapata huduma ya maji. Aidha, ili kuondoa tatizo hili, Serikali kuitia *DAWASA* inatekeleza mradi wa kukarabati na kuboresha miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam.

DAWASCO itaendelea kuwafungia wateja wake dira za maji ili kila mtu alipie huduma kulingana na matumizi yake ya maji. Hadi Juni, 2008, wateja 30,000 wamefungiwa dira 30,000 kati ya wateja 64,000. Katika mwaka 2008/2009, *DAWASCO* inatarajiwu kufunga dira nyingine 16,500.

Aidha Serikali inawataka *DAWASCO* kuzingatia mgao wa maji kwa kufuata ratiba waliojiwekea ili kila mteja apate ankara kulingana na huduma aliopata.

MHE. MWAKA ABDULRAHMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali la kwanza kama ifuatavyo:-

(a)Kwa kuwa kuna baadhi ya nyumba nyingi kama nilivyoeleza katika Jiji la Dar es Salaam bado hawajafungiwa mita na wale ambao hawajafungiwa mita ikifika mwisho wa mwezi wanapelekewa bill na mchana kubwa maji yanakuwa hayapatikani yanapatikana time za usiku. Hizo bill zinapopelekwa huwa haziwi nusu kama vile yanapatikana maji zinakuwa kamili. Je, tatizo hili la kupata maji usiku litaisha lini ili wananchi wa Jiji la Dar es Salaam waweze kulala vizuri wakati wa usiku na siyo kukaa kulinda maji?

(b)Kwa kuwa katika Jiji la Dar es Salaam mara nyingi maji yanakuwa yana vumbi na inabidi mtu ayaweke yale maji kwa muda mrefu ili yawewe kujichuwa kujitenga maji safi juu na maji yenye tope yaye. Je, tatizo hili litaisha lini kukaa mtu akayasubiria maji yajichuje safi juu na chini maji machafu yenye tope kwani hapa kila siku likiulizwa suala

hili tunaambiwa kunafanya marekebisho. Haya marekebiso yamatilizika lini ili watu waweze kupata maji bila kupoteza muda wa kuyasubiria kujichuja? Ahsante.(*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwaka yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tayari *DAWASCO* kwa kushirikiana na *DAWASA* wanaweka utaratibu wa kutuwekea mita na nimesema kwamba wamefunga mita/dira za maji 30,000. Sasa mwaka huu pia tunatarajia pia wafunge mita/dira zingine 16500 hii ndiyo njia mojawapo itakayotusaidia kuhakikisha kwamba watu wanapata maji kulingana na kiasi walichotumia.

Lakini nikija kwa ujumla katika suala la lini haya matatizo yataisha kama nilivyosema pia ni kwamba Wizara ya Maji hivi sasa inao utaratibu wa kukarabati miundombinu ya maji katika vituo vyote vya kusukuma maji, Ruvu Chini, Ruvu Juu, Mtoni, kote huko utaratibu unaendelea maana yake kwamba mradi unaendelea kutekelezwa.

Sasa itakapokuwa tayari vichujio vimetengenezwa basi mimi nina hakika kabisa tatizo hili litakuwa limekwisha katika muda si mrefu. Maana kazi zinaendelea. (*Makofî*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Benki ya Dunia inafadhili miradi ya maji katika vijiji vyetu na kila Wilaya imepangiwa vijiji 10; na kwa kuwa sera ya maji ni kuchangia mifuko ya maji na kuwa Wilaya nyingi zimechangia mifuko ya maji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri analieleza nini Bunge hili kwa nini miradi hii awamu ya tatu imechelewa sana kikiwemo kijiji cha Chunyu ambako wanunuua ndoo moja ya maji shilingi 400?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri. Hili swali limehama kutoka *bill* nusu sasa inatakiwa maji kamili.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikiri kwamba mradi huu umechelewa sana kuliko tulivytarajia na wananchi kule wanasubiri sana na wamekwishachanga na fedha. Lakini nitoe taarifa tu kwamba baada ya kuona tatizo hili Wizara imeamua kwamba Wizara mwenye dhamana aje Bungeni atoe kauli ya utekelezaji wa mradi huu na atakapokuja ataeleza nini hasa kilichotusibu katika kuchelewesha ikiwa ni pamoja na kueleza sasa ni hatua gani tuzifanye. Kwa hiyo, naomba tuwe na subira kidogo kwa sababu atafanya hivyo katika Mkutano huu huu wa 12. Hili naomba pia niseme kwamba najua baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge wengi watataka kujua orodha ya wale watu au Halmashauri ambazo zimepelekewa fedha zile za mradi wa maji safi na usafi wa mazingira. Ni kweli hii orodha tumeitoa na fedha zimeshafika. Lakini naomba tumekubaliana na

Mheshimiwa Waziri kwamba baada ya kutoa kauli kuhusu mradi huu na *way forward* basi na orodha hiyo tutaitoa wakati huo huo. (*Makofî*)

Na. 158

Ujenzi wa Mabwawa

MHE. JACOB D. SHIBILITI aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilianza uchimbaji wa Bwawa la Nyashitanda Wilayani Misungwi tangu mwaka 200; na kwa kuwa, Mkandarasi huyo hakuwa na vifaa vya kutosha na masika ilimkuta akiwa hajamaliza kazi hiyo; na kwa kuwa, Serikali ilijibu katika Kamati kuwa; kazi hiyo imefanyika kwa asilimia 80 (80%):-

- (a) Je, ni kweli kuwa matengenezo hayo ni asilimia 80 ya ujenzi?
- (b) Je, ukamilishaji wa bwawa hilo utanza lini na ni nani atakayekamilisha kazi hiyo?
- (c) Je, bwawa la Ikungumhulu likoje kwa sasa na sehemu ya kunyweshea mifugo ilishajenngwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Bwawa la Nyashitanda ulianza mwezi Juni mwaka 2007. Mwezi Novemba, 2007 ujenzi ulisimama kutohana na mvua nyingi zilizonyesha katika eneo la Bwawa na maeneo mengine jirani. Hadi ujenzi uliposimama, ni kweli kuna utekelezaji ulikuwa umefikia wastani wa asilimia 80, kama ifuatavyo:-

- (i) Uchimbaji wa udongo kwenye eneo la Bwawa kwa kina cha meta 13 za ujazo 42,997 ulikuwa umekamilika;
- (ii) Uchimbaji wa utoro wa maji (*speed way*) umekamilika;
- (iii) Uchimbaji wa msingi wa tuta nao (*core trench*) umekamilika;
- (iv) Ukusanyaji wa mawe kwa ajili ya tuta la bwawa umekamilika.

(b) Kazi iliyobaki katika ujenzi wa Bwawa la Nyashitana ni ujenzi wa tuta lenye kimo cha meta 2.1 na urefu meta 358. Kazi hii inatarajiwaa kuanza tarehe 14/7/2008

ambapo mitambo ambayo hivi sasa iko katika eneo la kazi itaweza kufanya kazi bila kukwama.

Aidha, kazi yote iliyobaki itakamilika na mkandarasi ambaye ni Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mbwawa (*DDCA*) akisaidiwa na Kampuni ya *Ntui Commercial Company* ambayo ndiyo mkandarasi msaidizi wa ujenzi wa Bwawa hilo.

Utaratibu umeandaliwa ambapo mkandarasi anajipanga vizuri kwa kupelekea malori na mafuta ili kazi iweze kuendelea. Mpango kazi uliopo unaonyesha kwamba kazi zilizobaki zitachukua muda wa majuma sita. Kwa hiyo, tutarajie kukamilika kwa Bwawa mwishoni mwa mwezi Agosti, 2008.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa ujumla wake kwa kuwasaidia sana wananchi wa Kata ya Shilalo na Buhungukila kwa ujumla wake wanasema hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri hiyo.

Kwa kuwa tatizo la Shilalo linafanana kabisa na tatizo la Kata ya Mwaniko nimeshatuma maombi yangu kwake hali yao ni mbaya sana anaahidi nini kwa Kata yangu ya Mwaniko ambao wana tatizo linalofanana na lile la Shilalo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, matatizo hayo yanafanana kwenye Kata hizo zote mbili.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti kama ifuatavyo:-

Kwa kawaida huwa hatutoi miradi kwa kuchagua Kata, isipokuwa kama walivyofanya kwa mabwawa mengine yaliyoteklezwa. Mimi ninamshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba ye ye apite katika vikao vya Halmashauri halafu basi alete mapendekezo ya miradi gani, ni mabwawa ambayo angependa tufanye kama tunavyoendelea kufanya. Nataka nimwahidi Mheshimiwa Shibiliti rafiki yangu sana kwamba akifuata taratibu hizo na mimi ninamwahidi kwamba nitakuwa tayari kumsaidia na Kata hizo zingine nazo zipate. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa eneo hili linalozungumzwa la matatizo ya maji la Misungwi kuna mradi mkubwa wa *Lake Victoria* ambao umeshakamilika na sasa hivi unasubiri kusambazwa maji kwa wananchi wa Shinyanga na Kahama na kwingineko.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kupeleka bomba katika Jimbo la Misungwi ili kutatua haya matatizo ambayo yanawakabili wananchi hao kwa sababu eneo ni hilo hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Kahama – Shinyanga wa kutoa maji *Lake Victoria* umekwisha kamilika kama alivyosema mwenyewe. Hivi sasa tunachofanya tunafanya *test* au *trial run* kuhakikisha kwamba maji yale yatakapotiririka mpaka Kahama basi vile vifaa vyote tulivyoweka ikiwa ni pamoja na mabomba na matanki visiharibike. Kwa hiyo, sasa ni uchunguzi tu wa mwisho wa kiutaalam kuhakikisha kwamba hayo maji yatatiririka bila kuleta athari. Lakini kuhusu maji hayo kuanza kusambazwa katika maeneo mengine, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba huu mradi ulipowekwa ulikuwa na malengo yake, vijiji vilivyopangwa na kwamba hivi sasa tunachofanya ni kwamba vijiji vilivyoko kilomita 5 kutoka kwenye bomba kuu kulingana na mradi ndivyo kwanza tuhakikishe vinapata maji. Sasa kama yatakuja maombi mengine baadaye yatakuja baada ya hii awamu ya kwanza kwisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Swali la mwisho, uwakilishi wa *gender* Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na kuniona kwa jicho la huruma. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba niulize swali ndogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, tatizo la Wilaya ya Misungwi linafanana na tatizo la Manispaa ya Tabora kwenye Bwawa la Igombe. Bwawa la Igombe ni la miaka mingi tangu wakati wa mkoloni, na bwawa la Igombe linatoa maji machafu ambayo ni kama tope na yana harufu mbaya. Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuhakikisha kwamba inaboresha hayo maji ili wakazi wa Manispaa ya Tabora waweze kupata maji safi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Igombe ni mojawapo ya vyanzo vya maji tunavyovitegemea kwa ajili ya Mji wa Tabora. Sasa tunachokifanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba vyanzo vyote vinahifadhiwa na vikishahifadhiwa basi tunaweka pia taratibu za kwamba maji yanapotoka pale yapate vichunjio na yawafikie wananchi yakiwa salama. Kwa hiyo, mimi ninchoweza kusema tu ni kwamba Wilaya au Halmashauri ile ya Mji iendelee kufuutilia utaratibu wetu wa kuomba fedha kwa sababu zipo ili Bwawa hilo liweze kushughulikiwa kama Mabwawa mengine yanavyoshughulikiwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, swali 159 ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Mpenda kwa ridhaa yake Mheshimiwa Issa Kassim Issa ameliondoa swali hilo. Kwa hiyo, halitajibiwa tena leo ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

Na. 159

Liliondolewa na Muuliza swali Mheshimiwa Issa Kassim Issa.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, ninaomba niendelee na swali linalofuata nalo linaenda Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na litaulizwa na Mheshimiwa Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni.

Na. 160

Asili ya Wimbo Maarufu wa Malaika

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN aliuliza:-

Kwa kuwa, Wimbo maarufu wa ‘Malaika’ asili yake ni Mkoa wa Kilimanjaro – Tanzania; na kwa kuwa, waimbaji wengi wa kigeni kama vile Bonny M, Mariam Makeba n.k, wamekuwa wakiimba wimbo huo:-

Je, nchi yetu inanufaika vipi na wimbo huo kutoka kwa waimbaji wageni?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inanufaika kwa njia mbalimbali pale ambapo waimbaji wengi wakiwemo wa ndani na nje ya nchi wanapoimba wimbo wa Malaika na nyimbo nyingine nyingi zinazohusu nchi yetu ya Tanzania. Kwa kutumia mfano alioutoa Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, ambapo waimbaji wa kigeni kama vile Bonny M, Mariam Makeba n.k ambao wamekuwa wakiimba wimbo maarufu wa Malaika, Serikali inanufaika sana kutokana na wimbo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, wimbo huo unaitangaza nchi yetu duniani. Lakini pia kwa vile wimbo huo umeimbwa kwa lugha ya Kiswahili, hivyo basi wanaitangaza lugha yetu ya Kiswahili. Kwa namna nyingine, pindi wimbo huo unaposikika, wasikilizaji wanatambua kama kuna lugha ya Kiswahili na asili yake. Aidha, wasikilizaji wa wimbo huo hushawishika kujifunza lugha ya Kiswahili. (*Makofit*)

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida hizo alizozisema Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina taarifa kuna nchi moja jirani inanufaika kifedha. Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Sasa nchi hiyo sijui ni nchi gani. Nafikiri tuendelee na swali lingine la nyongeza. Mheshimiwa Mbunge, kama unaijua nchi hiyo nitaomba umnong'oneze Mheshimiwa Naibu Waziri ili basi aende akafuatilie yatusaidie hayo mapato yaweze kuja katika nchi yetu ya Tanzania pia.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana na ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, sisi wengine humu ndani Bungeni tulikuwa waimbaji ni vyema tukamjua huyo mtunzi wa wimbo huo na yeze mwenyewe anafaidika na nini huyo mtunzi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri amesikia swali hilo au kama anamfahamu hebu atwambie huyo mtunzi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba wimbo huo unaojulikana kwa jina la Malaika ulitungwa na Mtanzania ambaye alikuwa anamsifia mpenzi wake anayeitwa Malaika, na kwa bahati mbaya kwa utafiti wote na wataalam wote wamefanya mpaka sasa hivi jina la huyo aliyeutunga halijajulikana, lakini ni Mtanzania anayetoka Kilimanjaro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini anafaidikaje? Kwa bahati mbaya kama walivyosema Mheshimiwa Parmukh Hoogani na Mheshimiwa Haroub Masoud, aliyeafaidika na kupata hakimiliki na mirahaba ya wimbo huo ni mzee mmoja ambaye amefariki ni Mkenya anaitwa Fadhili Williams, yeze ndiye aliyekuwa anafaidika na wimbo huo kwa sababu yeze ndiye aliyeurekodi. Sasa Sheria za hakimiliki ni kwamba anayerekodi kwa Sheria za Kenya ndiye anayepata mirahaba. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, labda tumsikie Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kwa sababu ni Mbunge wa siku nyingi anaweza akawa anamjua huyo mtunzi.

MHE. TEDDY L. KASELLA -BANTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kukiri kwamba pamoja na kwamba ni Mbunge wa siku nyingi simfahamu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na majibu mazuri ya nyongeza naomba niulize swali moja la nyongeza dogo. Kwa kuwa, wimbo wa Malaika na nyimbo

nyingine huwa zinatakiwa ziendelee hivyo hivyo bila kubadilisha lafidhi au maneno na sasa vijana wa siku hizi wanauimba wimbo huo wanaubadilisha. Je, Serikali inasemaje kuhusu ubadilishwaji huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu swali lako kwa kweli kulijibu kwa haraka ni swali ngumu sana. Nitaomba uwasiliane na Mheshimiwa Naibu Waziri ili muweze kusaidiana.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali linalofuata. Lakini leo kwa kweli ni *challenge* kwa wimbo huo na nadhani Wizara yetu ya Habari, Utamaduni na Michezo inatakiwa kufanya kazi ya ziada kwenye eneo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma ,Mbunge wa Kalenga na linaenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 161

Fedha za Ruzuku Kwa Bodi za Mazao

MHE. STEPHEN J. GALINOMA aliuliza:-

Kwa kuwa, kwenye Bajeti ya mwaka 2007/2008 karibu Bodi zote za mazao ya kilimo zilipewa fedha chini ya mahitaji yao kwa kiwango cha kuzifanya zishindwe kutekeleza majukumu zilizopewa na Serikali. Kwa mfano Bodi ya Tumbaku iliomba sh. 1,066/= milioni lakini ikapewa sh. 310m/= ambazo hazikidhi shughuli za ununuzi wa Tumbaku, msimu utakapoanza mwezi Mei, nayo Bodi ya Pareto iliomba shs. 1,557 milioni lakini ikapewa sh. 250 milioni tu sawa na asilimia 16 (16%) uamuzi huo ulifanywa na Serikali ili kuinua bei ya mkulima kwa kuzingatia ushuru mbalimbali lakini ni wazi kwamba Bodi hizo hazitawenza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.-

Je, Bodi hizo zitatekelezaje majukumu yake ikiwa Serikali inazipa majukumu bila kuzipa uwezo wa kifedha kwa kutozipa ruzuku au uwezo wa kutoza ushuru?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Ili kumwongezea mkulima kipato kutohana na mauzo ya mazao yake, mwaka 2006/2007 Serikali ilianza kutekeleza urazinishaji wa majukumu, miundo na ugharamiaji wa Bodi za mazao kwa kufuta ushuru wa mazao (*crop levy/cess*) ambao ulikuwa unatumika kugharamia Bodi hizo na badala yake Serikali ilianza kugharamia moja kwa moja shughuli za usimamizi na uendeshaji wa Bodi hizo.

Aidha, jukumu la kuhamasisha uzalishaji (*Promotional Role*) linalofanywa kwa pamoja na wadau mbalimballi zikiwemo Halmashauri za Wilaya na inapaswa kugharamiwa kwa pamoja kuitia vyanzo mbalimbali nya fedha kwa mfano mifuko ya kuendeleza mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Galinoma kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika mwaka 2007/2008 Bodi za Mazao zilipata fedha kiasi pungufu ya kile kilichoombwa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Serikali iliweza kuzitengea Bodi hizo kiasi cha shilingi bilioni 2.47 ikilinganishwa na mahitaji ya shilingi bilioni 4.94. Katika mwaka wa 2008/2009 Serikali imetenga shilingi bilioni 3.98 sawa na ongezeko la asilimia 61.13. Kutokana na ongezeko hilo Bodi ya Pareto imetengewa shilingi milioni 450 ikilinganishwa na shilingi milioni 250 za mwaka jana na Bodi ya Tumbaku imetengewa shilingi milioni 500 ikilinganishwa na shilingi milioni 310 za mwaka jana. Hata hivyo pamoja na ongezeko hilo, fedha zilizotengwa bado hazitoshelezi mahitaji. Serikali itaendelea kujitahidi kutenga fedha zinazowezesha Bodi za Mazao kuendesha shughuli za msingi kila inapoweze kana kwa jinsi Bajeti itakavyoruhusu.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwanza nimshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri ya kweli kabisa ambayo nafikiri yanaonyesha kwamba yeche na sisi tunaouliza maswali haya tuko pamoja. Lakini ningependa nizungumze kidogo kwamba athari ya ufinyu wa bajeti ni kubwa, kwanza itakiuka Sheria za Masoko ya Tumbaku ambazo tumepangiwa na pili ubora wa tumbaku katika zao hili zima litapungua na tukikumbuka kwamba zao hili ni *international* la Kimataifa. Serikali inasemaje juu ya athari ambazo zitatokana na ukosefu wa ubora wa tumbaku unaotokana na ufinyu wa Bajeti?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua tatizo linaloweza kutokea kutokana na ufinyu wa Bajeti. Ndiyo maana katika mwaka unaofuata ili kurekebisha hali hiyo tumeongeza hali bajeti hii kupunguza athari yoyote inayoweza kuyapata mazao hayo kutokana na usimamizi hafifu.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa lengo la Serikali la kutoa ruzuku lilikuwa kwanza kuongeza bei kwa wakulima lakini vile vile Bodi zisitegemee wakulima. Na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anajibu hapa inaonekana wazi kabisa kwamba Serikali imeshindwa kukidhi haja ya kuhakikisha Bodi zinajitegemea kwa asilimia 100 kama zilivyokuwa zinafanya huko awali. Sasa Waziri anaweza kusema nini, lengo la Serikali limetimia au limeshindwa kutimia?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kwa kawaida, malengo huwa ni ya muda mrefu na yanaweza yakawa

yanatimia hatua kwa hatua. Mpaka hivi sasa bado hayajatimia lakini jitihada ni kuyafanya yatimie kadri tunavyoendelea.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa Wizara hiyo bado haijasoma hotuba ya Bajeti, tutaendelea na Wizara hiyo huko mbele. Lakini nimwite Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage na yeze ana swali linakwenda Wizara hiyo hiyo pia.

Na. 162

Kuwakwamua Wakulima Vijijini

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne ina mikakati mizuri ya kuwainua wananchi wake kwa kuboresha sekta ya kilimo ambacho ndicho uti wa mgongo wa Taifa:-

- (a) Je, Serikali inawasaidiaje wakulima kujikwamua kupitia mazao yao?
- (b) Je, Serikali itaboresha lini kilimo cha umwagiliaji na kupeleka wataalamu wa kilimo kwenye Wilaya za Karagwe, Ngara, Biharamulo na Bukoba Vijijini?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Savelina Mwijage (Viti Maalum) lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawasaidia wakulima kujikwamua na umaskini kupitia mazao yao kwa kuwasaidia kuongeza tija na uzalishaji wa mazao kwa kuimarisha huduma za ugani, mifumo ya upatikanaji usambazaji pembejeo, kuimarisha huduma za ushirika, masoko ya mazao pamoja na kurekebisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuwekeza katika Kilimo kupitia Mpango wa Sekta ya Kilimo (ASDP). Aidha, ili kupunguza uharibifu wa mazao kutohana na visumbufu vya mimea na mazao, Serikali imekuwa ikitenga wastani wa shilingi milioni 700 kila mwaka kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao ikiwa ni pamoja na ndege waharibifu, nzige, viwavijeshi na panya. Wakati huo huo, Serikali imeendelea na mpango wa kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu na miche bora pamoja na madawa.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) imeainisha bayana uendelezaji wa kilimo cha Umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs). Hivyo, azma ya Serikali ni kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwa kuibua miradi huko Wilayani na hatimaye kupatiwa fedha za utekelezaji. Mkoa wa Kagera umefanyiwa upembuzi yakinifu kwa miradi ya Buhangaza na Buyaga Wilaya za Muleba, Buchurago, Kyaka, Gera na Kajunguti Wilayani Bukoba Vijijini, Skimu za *Mwisa Valley*, Ushuhuda

Wilayani Biharamulo na Skimu ya Nkono-Ikamba Wilayani Bukoba. Utekelezaji huu ni moja ya mikakati ya Serikali ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wataalamu linaendelea kushughulikiwa kati ya Wizara na Halmashauri ambapo mpango unaendelea wa kuajiri maafisa ugani. Kama ilivyo kwa maafisa ugani. Halmashauri za Wilaya za Karagwe, Ngara, Biharamulo na Bukoba Vijijini zinashauriwa kutenga Bajeti kwa ajili ya kuajiri wataalamu wa umwagiliaji.

Aidha, Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji ya Mwanza itaendelea kutoa msaada wa kitaalamu katika fani ya umwagiliaji kwenye Wilaya za Mkao wa Kagera.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Mkao wa Kagera toka zamani wamezoea kutumia mbolea ya kienyeji inayoitwa samadi. Mbolea ya kitaalamu wanasema kwamba inaharibu sana udongo hawawezi wakapanda kitu chochote kikaota kwa sababu udongo umeshaharibika. Je, Serikali inawasaidiaje wakulima wa Kagera kuhusu mbolea yao ya kienyeji waliyokuwa wanatumia toka zamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mito mingi ya Kagera kama nilivyosema swali la msingi sijaona sehemu yoyote ambako Serikali imesaidia angalau kuwasaidia wakulima kuwaelekeza kupata kilimo hicho, eeh nikiuliza swali hapa linalekezwa Manispaa au Halmashauri. Je, ni lini hiyo Serikali itaisaidia Halmashauri kipato kingine kuongezea ili kupata wataalamu wa kuwasaidia mkoa mzima?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kutumia mbolea ya samadi ni jambo jema sana. Watu wanaotumia mbolea ya samadi kwa kawaida ni wale amba wako karibu na ile samadi, kwa sababu Serikali haiwezi kuhamisha samadi kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Lakini samadi kama ipo pale pale inapatikana katika eneo hilo kama inavyopatikana katika mikoa yote ya wafugaji ni jambo jema sana wafugaji wakatiwa moyo ili waendelee kutumia samadi badala ya kutegemea mbolea ya viwandani ambayo haipatikani kwa wingi. Ningependa kutumia nafasi hii kuwaomba wananchi wa Kagera kama wanayo samadi waendelee kuitumia. Pili, ningependa kumsaidia Mheshimiwa Mbunge na kuwasaidia wananchi wa Kagera kwamba mbolea ya chumvi chumvi inaharibu ardhi hii sio kweli. Hilo ni jambo ambalo limesemwa sana lakini halina ukweli. Kinachosemwa hapa ni kwamba ili mbolea isiweze kuharibu ardhi lazima uweke mbolea kulingana na kipimo cha kitaalamu kinachotakiwa. Kwa hiyo, tunawataka wataalamu wawasaidie wananchi wa Kagera kuwaelekeza ni kiasi gani cha mbolea kinachowekwa katika shamba bila ya kuathiri ardhi yao.

Swali la pili, kwamba hakuna umwagiliaji katika Mkao wa Kagera. Upo umwagiliaji ingawa haujawa mkubwa sana katika Wilaya ya Misenyi kwa mfano, mimi nimewahi kutembelea mradi wa umwagiliaji amba umetekelizwa na Serikali na unawashirikisha wakulima wadogo. Lakini unahitaji kuimarishwa na Bajeti yake ya

kuimarisha inapitia katika Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi. Kwa hiyo upo umwagiliaji, lakini ningependa vile vile kusema nadhani ni vizuri fedha ambazo zinapelekwa Wilayani sababu ndio mfumo wenyewe tuliokulaliana kwamba Bajeti ya utekelezaji wa *ASDP* inatekelezwa kuititia Wilaya na Bunge hili wakati Waziri Mkuu anawasilisha hoja hapa imepitisha fedha na zipo katika jedwali la Ofisi ya Waziri Mkuu zinaonyesha kila Wilaya fedha kiasi gani zimepelekwa kwa ajili ya *investment* katika kilimo ambazo zinastahili kutumika kwa ajili ya umwagiliaji maji. Katika Serikali hakuna fedha inayobaki maana yote inapelekwa kule Wilayani.

MWENYEKITI: Majibu yamekuwa marefu sana. Na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri bado hajasoma hotuba yake kama nilivyosema nadhani hiyo ni changamoto wakati atakaposoma hotuba yake hapa Bungeni halafu tunaweza tukapata majibu ambayo ni ya kina zaidi. Ninaomba tuendelee Waheshimiwa Wabunge. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum na yeze swali lake analielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mkiwa tafadhali.

Na. 163

Ziara za Wabunge Katika Maeneo ya Utalii

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya nchi zinazoendesha shughuli za utalii mapato makubwa huwa yanatokana na utalii wa ndani, kinyume na ilivyo hapa Tanzania; na kwa kuwa, Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuwa Mabalozi wazuri wa kukuza utalii wa ndani na kuongeza pato la Taifa. Je, Serikali iko tayari kuwaandalia Waheshimiwa Wabunge ziara za kutembelea vivutio vya kitalii na kuwapatia nyenzo nyingine ili iwe ni chachu ya kutangaza utalii na kukuza uchumi wa nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: Serikali kwa kutambua umuhimu wa kukuza na kuendeleza utalii wa ndani, imechukua hatua za makusudi kabisa kuweka viwango vya chini vya kuingia katika maeneo ya vivutio vya utalii, ili wananchi waweze kuvimudu. Mathalan ikilinganishwa na wageni wengine, Watanzania hulipa viwango nafuu kuingia katika hifadhi zetu za Taifa, kama ifuatavyo:-

JINA LA HIFADHI

**VIWANGO KWA
VIWANGO KWA WAGENI
WATANZANIA**

Serengeti na
50 (watu wazima)
Kilimanjaro
(watoto)

Tshs. 1,500 – (watu wazima)

USD

Tsh. 500 –(watoto)

USD

10

Arusha, Tarangire (watu wazima) na L. Manyara	Tsh. 1,500 – (watu wazima) Tsh. 500 – (watoto) <i>USD 10</i> (watoto)	<i>USD</i>	<i>35</i>
Katavi, Mikumi, <i>20</i> (watu wazima)	Tsh.1,000 –(watu wazima)	<i>USD</i>	
Ruaha, Rubondo (watoto) na Udzungwa	Tsh. 500 – (watoto)	<i>USD</i>	<i>5</i>
Gombe wazima)	Tsh. 1,500 –(watu wazima)	<i>USD</i>	<i>100</i> (watu
USD 40	TSh. 500 – (watoto)	<i>USD 20</i> (watoto) <i>Expartriates</i>	(watu
Wazima) na <i>USD 20</i> (watoto)			
Mahale wazima)	Tsh. 1,500 – watu wazima)	<i>USD</i>	<i>80</i> (watu
wa	Tsh. 500 – (watoto)	<i>USD</i>	<i>30</i> (watoto) <i>Wataalam</i>
<i>USD40</i> (watu wazima) na <i>USD</i> <i>10</i> (watoto)			<i>Kigeni</i>

Naomba nichukue fursa hii kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge kutembelea maeneo yetu ya utalii ili waweze kutusaidia kuhamasisha zaidi wananchi, hivyo kukuza uelewa wa hazina tuliyonayo na kuchochaea ulinzi na uhifadhi wa maeneo hayo. Aidha, kwa njia hii tutakuza utalii wetu wa ndani. Wizara yangu kwa ushirikiano na taasisi zake itaendelea kutengeneza na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge majarida, vipeperushi na nyenzo nyingine za utangazaji utalii mara kwa mara ili waweze kuvitumia kuhamasisha utalii wa ndani kwenye majimbo yao.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa vivutio vingi nya kitalii viko mbali na makazi ya wananchi. Na kwa kuwa kuvifikia vituo hivyo kunahitaji gharama kubwa ya usafiri ambayo wananchi wengi wameshindwa kuimudu gharama hiyo. Je, Serikali iko tayari kuandaa magari kwa gharama nafuu ili wananchi wengi waweze kuvifikia vivutio hivyo. Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amewahamasisha Wabunge kutembelea mbuga na vivutio nya kitaifa. Je, Wizara ya Maliasili na Utalii iko tayari kuwapangia Wabunge safari za kupanda Mlima Kilimanjaro kwa awamu ili waweze kushuhudia na kuweza kutangaza utalii kwa makini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ingawa wazo hili ni la kimsingi kabisa sijui tutaweza kweli? Lakini ebu Naibu Waziri utujibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu kwamba vivutio viko maeneo ambayo ni mbali na wananchi. Kwa kiasi hiyo ni kweli lakini pia inawezekana kwamba kuna maeneo mengine yako karibu na wananchi. Kwa mfano vivutio tulivyonavyo si mbuga za wanyama peke yake ni pamoja kwa mfano na mambo ya Kale, maeneo ya kihistoria. Sasa kwa mfano Makumbusho ambayo pia ni vivutio vyatya utoo iko pale pale Dar es Salaam ukiuliza ni Watanzania wangapi wametembelea ni wachache sana. Kwa mwaka 2006 ni Watanzania 100,022 pekee walitembelea wakati Dar es Salaam ina watu milioni 4 sasa utasema kweli na Dar es Salaam kufika pale Makumbusho kunahitaji kutoa magari. Kwa maeneo ambayo yako mbali tumekuwa tukishirikisha sekta binafsi ambayo ni usafiri wa *public* kwa ajili ya kusafirisha wageni na viwango hivyo vinamilikiwa na kuendeshwa na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Waheshimiwa Wabunge kupanda mlima Kilimanjaro. Naomba kusema hili wazo ni zuri sana na sisi kama Wizara tuko tayari isipokuwa tuombe tu kwamba Wabunge wajipange na wapo wengi amba wamekuwa wakipanga taratibu hizo. Kwa mfano hivi karibuni Kampuni ya Geita *Gold Mine* imekuwa ikiratibu kila mwaka wananchi kupanda Mlima Kilimanjaro na sisi tumekuwa tukishirikiana nao. Kwa hiyo, hata Bunge likitaka kufanya hivyo sisi tuko tayari kushirikiana. Kwa hivyo tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge kupanda mlima huo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niuliza swali moja la nyongeza.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri sana na ni swali ambalo kwa kweli linahamasisha wananchi wote na sisi pia linatusaidia katika kazi kwenye Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa utoo wa ndani umekuwa ni kivutio kikubwa na nchi mbalimbali na sisi wenye tumejionea katika kutembelea huko kuona wenzetu jinsi ambavyo utoo wa ndani ndio mkubwa zaidi na ndio wengi wanaokwenda katika sehemu mbalimbali kuona utoo huo. Sisi hapa tuna mpango kabambe amba tutashirikisha Makampuni mbalimbali ya binafsi na Makampuni ya vyombo vyatya usafiri na Makampuni yanayoshughulika na kutembeza watalii ili tuweze kuwa na mpango maalum wa kuwezesha wananchi wa Tanzania nao waweze kupata fursa hizi za kwenda kutembelea. Huu ni mpango wetu mpya ni mpango amba tumejipanga kwa makini tutaushughulikia.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Salim kwa kuwa nilishamwita ebu nimpe nafasi aulize swali la mwisho la nyongeza.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ili kufika kwenye mbuga za watalii inahitajika usafiri, chakula na malazi. Kwa kuwa kipato cha Mtanzania ni chini ya shilingi 1,000/= kwa siku. Je, kiwango hiki cha shilingi 1,500/= bado ni kikubwa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango nya shilingi 1,500/= ni viwango ambavyo viliwekwa miaka mingi iliyopita, zaidi ya miaka mitano. Kwa sasa hivi tulitegemea kwamba tungeweza kuvi-revise viendane na gharama halisi ya uendeshaji, lakini tumeacha kufanya hivyo kwa makusudi kabisa ili kuwawezesha wananchi wengi waweze kutumia fursa hiyo. Aidha, katika maeneo hayohayo ambayo ni ya mbuga pia kuna *accommodation facilities* ambazo kwa kweli *rates* zake ni chini sana. Kwa mfano wanafunzi ni bure kutumia hosteli ambazo ziko kwenye mbuga zetu za wanyama. Kwa hiyo yote hii ni kuhamasisha wananchi waweze kutumia huduma zetu.

Na. 164

Upungufu wa Askari wa Wanyamapori Liwale

MHE. HASSAN C. KIGWALILO aliuliza:-

Kwa kuwa, mionganoni mwa kero kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Liwale ni upungufu wa askari wa wanyamapori (*Game scouts*) wa kudhibiti wimbi kubwa la wanyamapori wanaohatarisha maisha ya wananchi na kuharibu mazao mbalimbali kama vile Mahindi, Mtama, Korosho na kadhalika; na kwa kuwa, jitihada za kuajiri askari wanyamapori wenyе Stashahada (*Diploma*) ya Chuo cha Mweka ni kikwazo kikubwa kwa ajira hizo:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulegeza sharti hilo kwa muda ili kukidhi mahitaji, na je, kuna vyuo vingapi vinavyotoa taaluma hiyo na hutoa askari wangapi kwa mwaka?
- (b) Je, ile mbinu mbadala ya kutumia pilipili na tumbaku inayotumiwa na *WWF* kwa kushirikiana na wananchi kwa lengo la kupunguza mgongano kati ya wananchi na Ndovu imesaidia kwa kiasi gani?
- (c) Je, Serikali inaweza kutoa mwongozo/utaratibu ulio wazi wa jinsi ya kupata kifuta machozi kwa waathirika wa wanyamapori ili kupunguza usumbufu kwa wafuatilaji?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Kutokana na mazingira ya kazi ya kukabiliana na majangili na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu, ni dhahiri kuwa watumishi wenyе sifa na uwezo wa kitaaluma na kutumia silaha wanahitajika. Hivyo ni muhimu kuwa na watumishi hao ambaо wamepatiwa mafunzo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inasimamia vyuo viwili ambavyo vinatoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori, vyuo hivyo ni:-

(i)Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasansi Mwanza, ambacho hutoa cheti cha awali cha uhifadhi (*Basic Certificate in Wildlife Management*). Chuo kina uwezo wa kutoa wanafunzi 95 kwa mwaka.

(ii)Chuo cha Usimamizi Wanyamapori Mweka, Moshi, ambacho kinatoa Astashahada, Stashahada na Stashahada ya Juu (*Advance Diploma, na Post Graduate Diploma*). Chuo kina uwezo wa kutoa wahitimu 120 kwa mwaka.

(b)Mbinu mbadala ya kutumia pilipili na tumbaku inayotumiwa na *WWF* Wilayani Liwale na Kilwa imeonyesha mafanikio kwani tangu ilipoanza kutumika mwaka 2005, idadi ya matukio ya tembo ya kushambulia mazao ya wananchi imekuwa ikipungua.

Kwa mfano, mwaka 2003/2004 kwa Kata tatu za Mpigamiti, Barikiwa na Mkutano, kulikuwa na matukio 380. Katika mwaka 2004/2005 matukio yalipungua na kufikia 185 na mwaka 2007/2008 ni matukio 26 tu yaliyoripotiwa.

(c)Utaratibu wa kupata kifuta machozi kwa waathirika wa wanyamapori ni kama ifuatavyo:-

Taarifa ya uharibifu hutolewa Wilayani kupitia uongozi wa vijiji. Wilaya hufanya uhakiki wa kiwango cha uharibifu na kuandaa taarifa ambayo huwasilishwa Wizarani kwa ajili ya malipo. Baada ya hapo malipo hufanyika kupitia Halmashauri ya Wilaya husika.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ambayo yanawashangaza wananchi wa Liwale.

Kwa kweli Liwale yenyewe kiasili tunaishi na wanyama na sio wananchi wote wa Liwale wamekwenda shule. Inashangaza leo hii kuwadhibiti wanyama kitu ambacho kilikuwa kinawezekana na wananchi leo hii inatakiwa watu wenye diploma na stashahada. Hivi ni kweli wanyama hawa wamekwenda shulen iku hizi?

Pili, wakati wa msimu wa uwindaji baadhi ya wawindaji Makampuni hayo uwaahidi wanakijiji kuwafanya miradi mbalimbali katika vijiji hivyo vinavyohusika na maliasili. Lakini mara tu uwindaji ukiisha wanaingia mitini hawapatikani kwa simu na ile miradi huwa haifanyiki tena. Kwa vile wanadanganywa na Serikali inajua hilo mwaka huu iko tayari Serikali kuzuia uwindaji katika Wilaya ya Liwale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Wanyama nao wamesoma?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kusema kwamba kwa ajili wanyama hawa kuna baadhi ya wanyama ni wanyama hatari na kuna baadhi ya wanyama waharibifu na hali hiyo basi na jinsi dunia inavyokwenda tunaona kwamba lazima tutumie mbinu za kisasa za kuweza kuwakabili hawa wanyama kuliko kuwaachia wananchi wapambane na wanyama. Kwa sababu wananchi ni binadamu na zile ni roho tusingependa maisha ya mtu yapotee huku Serikali tumekaa pembedi ndiyo sababu tumeona kwamba hilo ni jukumu letu na sisi tutatumia kila aina ya utaalam kuweza kuwalinda wananchi wetu.

Katika swali lake la pili la kuhusu hawa wawindaji wanapokwenda kule wanatoa ahadi na baada ya hapo wakishawinda hawatoi hizo ahadi. Napenda kusema kwamba hilo ni tatizo ambalo tunalifahamu sana na ni tatizo ambalo tumejaribu kila sehemu kwenda kulitazama. Lakini naomba kwamba wananchi wahusika katika hivyo vijiji pindi ambapo mwindaji au mwekezaji wa aina yoyote anapokwenda wasikubali wenyewe kupewa ahadi za mdomo ila watumie wataalamu wao Wanasheria wao kwenye Halmashauri, hizi ahadi ziandikwe kimaandishi ili ziwe halali. Wengi wanafanya mikataba ya kienyeji wenyewe na hawa wawindaji na wawindaji ndiyo maana yake wanawatoroka. Naomba Halmashauri za Wilaya zitusaidie katika jambo hilo. Ahsante.

Na. 165

Kituo cha FFU cha Matangatwini Kupatiwa Umeme

MHE. DR. ALI TAARAB ALI aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha *FFU* kilichopo Matangatwini Jimbo la Konde hakina umeme, na kuwa kituo hiki kipo mita mia tano (500m) tu kutoka kituo cha kilimo ambapo kuna umeme kwa wingi na kuna transfoma:-

Je, ni lini kituo hicho cha *FFU* kitaunganishiwa umeme kutoka kwenye transfoma iliyopo kwenye kituo cha kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijbu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Matangatwani ni eneo ambalo lilikuwa likitumiwa na Kikosi cha Kutuliza Ghasia (*FFU*) kama kambi ya muda (*detach*) lakini kwa sasa kambi hiyo imehamishiwa katika eneo la Finya. Mpango wa Jeshi la Polisi ni kujenga Kituo cha Polisi katika eneo la Matangatwani na kukarabati nyumba zilizopo ili ziweze kutumika kwa makazi ya askari watakaopangwa kufanya kazi katika kituo cha

Matangatwani. Kwa sasa Jeshi la Polisi haliwezi kuweka umeme katika kituo hicho mpaka hapo ujenzi wa Kituo cha Polisi utakapokamilika sambamba na ukarabati wa nyumba hizo.

MHE. DR. ALI TAARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na jawabu la kukatisha tamaa la Mheshimiwa Waziri nilitaka kusema kituo hicho si cha muda kimeanza tangu miaka ya 1960. Pili, lindo hilo linalofanyika na askari wetu hapo usiku linatumia taa za kandili. Na kwa kweli kwa mujibu wa tathmini ya Shirika la Umeme Zanzibar tawi la Pemba kuunganisha umeme kutoka kituo cha Kilimo mpaka hapo kutuo cha *FFU* ni shilingi milioni 7.5. Je, hiyo isingekuwa ni faraja kwa wananchi wa Kijiji cha Matangatwani na askari wetu kuunganisha umeme hivi sasa?

Swali la pili, hicho Kituo cha Polisi ambacho kinakusudiwa kujengwa katika kijiji cha Matangatwani ni lini kituo hicho kitajengwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge asikate tamaa na haikuwa azma yangu kumkatisha tamaa kwa jibu ambalo nimelitoa isipokuwa nimejibu kwa ukweli wa mambo ulivyo kwamba pale kweli kulikuwa na Kituo cha *FFU* na uamuzi umefanyika kuhamisha kituo hicho na pale sasa itakuwa ni makazi ya Kituo cha Polisi; na kwa kuwa Polisi wanafanya utaratibu wa kujenga na kukarabati majengo yaliyopo pale, ni wakati huu shughuli hii itakapokuwa inafanyika basi na umeme utaunganishwa katika majengo haya. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa asiyachukulie majibu haya kama yakumkatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwamba ni lini kituo hicho kitajengwa, ni kwamba kituo hicho na vituo vingi nchini ambavyo tumeviombea pesa katika bajeti ya mwaka huu, napenda kumwambia kwamba hatukuweza kupata fedha zote kama tulivyozionba. Lakini tutatizama kadri tutakavyokuwa tunapata na bajeti ikitiruhusu basi tutafanya hivyo. Lakini namwomba Mheshimwa Mbunge avute subira na wala asikate tamaa. Azma ipo na nia ya kufanya hivyo ipo.

Na. 166

Kuongezeka kwa Wizi na Ujambazi Nchini

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa suala la wizi na ujambazi limekithiri sana hapa nchini; na kwa kuwa wakati mwingine wezi hao huwa wanatumia silaha au nguo za vyombo vyatundu ili wasiweze kutambuliwa na raia:-

- (a) Je, ni Sheria gani zimechukuliwa kwa waliowahi kukutwa na uhalifu wa aina hiyo?
- (b) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili kuwa wahalifu hao hupata wapi nguo hizo?
- (c) Je, kwanini uhalifu bado unaendelea kufanyika nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mhalifu yejote anayekamatwa kwa tuhuma ya wizi wa kutumia silaha, hushitakiwa kwa kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania. Aidha atashitakiwa kwa kosa la kupatikana na silaha na sare za vyombo vya Ulinzi na Usalama iwapo wakati anakamatwa atapatikana na vifaa hivyo. Adhabu ya juu endapo atapatikana na hatia ya kosa la wizi wa kutumia silaha ni kifungo cha miaka 30 jela pamoja na viboko.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, nguo zinazosadikiwa kufanana na sara za Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama, hazitoki katika maghala ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi, umebaini kwamba nguo hizo zinazofanana rangi na sare za vyombo Vyetu vya Ulinzi na usalama, hushonwa kwa kutumia vitambaa vinavyofanana rangi na sare hizo au kutoka kwenye maduka ya mitumba. Kwa mfano, ni jambo la kawaida katika nchi za Ulaya na Marekani kuwaona raia barabarani wamevaa kama fasheni sare za Kijeshi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za jumla na zilizo mahsusizi zinazochangia kuendelea kufanyika kwa uhalifu nchini ni pamoja na:-

- Uingiaji holela wa silaha kutoka nchi jirani;
- Uingiaji nchini holela wa wakimbizi na wahalifu wengine kutoka nchi jirani zinazotuzunguka;
- Kuibuka kwa mitambo ya uhalifu inayoshirikisha nchi na nchi;
- Kukua na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya kisasa mionganini mwa wahalifu kama vile mitandao ya simu, *internet* na kadhalika; na
- Vilevile tabia ya kuweka fedha nyingi nyumbani badala ya benki na mazoea ya kufanya malipo ya huduma mbalimbali kwa kutumia fedha taslimu, nayo huchangia kutoa mwanya na fursa ya uporaji.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninalo swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mara nyingi yanapotokea masuala ya wizi au ujambazi na wananchi wanapochukua juhudi za haraka kuvijulisha Vituo vya Polisi vilivyokaribu nao, imejengeka tabia kwa baadhi ya Askari hucheleva kuchukua hatua za haraka kufika sehemu husika ili kudhibiti hali hiyo na wakati mwingine hufikia kuua, kujeruhi au wananchi kuchukua sheria mikononi mwao. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa vituo vitakavyohusika na uzembe wa aina hiyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli zimekuwepo *cases* ambazo zimeletwa kuhusu Maaskari kufika kwenye tukio kama aliviyotamka lakini hii ninaomba izingatiwe kwamba Askari wetu kwa kweli wanajitahidi na tumekuwa na uhaba wakati mwingine wa vitendea kazi na hili ni jambo ambalo tumekuwa tunalisema mara kwa mara. Lakini hili lisichukuliwe kama uzembe upande wa Maaskari isipokuwa ni matatizo ya vitendea kazi ambavyo tumekuwa navyo. Lakini naomba niseme kwamba jitihada kubwa zimekuwa zinafanyika kwa Askari wetu kuweza kufika sehemu za matukio na kuweza kuchukua hatua zinazostahili kuchukuliwa katika kunusuru watu, mali zao na kadhalika na wakati mwingine kuwakamata majambazi.

Kuhusu suala la pili la wananchi kuchukua sheria mikononi mwao, ninasema kwamba hili ni jambo ambalo Serikali imekuwa inalisema mara kwa mara. Najua kweli wakati mwingine wananchi wamekuwa wanakata tamaa lakini Sheria lazima iwe ni Sheria na kwa kweli tunasema kwamba wananchi wasichukue Sheria mikononi mwao na Serikali bado haijachoka wala haijashindwa. Jitihada zinafanyika siku zote kuzingatia matukio haya na kuchukua hatua ambazo zinastahiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, shughuli za Maswali na Majibu kwa ratiba ya leo asubuhi imekamilika.

Baada ya kumaliza ratiba hiyo ya mswali, nitaomba nichukue nafasi hii niwatambulish wageni amba wako nasi hapa leo.

Kwenye eneo la wageni la Spika, wote tunafahamu kwamba tunacho chombo chetu ambacho kinatambulika kama *Tanzania Center for Democracy* na chombo hiki kinajumuisha Wenyeviti na Makatibu wa Vyama vyote vya Siasa vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini Mwenyekiti wa *Center* hiyo ni Mheshimiwa John Momose Cheyo ambaye ni Mbunge na labda ninamwomba Mheshimiwa Cheyo asimame kwa sababu ameniomba anitambulish wageni wake na kwa heshima ya Uwenyekiti basi ungesimama tu kwa dakika moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Cheyo, ameomba nitambue uwepo wa Wenyeviti na Makatibu Wakuu wa Vyama Vyote vilivyo na Uwakilishi Bungeni na Viongozi hao ni

Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba, Mwenyekiti wa Chama cha CUF, Mheshimiwa Agustine Lyatonga Mrema, Mwenyekiti wa Chama cha TLP, Mheshimiwa Pius Msekwa, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Katibu Mkuu wa CHADEMA, Mheshimiwa Seif Shariff Khamad, Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, Mheshimiwa John Komba, Katibu Mkuu wa TLP, huyu si Capt. John Komba wa CCM, Mheshimiwa John Nkorro, Katibu Mkuu UDP na naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Yusuf Makamba ingawa yumo humu ndani na yeye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba msiutafune muda wangu tuendele. Naomba nimirambulisha sasa Mkurugenzi wa Kituo hicho na yeye anaitwa Mheshimiwa Daniel Loya lakini wameongozana na *Technical Committee* ya *TCD*, sasa wale Wajumbe wa Kamati hii, naomba wote wasimame kwa umoja wao. Karibuni sana, Mheshimiwa Mwenyekiti, John Momose Cheyo tunakuomba uongoze vizuri chombo chetu, tunaamini kitaleta msaada mkubwa katika maendeleo ya demokrasia katika nchi yetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima kabisa leo pia tumefikiwa na wageni kutoka Jimbo la Gauteng kutoka Afrika Kusini na wanaongozwa na Komredi Nakutura Sikakhane, yeye ni *Deputy Chief Whip*. Pia yupo Komredi Sipho Makama, yeye ni *Protocol Chief Whip Officer*, pia wapo Komredi Mbeki Nkosi na Komredi Mbongeni Ladebe. Waheshimiwa majina ya Wangoni wenzangu hawa ni kiboko kweli. (*Makofi/Kicheko*)

Pia kuna Komredi Regina Dladla, Komredi Femie Maseko, hili rahisi hata kule Ungonini wapo wa kina Maseko. Tunaye Komredi Thuran Matathi. Ahsante sana. *We are very much happy for your presence in our house and we wish you safe and good stay in our country.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, anaomba kumtambulisha Bibi Adelina Kamala, ambaye ni mke wake lakini ameambatana na wadogo zake wawili God Mkwaruzi na Frank, wadogo wa Mheshimiwa Kamala, sijui wamekaa wapi. Tunakupongeza sana mama Adelina, tunafikiri unafanya kazi kubwa sana ya kumtia moyo na nguvu Dr. Kamala katika kufanya kazi yake vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wageni kutoka Afrika Kusini lakini tunao Waheshimiwa Wabunge wa Afrika Mashariki ambao sisi ndiyo wapiga kura wao kwa hiyo wapo Jimboni kwao na wamekuja kusikiliza hotuba hii ya Wizara ya Afrika Mashariki nao ni Mheshimiwa Janeth Deo Mmari na Mheshimiwa Gharib Bilali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea na wageni wengine labda nitangaza kabisa matangazo ya kazi.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 4/7/2008, saa

tano asubuhi kutakuwa na Mkutano katika Ukumbi, namba 227, ghorofa ya pili, jengo la utawala.

Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na yeye ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa tano asubuhi katika chumba namba 219, ghorofa ya pili, jengo la utawala, kutakuwa na kikao.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na yeye ameniomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa mukutano wa Kamati, ukumbi namba 428, ghorofa ya nne, jengo la utawala. Leo kazi kweli kweli sijui humu ndani tutafanyaje?

Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao ukumbi namba 231, jengo la utawala kukagua hesabu za *TBC*.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwanza anaomba kumkaimisha shughuli za Kamati leo Makamu wake Mheshimiwa Haroub Masoud na anaomba Makamu Mwenyekiti aendeshe Kikao cha Kamati hiyo leo saa tano asubuhi kwenye ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, saa saba mchana Wajumbe wa Kamati ya Tafrija, watakatana katika Mkutano mfupi, ukumbi namba 133, ghorofa ya kwanza, jengo la utawala, saa saba mchana.

Ninaomba niwatangazie tangazo lingine kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Spika ambalo ni la Mwaliko kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara amewaalika kwenye Maonyesho ya Sabasaba yatakofanyika kwenye kilele chake siku ya Jumatatu tarehe 7/7/2008 Jijini Dar es Salaam. Tafadhali Wabunge watakaokuwa tayari kuhudhuria wajiandikishe mapokezi, jengo la utawala ili utaratibu wa usafiri uandaliwe kwa ajili ya kusafiri Jumamosi tarehe 5/7 mwaka 2008.

Lakini nimepata pia tangazo lingine, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, amesisitiza wale watakaopenda kupanda Mlima Kilimanjaro, wawasiliane na Wizara lakini yeye ana uwezo wa kusaidia kuandaa safari hizo.

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao hapa leo ni Wageni wa Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mzee James Wambura ambaye ni Baba yake Mzazi, Bwana Laurent Paul, Mume wake Mheshimiwa Anastazia na Bi. Melania Laurent mtoto wake, karibuni sana. (*Makofî*)

Wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, ni Konjeta Chembira kutoka Ukaguzi Kanda ya Kati na Benadeta Kabasi, kutoka Ofisi ndogo ya Waziri wa Sheria hapa Dodoma.

Wageni wa Mheshimiwa Hafidh Ali, ni Ndugu Akiba Ramadhan, ni Mwenyekiti wa Wazazi wa Jimbo, Ali Mohamed na Ali Faki Wajumbe wa Wadi Jimbo, Ali Hifadhi, Katibu Mwenezi Tawi la CCM Nyamazi, Abdallah Mohamed, Katibu wa CCM Tawi la Fumba, Hassan Mohamed, Katibu wa Vijana Jimbo, Mariam Hassan, Katibu Mwenezi Tawi, Ndugu Sedi Ramadhan Mjumbe wa Kamati ya Siasa, Juma Khamis Mwinyi, Mzee wa Chama na Ndugu Fikiri Mohamed, Kaimu Katibu wa Jimbo la Dimani. Karibuni sana na poleni na safari ya kutoka huko Zanzibar. (*Makofî*)

Wageni wa Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, ni Zainab Zaidi na Nasra Zaidi, watoto wake.

Tunao pia wanafunzi 31 kutoka *CBE* Dar es Salaam ambao leo hii wanawaaga rasmi Waheshimiwa Wabunge na wanatarajia kuondoka kesho baada ya kumaliza ziara yao ya mafunzo hapa. Naomba wasimame, ahsante sana kwa kushirikiana nasi hapa Bungeni. Tunaomba msichoke siku nyingine pia mpange ziara kama hii inatupa moyo na inawasaidia hata nyie.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitangaze kuna mtu kasahau kalamu yake kwa hiyo nitaomba awaone Makatibu.

Tangazo lingine la mwisho la Mheshimiwa Joyce Masunga anawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kushiriki katika msiba wa baba yake na anaomba kuwaambia kwamba kesho tarehe 5 nyumbani kwake marehemu kule Kawe Ukwamani Dar es Salaam, atakuwa anahitimisha msiba huo kwa kufanya arobaini, saa nne asubuhi mpaka saa nane mchana. Kwa hiyo, anatoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Spika na kwa Waheshimiwa Wabunge wote na anaomba watakaoweza kuhudhuria anawakaribisha.

Waheshimiwa Wabunge, hapa ndiyo mwisho wa matangazo yetu ya leo na naomba Katibu atuongoze na shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 - Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Vita Kawawa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai mimi na familia yangu hadi kufika siku hii ya leo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyokuwa nayo juu yangu kwa kunitua na kunikabidhi dhamana ya kuiongoza Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia uniruhusu kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Nkenge kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu Jimboni. Naomba ushirikiano huo uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Uteuzi wake ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo kwake viongozi wa Bara la Afrika. Aidha, nampongeza kwa busara na hekima zake zilizosaidia kufikia makubaliano ya kumaliza mgogoro wa kisiasa uliotokea nchini Kenya mara baada ya uchaguzi mkuu nchini humo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kumpongeza Rais wetu kwa kufanikisha Mkutano wa Nane wa Leon H. Sullivan uliofanyika Arusha mwezi Juni, 2008. Mkutano huo ulikuwa ni jukwaa la kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo na fursa za uwekezaji nchini. Mafanikio haya yametokana na nchi yetu kuwa kisiwa cha amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais, na baadaye kuthibitishwa kwa kura za kishindo na Bunge letu Tukufu kushika wadhifa huu mkubwa. Kuteuliwa kwake na baadaye kuthibitishwa na Waheshimiwa Wabunge kunadhihirisha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais na Watanzania juu ya uwezo wake wa utendaji kazi katika kusimamia majukumu ya Serikali. Namtakia mafanikio katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukupongeza kwa kuteuliwa kwako kuwa Makamu wa Rais wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*CPA*). Uteuzi huu unathibitisha uwezo wako katika kuongoza shughuli za Bunge. Vilevile, uteuzi huo umeongeza sifa ya Tanzania katika medani ya Kimataifa. Nakutakia mafanikio katika kutekeleza jukumu hilo kubwa na muhimu kwa Tanzania na Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali. Aidha nampongeza Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mkuu wa Mkoa wa Pwani na Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Al Shaymaa Kwegyir kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Benedicto Ole Nangoro kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kiteto. Nawatakia heri katika kutekeleza majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishukuru kipekee Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Wilson

Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, kwa ushauri na maoni waliyotoa katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2007/2008 na kujadili Makisio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2008/2009. Ushauri na maelekezo ya Kamati katika mchakato wa kuandaa Bajeti ya Wizara umeniwezesha kuwasilisha hotuba hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na marafiki kufuatia kifo cha Mheshimiwa Hayati Salome Mbatia (Mb) aliyekuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; na Mheshimiwa Hayati Benedict Kiroya Losurutia aliyekuwa Mbunge wa Kiteto. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda; na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa P. Mkulo, zimetoa taarifa muhimu kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Serikali kwa mwaka 2007/2008 na mwelekeo wa jumla kwa kipindi cha mwaka 2008/2009. Napenda niwashukuru sana kwani hotuba zao zilikuwa mwongozo mzuri katika kuandaa Bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2007/2008 na mpango na bajeti ya mwaka 2008/2009. Baada ya maelezo ya utangulizi sasa naomba niwasilishe mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Bajeti ya mwaka 2007/2008 na malengo na majukumu ya Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unazingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005; Dira ya Taifa 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Kwa mantiki hiyo, Wizara yangu ina majukumu ya msingi yafuatayo:-

- (a) Kusimamia, kuratibu na kushiriki katika utekelezaji wa Mkataba wa uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;
- (b) Kuratibu, kushiriki na kusimamia majadiliano yahusuyo ushirikiano wa Afrika Mashariki hususan Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu Moja na hatimaye Shirikisho la Kisiasa;
- (c) Kuhimiza ushiriki na uelewa wa sekta ya umma na sekta binafsi katika kutumia fursa za kiuchumi, kibashara na uwekekezaji zitokanazo na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (d) Kujenga uwezo wa Wizara na watumishi katika kutoa huduma bora kwa wadau na wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo Mkakati ya Wizara (*Ministerial Strategic Plan 2007-2010*) ambayo ndiyo mwongozo wa utekelezaji wa majukumu yake, yameainishwa kama ifuatavyo:-

- (a) Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama mojawapo ya Kanda za Ushirikiano na Taasisi za kimataifa ambazo Tanzania ni muasiyi wake;
- (b) Kujenga uwezo wa utendaji kazi katika Wizara na rasilimali watu kwa kuongeza ujuzi na vitendea kazi kwa lengo la kuongeza tija katika utoaji wa huduma; na
- (c) Kushiriki kikamilifu katika kuchangia jitihada za kitaifa za kupambana na majanga ya kitaifa na dunia nzima hususan kupunguza maambukizi ya UKIMWI na kutoa huduma bora kwa walioathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08 Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake ikiwa ni pamoja na maamuzi mbalimbali yahusuyo Jumuiya kama nitakavyoeleza katikaaya zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha, hatua ya mwanzo katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Umoja wa Forodha (*Customs Union*). Utekelezaji wa hatua hii ya mtangamano ulianza rasmi mwezi Januari, 2005. Tangu wakati huo mafanikio makubwa yamepatikana. Kwa mfano, Tanzania, Kenya na Uganda zimeweza kutekeleza ratiba ya uondoaji ushuru wa forodha kama ilivyokubalika.

Kwa sasa, hakuna ushuru wa forodha katika biashara baina ya Tanzania na Uganda; bidhaa za Kenya zinazoingia Tanzania ziligawanywa makundi mawili, kundi A na kundi B. Kundi A linajumuisha bidhaa ambazo zilioneekana kuwa hazina madhara makubwa kwa uchumi wa Tanzania na kwa hiyo hazitozwi ushuru wa forodha ziingiapo Nchini. Kundi B linajumuisha bidhaa zilizooneekana kuwa ni nyeti ambazo uingizwaji wake bila ushuru wa forodha ungeathiri uchumi wetu. Kwa sababu hiyo na ili kuvipa viwanda vya Tanzania fursa ya kuijandaa, bidhaa za kundi hili ziliendelea kutozwa ushuru wa forodha kwa viwango vinavyopungua kila mwaka ambapo kufikia mwaka 2010 hazitatozwa ushuru wa forodha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba ya uondoaji wa ushuru wa forodha kwa bidhaa za kundi B kutoka Kenya ziingiapo Tanzania ni kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho A. Kwa hiyo, napenda kutumia fursa hii kuwaasa wafanyabiashara wetu kuendelea kujizatiti kiushindani katika soko la Afrika Mashariki tukitambua kwamba ushindani utaongezeka zaidi ifikapo mwaka 2010. Miaka mitano iliyotolewa kwa ajili ya viwanda vyetu kuijandaa ni vyema itumike kujizatiti kukabili ushindani siyo kwa bidhaa kutoka Kenya tu bali kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Umoja wa Forodha kuanzishwa, biashara baina ya Nchi Wanachama waanzilishi imeongezeka. Mauzo ya Tanzania katika Jumuiya yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani 95.4 Milioni mwaka 2004 hadi Dola 173.1 milioni mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 81.4 ikilinganishwa na mwaka 2004. Katika kipindi hichohicho, manunuzi ya Tanzania kutoka Afrika Mashariki yameshuka kutoka Dola 137.7 Milioni mwaka 2004 hadi Dola 106.6 Milioni mwaka 2007, sawa na punguzo la asilimia 22.6. Muhtasari wa mauzo na manunuzi kwa kila Nchi Mwanachama mwanzilishi ni kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda na Burundi hazijaanza kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha hususan Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha (*Common External Tariff*) na Upunguzaji wa Ushuru kwa bidhaa kutoka Tanzania. Bidhaa zitokazo Kenya hazitozwi ushuru ziingiapo Rwanda na Burundi na vivyo hivyo ushuru kwa bidhaa za Uganda umepunguzwa kwa asilimia 80 chini ya utaratibu wa COMESA. Chini ya makubaliano ya kuziingiza Rwanda na Burundi katika Jumuiya, nchi hizo zinatakiwa kupunguza ushuru wa forodha kwa asilimia 80 kwa bidhaa kutoka Tanzania na vivyo hivyo Randa na Burundi kupunguziwa ushuru wa forodha katika bidhaa zao ziingiapo Tanzania. Maandalizi yanafanywa ili kutekeleza makubaliano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikwazo Visivyokuwa vya Ushuru (*Non Tariff Barriers*) bado ni kero kubwa kwa wafanyabiashara katika Jumuiya. Vikwazo vilivyobainishwa ni pamoja na urasimu katika usimamizi wa masuala ya forodha, taratibu ngumu za ukaguzi wa ubora na viwango vya bidhaa, vizuizi visivyo vya lazima barabarani, mlolongo wa vyombo vinavyosimamia masuala ya forodha yanayofanana na taratibu ngumu za usajili na kupata leseni. Vikwazo hivi viro katika nchi zote za Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondoa vikwazo hivi, mwaka 2007 nchi wanachama ziliunda Kamati za Kitaifa za kusimamia na kuratibu uondoaji wa vikwazo vya kibiashara. Kamati ya Kitaifa ya Tanzania inaundwa na wajumbe kutoka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Mambo ya Ndani; Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (*CTI*) na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (*TCCIA*). Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo mratibu wa Kamati ya kitaifa kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki ni muhimu sana katika kutatua Vikwazo Visivyokuwa vya Ushuru. Kwa sababu hiyo, napenda kutoa wito kwa wafanyabiashara na wasafirishaji mizigo nchini kuwasilisha kero wanazokabiliana nazo katika kufanya shughuli zao za kibiashara. Fomu maalum zimeandaliwa zinazowezesha kubaini vikwazo katika shughuli za kibiashara. Fomu hizo zinapatikana Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, *TCCIA*, *CTI*, *TRA* na katika vituo vya Forodha vya mipakani. Aidha, wananchi wanawenza kupata fomu hizo katika Tovuti ya Wizara ya Afrika Mashariki yaani www.meac.go.tz. Mfano wa Fomu hizo ni kama Kiambatisho C.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha hususan kubaini kero za wananchi katika kutumia fursa za soko la Afrika

Mashariki, Wizara katika mwaka 2007/2008 ilifanya ziara katika maeneo ya mipakani hususan Namanga, Holili, Horohoro, Mutukula na Sirari. Vile vile Wizara ilifanya ziara katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Kagera na Dar-es-Salaam kwa lengo la kutoa ushauri na elimu kuhusu uzingatiaji wa viwango vya ubora wa bidhaa ili kuongeza mauzo nje ya nchi. Mionganoni mwa Taasisi zilizotembelewa ni pamoja na Soko la Samaki Kirumba, Kiwanda cha *Nile Perch Fisheries Ltd*, *C.K. Home Products Ltd*, *Allied Chemicals*, Kiwanda cha kutengeneza bidhaa za ngozi cha *JAET Ltd*, Kiwanda cha kutengeneza vipuri mbalimbali cha *Dillu Engineering Co.Ltd*, pamoja na *SIDO*. Vile vile Wizara ilitembelea kiwanda cha Kutengeneza Vifaa vya Umeme kilichopo Arusha (*TANALEC*). Tunatarajia kuwa ushauri tuliuoutoa katika kuimarisha shughuli za Viwanda utazingatiwa ili kuongeza tija na ubora wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundwaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Soko la Pamoja ni hatua ya pili ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kifungu cha 76(1) cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kimeainisha nyanja zifuatazo za ushirikiano katika Soko la Pamoja:-

- (a) Uondoaji wa Vikwazo vya Kibiashara;
- (b) Uhuru wa Wananchi wa Jumuiya kwenda watakako, kufanya kazi na kuishi sehemu yoyote ya Jumuiya;
- (c) Uhuru wa kutoa huduma za kibiashara katika Jumuiya; na
- (d) Uhuru wa kuwekeza mitaji.

Maeneo mengine ya ushirikiano yanahusu uhuishaji wa sera za jumla na za kisekta za kiuchumi na kijamii, usimamizi wa maadili ya ushindani wa kibiashara, sheria na taratibu za Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika Jijini Arusha tarehe 5 Aprili, 2006, uliagiza kuwa majadiliano ya Soko la Pamoja yaanze mwezi Julai, 2006 na kukamilika ifikapo Desemba, 2008. Ratiba inaonyesha kuwa Bunge lako Tukufu linatarajiwa kuridhia Itifaki ya Soko la Pamoja ifikapo Juni, 2009 na utekelezaji kuanza Januari, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya uundwaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki yameshaanza. Kwanza, Sekreterieti ya Jumuiya iliagizwa na Baraza la Mawaziri kufanya utafiti kuhusu mfumo wa Soko la Pamoja utakaofaa na kubainisha taasisi zitakazohitajika kuundwa ili kusimamia utekelezaji. Utafiti huo ulikamilishwa na Ripoti kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Agosti, 2007. Baraza la Mawaziri la Jumuiya lilijadili Ripoti ya utafiti huo na kuagiza kuwa Rasimu ya Itifaki iliyoandaliwa na Washauri Elekezi iwe mionganoni mwa nyaraka zitakazotumika katika majadiliano ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Pili, Wizara yangu ilishauriana kwa kina na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama,

Wizara mbalimbali, taasisi za umma na sekta binafsi kuhusu ushiriki wetu katika majadiliano ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Vile vile Wizara yangu imefanya utafiti wa kina kuhusu mambo ya msingi Ambato Tanzania ni lazima iyazingatie katika majadiliano ya kuandaa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2008, Wizara yangu ilianda semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ili kutoa taarifa ya maandalizi ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Taasisi na wadau wote hawa walitoa michango mizuri sana itakayosaidia majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya hoja za wananchi walizozitoa wakati wa kukusanya maoni kuhusu kuharakisha au kutoharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki zinagusa moja kwa moja suala ya Soko la Pamoja. Kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka jana tumeanza kuzifanyia kazi hoja za wananchi. Tunatarajia kuwa uchambuzi wa hoja za wananchi utatuwezesha kubaini uwezo na udhaifu wetu katika ushirikiano wa Kikanda na jinsi ya kujipanga kukabiliana na changamoto zilizopo na zitakazojitokeza siku za usoni.

M h e s h i m i w a M w e n y e k i t i ,
n a p e n d a k u l i h a k i k i s h i a B u n g e l a k o T u k u f u k u w a u s h a u r i w a w a d a u
m b a l i m b a l i u t a z i n g a t i w a k a t i k a m a j a d i l i a n o y a S o k o l a P a m o j a i k i w a n i p a m o j a n a
k u l i n d a m a s l a h i y a T a i f a n a k u h a k i k i s h a I t i f a k i h i y o i n a k u w a y a m a n u f a a k w a T a n z a n i a
n a A f r i k a M a s h a r i k i k w a u j u m l a .

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa sekta binafsi, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha kuwa sekta binafsi ni mionganini mwa mihimili mikuu ya kuendeleza ushirikiano katika Afrika Mashariki. Kwa kuwa sekta binafsi bado ni changa, Nchi Wanachama zimejiwekea utaratibu wa kuandaa maonyesho ya kikanda ya sekta isiyo rasmi kila mwaka maarufu kama Maonyesho ya Jua Kali/Nguvu Kazi. Madhumuni ya maonyesho haya ni kujenga sekta isiyo rasmi ili hatimaye ikue na kufikia ngazi ya sekta rasmi. Mwaka huu maonyesho ya Nguvu Kazi/ Jua Kali yatafanyika Kigali, Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maonyesho ya Jua Kali/Nguvu Kazi, ni fursa nzuri kwa wajasiriamali wetu kukutana na kubadilishana mawazo na uzoefu juu ya kukuza na kuendeleza biashara zao, kujifunza na kuanzisha uhusiano wa kibashara. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa wadau wote kushiriki kikamilifu kama walivyofanya katika maonyesho yaliyofanyika Jijini Nairobi, Kenya, mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Vituo vya Uwekezaji katika nchi wanachama ilianda Kongamano la Uwekezaji Jijini Kigali, Rwanda kuanzia tarehe 26 hadi 28 Juni, 2008. Kongamano la Uwekezaji liliandaliwa na Kituo cha Uwekezaji cha Rwanda na kuratibiwa kwa pamoja na vituo vya uwekezaji katika Jumuiya ikiwemo Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (*TIC*). Kongamano hilo lilifanyika sambamba na Mkutano wa Viongozi Wakuu wa

Jumuiya na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya 700 toka ndani na nje ya Jumuiya. Lengo kuu la Kongamano hilo lilikuwa kutangaza vivutio vya uwekezaji katika Jumuiya na kuwakutanisha wawekezaji. Kongamano la aina hii litakuwa likifanyika kila mwaka kwa kupokezana miongoni mwa nchi wanachama. Mwenyeji wa Kongamano la Uwekezaji kwa mwaka 2009 atajulikana baada ya nchi mwanachama mmojawapo kujitokeza kuwa mwenyeji. Kwa sababu hiyo, nashauri Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) waangalie uwezekano wa kufanyika Kongamano la Uwekezaji hapa nchini kwa mwaka 2009 au 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*Tanzania Private Sector Foundation*) tumeanza maandalizi ya ziara ya wafanyabiashara wa Tanzania katika nchi za Afrika Mashariki. Ziara hiyo inatarajiwa kufanyika katika robo ya kwanza ya mwaka 2008/2009 na itahusisha washiriki takriban 60 kutoka sekta binafsi na umma ambao watatembelea na kukutana na wafanya biashara wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Madhumuni ya ziara hii ni kuwawezesha wafanyabiashara wetu kubainisha fursa za masoko na uwekezaji katika nchi hizo. Natoa wito kwa Wafanyabiashara na Wajasiriamali wajitokeze kwa wingi kushiriki katika ziara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaopenda kushiriki, wawasilishe maombi yao mapema iwezekanavyo kabla ya mwisho wa mwezi huu katika ofisi za Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi na programu za maendeleo. Mojawapo ya malengo ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuboresha maisha ya wananchi wa Afrika ya Mashariki kwa kutekeleza Miradi na Programu mbalimbali za Jumuiya zitakazowaletea maendeleo wananchi wa Afrika Mashariki. Kwa hiyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki inatekeleza miradi na programu za maendeleo katika sekta ya miundombinu, nishati, mawasiliano na uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa sekta ya Miundombinu, Nishati, Mawasiliano na Uchukuzi. Ubainishaji wa miradi ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hufanyika kwa pamoja lakini utekelezaji wake hufanywa na nchi husika. Kazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kubainisha miradi yenye sifa za kikanda, kuitangaza kwa wawekezaji na kutafuta wafadhili au mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha. Fedha zinapopatikana nchi husika ambapo mradi utatekelezwa na ambayo itakuwa na jukumu la kurejesha fedha hizo ndiyo huingia mkataba wa kuchukua mkopo unaohusika na utekelezaji wa mradi. Kwa mfano, hivi karibuni Jumuiya ilifanikiwa kupata mkopo wa mradi wa barabara ya Arusha – Namanga – Athi River kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) na Benki ya Japan (*JBIC*). Kwa utaratibu nilioueleza Tanzania itahusika na mkopo wa sehemu ya Arusha-Namanga na kwa upande wa Kenya sehemu ya Namanga – Athi River Serikali ya Kenya inawajibika kurejesha Mkopo huo.

Napenda kusisitiza na ielewewe kuwa inayokopa ni Nchi mwanachama na wala siyo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya ya Afrika Mashariki inawezesha upatikanaji wa fedha zinazosaidia utekelezaji wa miradi yenye sifa ya kikanda. Taasisi mbalimbali za

fedha duniani hupendelea kutoa fedha kwa miradi yenyeye sifa ya kikanda na ndiyo maana kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki tuliandaa programu mbalimbali zenyeye sifa ya kikanda. Programu hizo ni kama vile programu ya mtandao wa barabara za Afrika Mashariki, programu ya reli za Afrika Mashariki, programu ya kusaidia usafiri wa majini kwa maziwa na mito wa Afrika Mashariki, programu ya usafiri wa anga wa Afrika Mashariki, programu ya teknolojia ya habari na mawasiliano ya Afrika Mashariki na mpango wa nishati wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele kiichopo katika kuendeleza Reli katika Jumuiya ni kuziunganisha pale iwezekanapo na pia kuzifanyia ukarabati na kuwekwa katika mfumo wa kisasa kwa kuongeza upana wa njia ya reli. Kwa sasa wataalamu wanaendelea kufanya uchambuzi wa kina zaidi utakaowezesha uandaaji wa mapendekezo ya jinsi ya kutekeleza mkakati huu wa uendelezaji reli katika Jumuiya na pia kuainisha hatua za kuchukuliwa katika kuzifanya reli katika nchi Wanachama kuwa za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu duni ni miongoni mwa vikwazo vikubwa katika kukuza, kuendeleza uzalishaji na biashara katika Jumuiya. Kutokana na hali hii, Sekreterieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa mikutano ya Kazi (*Retreats*) ya kujadili hali ya miundombinu katika kanda hii. Mikutano hiyo ilifanyika mwezi Machi, 2008 jijini Mwanza kwa Makatibu Wakuu na kufuatiwa na mkutano wa Mawaziri uliofanyika mwezi Aprili, 2008 huko Kampala, Uganda. Taarifa ya Mkutano wa Mawaziri iliwasilishwa katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika Kigali, Rwanda mwezi Juni, 2008. Lengo kubwa la mikutano hiyo lilikuwa ni kujadili changamoto zilizopo katika kuendeleza miundombinu na ufumbuzi wake. Aidha, mwishoni mwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama, Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliagizwa kuendeleza jitihada za kubainisha miradi na kutafuta raslimali za utekelezaji kwa lengo la kuimarisha miundombinu katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji mafuta. Katika kuitangaza Afrika Mashariki kama eneo lenye utajiri mkubwa wa mafuta na gesi, Jumuiya ya Afrika Mashariki huandaa mkutano mkubwa wa uwekezaji katika sekta ya mafuta (*East Africa Petroleum Conference*) kila baada ya miaka miwili. Lengo la mkutano huo ni kutangaza fursa za uwekezaji katika sekta hii. Mkutano wa kwanza ulifanyika Nairobi, Kenya mwaka 2003 na kufuati Kampala, Uganda mwaka 2005. Mkutano wa tatu ulifanyika Arusha mwezi Machi 2007. Maandalizi ya mkutano wa nne ambao umepangwa kufanyika nchini Kenya mwezi Machi, 2009 yameanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mikutano hii imekuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji wa sekta ya mafuta na gesi ndani na nje ya Afrika Mashariki. Kwa mfano, mkutano uliofanyika Arusha uliwaleta pamoja washiriki zaidi ya 350 kutoka Nchi Wanachama, mashirika ya fedha ya kimataifa, watalaam kutoka taasisi mbalimbali, makampuni ya utafutaji mafuta na yale yanayotoa huduma katika shughuli za utafutaji mafuta. Watalaam hao walijadili mada mbalimbali kuhusu masuala ya utafutaji mafuta sanjari na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Nchi Wanachama zinadurusu Mpango Kamambe wa Kuendeleza Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda (*Regional ICT Infrastructure Master Plan*) ili izingatie mahitaji ya maeneo ya mijini na vijiji, uwekaji wa Sera za Kitaifa za Mawasiliano na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika nyanja hii. Maeneo ambayo yamebainishwa kuwa ni muhimu kuzingatiwa ni pamoja na Matumizi ya Mtandao wa Utoaji Huduma Serikalini (*e-Government*), Afya (*e-Health*) na Uhamiaji (*e-Immigration*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, mradi wa *e-Health* ulizinduliwa kwa majaribio katika Kanda ya Ziwa mwaka 2007/2008. Uzoefu utakaopatikana kutokana na utekelezaji wa mradi huu utatumika kusambaza huduma hii sehemu nyingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maji. Ziwa Victoria ni mojawapo ya raslimali ambayo Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi zinashirikiana katika matumizi yake. Kutokana na kuwepo uhusiano huu katika matumizi ya ziwa, Nchi Wanachama zilikubaliana kutekeleza miradi ya pamoja ili kukidhi haja ya matumizi endelevu ya raslimali hii muhimu. Baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekeliza katika Bonde la Ziwa Victoria na ambayo Tanzania inafaidika nayo ni pamoja na Awamu ya pili ya mradi wa Utunzaji wa Mazingira Katika Ziwa Victoria [*Lake Victoria Environment Management Project II (LVEMP II) (2008-2014)*]. Mradi huu utahusu maeneo makuu manne ambayo ni:-

- (a) Kuimarisha mfumo wa usimamizi na matumizi ya Ziwa na kuweka taratibu za ukaguzi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira;
- (b) Kuimarisha usimamizi wa maliasili hai katika Ziwa Victoria kuitia sera, sheria na mwongozo wa utunzaji mazingira;
- (c) Kuinua uchumi wa wakazi wa maeneo ya Ziwa kwa kutambua maliasili za uwekezaji zilizopo na zinazoweza kutumika bila ya kuharibu mazingira kwa kuuwezesha umma kuwekeza na kutunza mazingira, kuendeleza sekta binafsi na miradi ya wakazi; na
- (d) Kuongeza uelewa wa umma kuitia programu za mafunzo na mawasiliano ya moja kwa moja kwa kuanzisha vituo vya habari na kwa kuwaelimisha waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kuratibu utekelezaji wa miradi hii limewekwa chini ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria. Hivi sasa Kamisheni imeagizwa kufanya utafiti wa matumizi ya mito katika usafiri na usafirishaji kwa kuanzia na Mto Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zote hizo nilizozieleza zitasaidia kuinua hali ya maisha ya wakazi wapatao milioni 30 waishio kandokando ya Bonde la Ziwa Victoria. Kwa hiyo, nawaomba viongozi na wananchi wa eneo hilo waendelee kutoa ushirikiano wa kutosha kama walivyofanya katika Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi na programu za sekta ya huduma za jamii. Ushirikiano katika nyanja ya kijamii umejikita katika elimu, utamaduni, michezo, sayansi na teknolojia. Katika kuimarisha ushirikiano katika maeneo haya, Nchi Wanachama zimeandaa Itifaki za kusimamia masuala ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu, mchakato wa kupata Makao Makuu ya Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia unaendelea. Tanzania ni mionganini mwa nchi zilizoomba kuwa wenyeji wa Kamisheni hiyo. Aidha, mchakato wa kuridhia Itifaki ya Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia umekwishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya masuala yaliyotekeliza katika nyanja za kijamii kwa mwaka 2007/2008 ni pamoja na kuanza zoezi la kuhuisha mitaala ya elimu katika Jumuiya, kuendesha mashindano ya uandishi wa insha na kubainisha taasisi zitakazotambulika kama vituo vilivyobobe (*Centres of Excellence*).

Nchi wanachama ziko katika mchakato wa kubainisha taasisi zenye sifa ya kuweza kuwa vituo vilivyobobe na baada ya hapo kuwasilisha mapendekezo ya vituo hivyo kwenye Jumuiya ili taratibu za ukaguzi zifanyike kwa kulingana na vigezo vilivyowekwa. Kwa hiyo, natoa wito kwa Wizara zinazohusika kuwasilisha mapendekezo ya taasisi zao katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hatua hii itawezesha Wizara kushughulikia mapendekezo husika kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya. Kutambulika kikanda kwa vituo hivyo kutatoa fursa ya kutambulika kikanda na kimataifa na pia kufaidika na programu na miradi ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Tanzania imewasilisha mapendekezo ya miradi inayoweza kutekelezwa Zanzibar kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi iliyowasilishwa inahusu barabara, bandari, nishati na kilimo. Miradi husika ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar, Uwekaji wa Vituo vya Umeme wa Upopo Zanzibar, Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi, na Miradi Mitano ya Kilimo inayohusu utafiti wa kilimo cha Baharini, Magonjwa ya Wanyama, Teknolojia za Kuongeza Ubora wa Mazao, Uimarishaji wa Karantini za Mazao na Mifugo na Uimarishaji wa Miundombinu ya Uvuvi katika Bahari ya Kina Kirefu. Hii ni nje ya Uwanja wa Karume ambao tayari fedha zake zimepatikana kwa ajili ya kuboresha uwanja ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mradi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Uwezeshaji wa Biashara na Usafirishaji (*Trade and Transport Facilitation*), Sekretariati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imeagizwa kuandaa mfumo wa kisera wa kikanda kwa kushirikiana na nchi za SADC na COMESA kwa ajili ya kuwianisha masuala ya viwango vya uzito wa magari, utaratibu wa kupima magari kwenye mizani na matumizi ya TEKNOHAMA (*ICT*) katika masuala ya viwango vya uzito na mizani ya upimaji magari. Aidha, Sekretariati itashirikiana na Timu ya Wataalam kutoka Nchi Wanachama katika kufuatilia utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uzalishaji, kwa upande wa kilimo na usalama wa chakula, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeanza maandalizi ya Mfumo wa

Tahadhari ya Usalama wa Chakula na Mabadiliko ya Hali ya Hewa (*East African Early Warning System*). Aidha, Jumuiya imeandaa mapendekezo ya mfumo utakaotumika katika ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mkakati wa Kilimo na Maendeleo Vijijini kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya ya Afrika Mashariki imeunda pia Kamati ya kusimamia mradi wa Kuzuia na Kupambana na magonjwa ya mlipuko yanayosambazwa na binadamu na wanyama kati ya nchi wanachama (*Project Steering Committee on the Control and Prevention of Human and Animal Trans Boundary Project – TADs*). Aidha, nchi wanachama zimekamilisha taratibu za kusimamia afya za walaji kwa upande wa wanyama na mimea (*Sanitary and Phytosanitary*). Hatua hii itapunguza sana usumbufu uliopo katika biashara ya bidhaa za mimea na mifugo. Taratibu husika zitapatikana katika Tovuti ya Wizara katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii, uendelezaji wa utalii unategemea kwa kiwango kikubwa huduma za Hoteli. Kwa kutambua hilo Jumuiya imebuni vigezo vitakavyotumika kupanga madaraja ya hoteli, migahawa na huduma mbalimbali za kitalii katika Jumuiya. Zoezi la kupanga madaraja ya hoteli kwa kutumia vigezo vilivyowekwa lilifanyika nchini Uganda ili kufanikisha mkutano wa Jumuiya ya Madola. Zoezi hili ni muhimu katika biashara ya ushindani ikiwemo utalii. Kwa hiyo, hoteli zitakazovutia watalii ni zile zilizofikia vigezo vilivyowekwa na kukaguliwa ili kuthibitisha ubora wa huduma na vifaa vilivyomo. Zoezi hili litafanyika katika nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ningependa kushauri wafanyabiashara wa sekta hii kuanza maandalizi na kuzingatia vigezo vilivyowekwa ili kukidhi viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara za kuitangaza Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mkakati mmojawapo unaotumiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kutekeleza majukumu yake ni pamoja na kufanya ziara katika nchi marafiki na taasisi mbalimbali duniani. Katika mwaka 2007/2008 Mawaziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki walifanya ziara ya kikazi nchini China mwezi Mei 2008. Pamoja na kujenga uhusiano mwema na Jamhuri ya Watu wa China, ziara hiyo ililenga katika kuangalia uwezekano wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa pamoja hususan katika kuboresha miundombinu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hiyo ilikuwa ya mafanikio. Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imeonyesha nia ya kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuboresha Miundombinu. Napenda kushauri Wizara na taasisi zinazohusika na uendelezaji wa miundombinu na uwekezaji kuibua miradi na kufanya upembuzi yakinifu ili iweze kuwasilishwa kwenye Jumuiya na hatimaye Jamhuri ya Watu wa China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, demokrasia na haki za binadamu. Katika kuimarishe demokrasia mionganoni mwa nchi wanachama, Wenyeviti wa Tume za Uchaguzi katika Afrika Mashariki walikutana mwezi Mei, 2008 mjini Arusha ili kupitia na kuhuisha sera za uchaguzi mionganoni mwa nchi wanachama kwa lengo la kuwa na mfumo wa uchaguzi unaolingana. Wakuu wa Tume ya Haki za Binadamu kutoka nchi wanachama wa Jumuiya walifanya kikao cha kwanza mjini Arusha mwezi Februari, 2008. Madhumuni ya kikao hicho ilikuwa ni kuangalia uwezekano wa kuwa na sera na mfumo unaolingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika Mashariki katika mwaka 2007/08 Bunge lilijadili na kupitisha jumla ya miswada saba kuwa sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miswada hiyo ni:-

- (a) Muswada kuhusu Mapato na Matumizi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Appropriation Bill, 2007*);
- (b) Muswada wa kuhusu Nyongeza ya Mapato na Matumizi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Supplementary Appropriation Bill, 2007*);
- (c) Muswada wa Usafirishaji katika Ziwa Victoria (*The Lake Victoria Transport Bill, 2007*);
- (d) Muswada kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Customs Management Act (Amendment) Bill, 2007*);
- (e) Muswada kuhusu kukasimisha Madaraka na Majukumu ya Wakuu wa Nchi Wanachama (*The Summit (Delegation of Powers and Functions) Bill, 2007*);
- (f) Muswada wa Majadiliano ya Biashara wa Afrika Mashariki (*The East African Trade Negotiations Bill, 2007*);

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ili kuimarisha mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Bunge la Afrika Mashariki limekamilisha idadi ya Wabunge kufuatia Jamhuri za Rwanda na Burundi kukamilisha taratibu za uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Wabunge hao waliapishwa katika kikao cha sita cha Bunge la Afrika Mashariki kilichofanyika mwezi Mei, 2008 Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed ambaye naye baada ya mabadiliko tuliyoyafanya katika Mkataba Unaanzisha Jumuiya ya Afrika, sasa ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Jumuiya, jukumu kuu la Mahakama ya Afrika Mashariki ni kuhakikisha kuwa Mkataba wa Jumuiya unazingatiwa na kutoa tafsiri sahihi ya Mkataba huo pale inapohitajika. Mahakama hii imegawanyika katika vitengo viwili; Kitengo cha Awali (*Court of First Instance*) na Kitengo cha Rufaa (*Appellate Court*). Mahakama hii kwa sasa inaundwa na Majaji kumi. Majaji watano watakuwa katika Kitengo cha Awali cha Mahakama ya Afrika Mashariki na watano wengine watakuwa katika kitengo cha Rufaa cha Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

Walioteuliwa na kuapishwa kuwa Majaji wa Kitengo cha Rufaa cha Mahakama ya Afrika Mashariki ni:-

- (1) Mheshimiwa, Jaji Joseph N. Mulenga (Uganda);
- (2) Mheshimiwa, Jaji Harold R. Nsekela (Tanzania);
- (3) Mheshimiwa, Jaji Philip K. Tunoi (Kenya);
- (4) Mheshimiwa, Jaji Laurent Nzosaba (Burundi); na
- (5) Mheshimiwa, Jaji Emilie R. Kayitesi Rusera (Rwanda).

Wakuu wa Nchi wanachama vilevile waliteua na kuwaapisha Majaji wafuatao kuwa Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki wa Kitengo cha Awali:-

- (6) Mheshimiwa, Jaji John Mkwawa (Tanzania);
- (7) Mheshimiwa, Jaji Jean Bosco Butasi (Burundi); na
- (8) Mheshimiwa, Jaji Johnson Busingye (Rwanda).

Aidha, Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamewateua Jaji Kassanga Mulwa (Kenya) na Mheshimiwa Jaji Mary Stella Arach – Amoko (Uganda) ambao walikuwa Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki kuwa Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki Kitengo cha Awali (*First Instance Division*)

Vilevile Wakuu wa Nchi waliwateua sawia Mheshimiwa, Jaji Joseph N. Mulenga (Uganda) na Mheshimiwa, Jaji Harold R. Nsekela (Tanzania) kuwa Rais na Makamu Rais wa Mahakama Afrika Mashariki. Pia, Wakuu wa Nchi waliwateua Mheshimiwa, Kassanga Mulwa (Kenya) kuwa *Principal Judge* na na Mheshimiwa, Jaji Johnston Busingye (Rwanda) kuwa Deputy Principal Judge wa Mahakama ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa makao makuu ya Jumuiya. Katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2006/07 nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa suala la ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki limepatiwa ufumbuzi baada ya Serikali ya Tanzania kutoa eneo lenye ekari kumi na moja (11) kwa ajili ya ujenzi huo mkoani Arusha. Aidha, awali Serikali ya Ujerumanilitoa kiasi cha fedha za kigeni *Euro* milioni nane (8) kwa ajili ya ujenzi huo. Sasa napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya kufanya tathmini upya kwa kuzingatia kuongezeka idadi ya Nchi Wanachama za Rwanda na Burundi, Serikali ya Ujerumanilimekubali kuongeza fedha kiasi cha *Euro*

milioni sita (6) na hivyo ujenzi utaanza mwezi Septemba, 2008 na unategemewa kuchukua miezi 30 hadi mwezi Septemba 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma, mchakato wa kutafuta maoni ya wananchi kuhusu kuharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki ulibainisha kuwa wananchi wengi hawajui shughuli za Jumuiya. Kwa hiyo, Wizara imezingatia suala la utoaji wa elimu kwa umma kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki kama mionganini mwa majukumu ya msingi ya Wizara. Tunaamini kuwa elimu ya kutosha kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki itawawezesha wananchi kushiriki katika maamuzi yanayofanywa katika hatua za ushirikiano na kutumia kikamilifu fursa zitokanazo na ushirikiano. Wizara yangu imeanzisha kitengo cha Habari, Mawasiliano na Elimu kwa madhumuni ya kuboresha mawasiliano na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/08 Wizara iliendelea kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya Afrika Mashariki kupitia semina, warsha, magazeti, vipindi vya redio na Televisheni. Vile vile, Wizara ilitekeleza jukumu hilo kwa kushiriki katika Maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa jijini Arusha, kutoa elimu katika vyuo vikuu ikiwemo Chuo Kikuu cha Tumaini na Chuo Kikuu cha Ardhi vilevile Wizara ilitoa elimu kuhusu masuala ya Afrika Mashariki kwa Watendaji na Wafanyabiashara katika Mikoa ya Morogoro na Kagera. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza utaratibu wa Serikali wa kutoa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya wizara kwenye vyombo vya habari na pia kuimarisha tovuti yake ambayo ni www.meac.go.tz Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wanakaribishwa kutembelea tovuti hii ili kupata taarifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya maendeleo ya watumishi, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu katika kujenga uwezo wa watumishi na kuboresha utendaji, jumla ya watumishi kumi na nane (18) walipelekwa kwenye mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Wizara ilitoa mafunzo kuhusu taratibu, Kanuni na maadili ya utendaji katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2007/2008, Wizara ilifanya mapitio ya muundo wa utumishi ili kuboresha utendaji kazi. Mapendekezo ya mabadiliko ya muundo yamewasilishwa Serikalini kwa hatua zaidi. Aidha, katika kuunga mkono juhudhi za Serikali za kupambana na janga la UKIMWI, Wizara imeendesha mafunzo kwa watumishi jinsi ya kujikinga na maambukizi na pia kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji. Utekelezaji wa shughuli za Wizara ulikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Vikwazo vya kibiashara: Pamoja na kwamba uondoaji wa ushuru wa forodha mionganini mwa nchi wanachama uendelea vizuri, bado kuna changamoto kubwa kwa upande wa Vikwazo Visivyo vya Kodi yaani *Non-Tariff Barriers*. Nchi zote Wanachama zimekuwa na malalamiko ya wafanyabiashara wao kuhusu suala hili;

(b) Miundombinu Duni: Miundombinu duni, mathalani barabara zilizo chini ya viwango, umeme usio wa uhakika na wa gharama kubwa huathiri uzalishaji na tija katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(c) Kupanda kwa gharama za mafuta katika soko la dunia: Hii imesababisha kupanda kwa gharama za uendeshaji katika sekta zote za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2008/2009, baada ya kuelezea utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka uliopita, sasa napenda kuelezea kwa muhtasari majukumu yatakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2008/09. Wizara kwa kushirikiana na sekta na wadau mbalimbali itatekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

(i) Kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake na maamuzi mbalimbali ya vyombo vya Jumuiya ukiwemo Mkutano wa Wakuu wa nchi, Baraza la Mawaziri, Bunge na Mahakama ya Jumuiya ya afrika Mashariki;

(ii) Kuratibu ziara ya mafunzo kwa wajasiriamali, wafanyabiashara na wazalishaji wa Tanzania kutembelea nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa lengo la kujifunza, kubadilishana uzoefu na kubaini fursa na changamoto za kibiashara zilizopo;

(iii) Kuendelea kuratibu na kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya soko la pamoja la Afrika Mashariki;

(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa ujumla katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(v) Kuratibu na kushiriki vikao vya majadiliano na kuendelea kujenga uwezo wa Wataalam wanaohusika na majadiliano mbali mbali;

(vi) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha;

(vii) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kwa lengo la kubaini mafanikio na kasoro za utekelezaji na kutoa mapendekezo ya hatua zinazostahili kuchukuliwa;

(viii) Kutumia Balozi zetu nchini Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi katika kuendeleza biashara na uwekezaji;

(ix) Kutembelea Taasisi na miradi inayosimamiwa na Jumuiya;

- (x) Kushirikiana na Wizara, Sekta Binafsi na wadau wengine katika kuandaa na kuhuisha Sera, mikakati na programu za nchi ili ziendane na za Jumuiya;
- (xi) Kukamilisha majadiliano ya rasimu ya Itifaki ya Mambo ya Nje. Itifaki hii itachukua nafasi ya mkataba wa makubaliano maalum ya ushirikiano katika sera za nje (*MoU on Foreign Policy Coordination*); na
- (xii) Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani, mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yametokana na Ushirikiano wa Serikali yetu, Taassis binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, wafanyabiashara pamoja na wahisani mbalimbali. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wote waliohusika kwa njia moja ama nyininge katika ushiriki wao kwenye vikao na mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wafanyakazi wenzangu katika Wizara waliowezesha kusomwa kwa Hotuba hii katika Bunge lako Tukufu leo hii. Kwa heshima, napenda nimshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Mohamed Aboud, kwa msaada wa karibu anaonipa katika kusimamia shughuli za Wizara. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu, Bwana Bakari A. Mahiza, Wakuu wa Idara na Vitengo, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kukamilisha maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa wakati. Aidha, nawapongeza kwa utendaji kazi wao wenye tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo mwisho kwa umuhimu, naomba nimshukuru mke wangu Adelaide Kamala na familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa, pia ninawashukuru viongozi walionitangulia kuongoza wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kazi nzuri waliofanya. Waliontangulia kuongoza Wizara hii ni Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi; na Mheshimiwa Dkt. Ibrahim Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini. Wote kwa pamoja nawashukuru kwa kunifundisha kazi na kuniongoza nilipokuwa msaidizi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawashukuru Makatibu Wakuu wastaafu Ndugu Omar Bendera na Ndugu Wilfred Nyachia kwa kazi nzuri waliofanya kujenga Wizara mpya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha za Wizara kwa mwaka 2008/2009, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya jumla ya shilingi 10,941,750,000 (Bilioni Kumi Milioni Mia Tisa Arobaini na Moja Mia Saba Hamsini Elfu). Kati ya fedha hizo shilingi 10,359,750,000 (Bilioni Kumi Milioni Mia Tatu Hamsini na Tisa Mia Saba Hamsini Elfu) ni za Matumizi ya Kawaida na shilingi Shilingi 582,000,000 (Milioni Mia Tano Themanini na Mbili) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa bajeti kwa mwaka 2008/2009 ni kama ifuatavyo:-

Maelezo	Kiasi (Tsh.)
MATUMIZI YA KAWAIDA	10,359,750,000
(a)Mishara (PE)	353,128,000
(b)Matumizi mengineyo (OC)	10,006,662,000

MCHANGANUO WA MATUMIZI MENGINEYO

(i) Mchango kwa Jumuiya	5,920,000,000
(ii) Matumizi ya Kawaida	4,086,622,000
Jumla ndogo	10,006,622,000

BAJETI YA MAENDELEO

(c) Matumizi ya maendeleo	582,000,000
---------------------------	-------------

JUMLA KUU (a+b+c)	10,941,750,000
--------------------------	-----------------------

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dokta Kamala kwa hotuba yako nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, nitaomba mnisamehe kidogo, kwa kweli nitakuwa sijatenda haki wakati nikiatambulisha wageni, nafikiri kwa sababu leo nimesahau miwani yangu nyumbani, kuna wageni niliwaruka, sasa si vema kweli kutokfanya haki katika suala kama hilo, sasa naomba tu mkubali muwatambue watoto wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambao wapo hapa toka asubuhi lakini sikuweza kuwatambulisha na wameongozwa na Mama mkwe wake na shemeji yake, naomba wasimame. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, vilevile ninaomba kwa kweli niwatambue rasmi pia watoto wa Mheshimiwa Martha Mlata, Jonalith, Vanessa na Junior na wao kwa kweli wapo hapa ndani toka asubuhi, ningeomba nao wasimame. Nafikiri wamekimbia wakanywe chai kidogo baada ya kuona nimewasahau.

Kwa hiyo, naomba niombe radhi sana lakini niwaombe radhi pia Waheshimiwa, kwa kweli miwani yangu leo baada ya kuisahau, nikasahau na mambo mengine ya muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, ninaomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua bajeti hii, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama, aje awasilisha maoni ya Kamati hiyo na ninamwona Mheshimiwa Vita Kawawa anakuja kuwasilisha maoni hayo kwa niaba ya Mwenyekiti.

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuja kuwasilisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Vita, umesimama maana naulizwa hapa kama umesimama?

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama.

MWENYEKITI: Sawasawa, basi endelea.

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze nami kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema hadi kufikia muda huu nawasilisha hotuba hii kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Kamati ya Wabunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa kunichagua mimi kuja kuwawakilisha hapa mbele leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba univumilie, niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kwa imani na ushirikiano wanaonipa. Naomba niwahakikishie kwamba sitawaangusha na waendelee kunipa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimshukuru na kumwombea afya njema, Mzee wetu, Mzee Rashid Mfaume Kawawa, ili aendelee kutuongoza na kutupa busara yake katika familia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mke wangu, Siwa Kawawa, kwa kuiongoza vema familia yangu na kuendelea kunipa nguvu, naomba aendelee kunipa nguvu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba nimpongeze Waziri wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, kwa

kuiwasilisha vema hotuba yake ya bajeti ya Wizara yake na Naibu Wake Mohamed Aboud kwa ushirikiano wanaoipa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni Na. 99(7) Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha ya 2008/2009 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili maoni hayo na hatimaye kukubali kuidhinisha makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2007/2008, Kamati yetu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2007/2008. Katika taarifa hiyo Kamati ilielezwa kuhusu yafuatayo:-

1. Ushirikishwaji wa Wadau wa Masuala ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
2. Utekelezaji wa Umoja wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ulianza rasmi tarehe
01 Januari, 2005;
3. Hali halisi ya michango ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi mwezi Machi, 2008;
4. Soko la pamoja ambalo ni hatua ya Pili ya mtangamano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;
5. Miswada sita iliyopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki kwa Kipindi cha 2007/2008 pamoja na itifaki 8 kwa kipindi hicho;
6. Miradi mitatu inayotekerezwa nchini, kupitia ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki ambayo ni mtandao wa barabara, mradi wa Reli na mradi wa Ziwa Victoria; na
7. Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni kwa Kipindi cha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imejitahidi sana katika utekelezaji wa majukumu yake sambamba na kutekeleza ahadi za Serikali Bungeni. Hata hivyo, Kamati hii ilielezwa changamoto zilizojitokeza kwa mwaka wa fedha uliopita. Changamoto hizo ziligusa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni malalamiko yaliyopokelewa na Wizara kuhusu viwango vyta ushuru kwenye bidhaa za mitumba, baiskeli na vipuri vyake, karatasi, vifungashio, mafuta ya kutengeneza sabuni na magari ya abiria na mizigo.

Kamati iliambiwa kuwa Wizara iliwasilisha mapendekezo ya kurekebisha upungufu uliojitokeza kufanikiwa kushawishi nchi wanachama kupunguza ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa suala la ushuru katika magari ya abiria na mizigo halijapatiwa ufumbuzi. Aidha, vikwazo vyta kibishara ni changamoto nyingine katika utekelezaji wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vikwazo hivi ni vile Visivyo vyta Kodi yaani (*Non tariff barriers*). Suala hili ni changamoto kwa nchi zote wanachama na wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kuhusu kikwazo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha tuliarifiwa kuwa udhaifu wa miundombinu umeathiri sana uzalishaji na tija katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kukabliana na changamoto hii Baraza la Mawaziri lilipitisha miradi mbalimbali ukiwemo mradi wa mtandao wa Barabara za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2008/2009, baada ya kutoa taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka uliopita, Mheshimiwa Diodorus B. Kamala (Mb), Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki alieleza Kamati hii kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 pamoja na kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na yale ya Maendeleo kwa Fungu 97. Katika Makadirio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 10,941,750,000/- (Bilion Kumi, Milioni Mia Tisa na Arobaini na Moja, Laki Saba na Elfu Hamsini).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hizo Shilingi 10,359,750,000/- (Bilion Kumi, milioni Mia Tatu na Hamsini na Tisa, Laki Saba na Elfu Hamsini), ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 582,000,000/- (Milioni Mia Tano na Themanini na mbili) kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kutafakari kwa kina taarifa ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha uliopita na kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 kama zilivyoainishwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri iliyowasilishwa hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kwamba, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kueleza Maoni ya Kamati yangu kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni umiliki ardhi, kwa kuwa katika biashara kama msingi wa ushirikiano baina ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuna hatua mbalimbali ikiwemo utafiti wa Mazao ya Kilimo mionganoni mwa nchi wanachama na kwa vile ardhi ni rasilimali inayopatikana kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki, Kamati inashauri kuwa uwekwe utaratibu madhubuti wa Kisheria utakaosaidia kuwalinda Watanzania na ardhi yao dhidi ya wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni Hali ya Michango ya Nchi Wanachama hadi 2008, suala la michango ya nchi Wanachama ni muhimu sana katika uendeshaji wa shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuwa kuna maelekezo ya Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba nchi Wanachama zikamilishe kulipa michango yake hadi kufikia mwezi Disemba kila mwaka, kwanza tunaipongeza Wizara ya Fedha kwa kushirikiana vizuri na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na hatimaye kuiwezesha Tanzania kukamilisha malipo ya mchango wake kwa wakati.

Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa nchi zote ambazo hazijakamilisha kulipa michango yake zihimizwe kukamilisha michango kwa wakati. Aidha, kwa nchi yeoyote ambayo itabainika kuwa haijalipa michango yake, Wakuu wa Nchi wanachama washauriwe kufikiria kutoiruhusu nchi hiyo kushiriki Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni Bandari ya Dar es Salaam; uzoefu unaonyesha kuwa Bandari ya Dar es Salaam haina uwezo wa kutumia fursa zilizopo katika ushirikiano wa Afrika Mashariki jambo ambalo linakwaza uwezo wetu kufaidika na Bandari ya Dar es Salaam kimapato. Aidha taratibu za ushuru katika Kituo chetu cha Holili zimeifanya Bandari yetu ya Dar es Salaam kuwa ghali. Ili kujiweka katika nafasi nzuri kuhusu ushirikiano wa Afrika Mashariki kibiashara, Kamati inashauri kuwa Serikali ifikirie utaratibu wa Ki-ushuru utakaofanya Kituo cha Holili kichangie katika kuongeza mapato na ufanisi wa Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni upitishaji wa Miswada katika Bunge la Afrika Mashariki. Kama nilivyosema hapo awali, Kamati ilielezwa kuhusu Miswada iliyopitishwa Mwaka 2007/2008 wakati wa Awamu ya Pili ya Bunge la Afrika. Hata hivyo, ilielezwa kuwa Sheria hizo hazijaanza kutumika kwa sababu Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado hawajaziidhinisha. Kamati inashauri kuwa utaratibu wa Kisheria kwa mujibu wa Mkataba na Itifaki zake uangaliwe upya kwa lengo la kuuboresha ili uidhinishaji wa Sheria uwe rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni Mradi wa Mtandao wa Miundombinu, kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa kuyaunganisha maeneo ya mwambao Tanzania Bara na Zanzibar kwenye mtandao wa miundombinu, Kamati inashauri kuwa mradi wa mtandao wa Barabara za Afrika Mashariki ufikiriwe ili kuunganisha maeneo hayo kwenye mtandao huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni Bandari ya Tanga, Ili kuwa sambamba na mradi wa kuboresha miundombinu ya Afrika Mashariki, Bandari ya Tanga ipanuliwe na kuimarishwa kwa madhumuni ya kujenga mazingira mazuri ya kiuchumi sanjari na upanuzi huo. Vilevile Kamati inashauri kuwa Reli ya Tanga iboreshwe pamoja na kuendeleza barabara ya Tanga, Arusha hadi Musoma na Tanga, Pangani, Bagamoyo hadi Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba ni Mchakato wa Kuajiri, pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuendelea na mchakato wa kuajiri, bado kuna umuhimu mkubwa wa kuharikisha mchakato huo kwa kuzingatia Matakwa ya Makubaliano ya Makao Makuu (*The Headquarter Agreement*) kuhusu ajira kwa nchi mwenyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dk. Diodorus B. Kamara,(Mb), Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Mohamed Aboud,(Mb) Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Katibu Mkuu Bwana Bakari Mahiza, pamoja na Wataalam wa Wizara hiyo kwa maelezo ya kina mbele ya Kamati na kwa kweli tunaridhishwa na kazi nzuri ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wasaidizi wake wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao na kwa kufanya uchambuzi wa kina ulioiwezesha hoja hii kufikia hatua iliyopo sasa. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson. M. Masilingi, Mb – Mwenyekiti na Mheshimiwa Musa A. Zungu, Mb - Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brg.Jen Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini sio kwa umuhimu, napenda niwashukuru Dkt. Thomas D. Kashilillah, Kaimu Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa. Bila kuwasahau Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Athuman Hussein na Ndugu Neema Kiula kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama alivyowasilisha mtoha hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Vita Kawawa.

Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na yeye aweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Afrika Mashariki.

MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY- MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa Bungeni tukiwa wazima na wenye afya.

Pili, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7) toleo la 2007, kutoa maoni, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusiana na Wizara ya Afrika Mashariki, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi zetu za Afrika Mashiriki. Nchi hizi kwa hivi sasa ni pamoja na Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nichukue nafasi hii, kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa uongozi wao madhubuti wenyе kuifanya Kambi ifanye kazi yake kulingana na Kanuni zetu za Bunge na kwa maana hiyo kuwapa Watanzania matumaini mema ya kuona kuwa kuna watu wanaowatetea kulingana na matakwa yao. Bila kusahau, nitoe pia pongezi kwa Wabunge wote wa Upinzani kwa ushirikiano walionao, ambao kwa pamoja ndio wanaofanya Kambi hii kuwa imara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na misiba, maafa na majanga mbalimbali ambayo yote ni mionganini mwa mitihani yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tuwaombee wenzetu wote waliokwishatangulia makaazi mema peponi na wale waliopatwa na maumivu wawzeze kupona haraka. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ilikubaliwa na Jumuiya kwa kupitia wakuu wa nchi hizo wanachama kwamba ifikapo Desemba 2007 kila nchi mwanachama iwe imeshalipia mchango wake wa \$4,296,532.00

mchango ambao kwa pamoja ungesaidia sana matumizi ya Jumuiya hiyo pamoja na kuwalipia gharama za mishahara kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko makubwa kwamba hadi hivi sasa ni Tanzania na Uganda tu ndio waliolipa ada zao kwa asilimia mia moja. Napenda nichukue nafasi hii kuzipongeza sana nchi hizi mbili kwa kitendo chao hicho cha uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tulizo nazo, Kenya inadaiwa karibu asilimia 7.5% wakati Rwanda inadaiwa asilimia 75%. Burundi bado haijalipa hata senti moja na hivyo kudaiwa asilimia mia moja (100%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona hii ni dosari kubwa sana kwa nchi hizo ambazo hazijalipa na bado kuendelea kutumia fursa za jumuiya hiyo kwa sababu mkataba unasema chini ya Ibara ya 132(4) kuwa bajeti itagharimiwa (*funded*) na michango sawa kutoka nchi wanachama wa jumuiya, kulikoni leo baadhi ya nchi zichangie na nyingine zisichangie na hatua zozote zisichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya nyingi za aina hii, ambazo huhitaji michango ya nchi mwanachama kujidesha, basi huwa na vifungu maalumu ndani ya Katiba zao zinazotoa adhabu kwa nchi zisizolipa ada zao. Umoja wa Mataifa Umoja wa nchi huru za Kiafrika, Umoja wa nchi za Ulaya na kadhalika ni mifano tosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika makubaliano (mkataba) ya Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, Ibara ya 143, inasema kwamba nchi mwanachama ambae atashindwa kutekeleza wajibu wake wa kifedha na majukumu mengine atakabiliwa na vikwazoama adhabu (*sanction*) kama vile ambavyo *Summit* itaamua.

Vile vile Ibara ya 146(1) inasema *Summit* inaweza kumsimamisha mwanachama kushiriki katika shughuli za jumuiya mwanachama atakayeshindwa kwenda sambamba na kutekeleza misingi na malengo ya mkataba huu ikijumuisha kushindwa kutekeleza wajibu wake kifedha (*failure to meet financial commitments*) kwa jumuiya kwa kipindi cha miezi 18.

Ibara ya 146(2) inaongeza kuwa mwanachama aliyesimamishwa hataruhusiwa kuendelea kufaidika na matunda ya jumuia (*cease to enjoy the benefits provided*). Kiuhalisia hapa inajumuisha wanachama ambao hawajalipa ada zao wasiruhusiwe kufaidika na huduma zinazotolewa na Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko makubwa kuwa nchi kama Burundi ambayo haijatoa hata shilingi moja bado wanaruhusiwa kupata huduma za Jumuiya hiyo ikiwemo kuhuduria Bunge la Jumuiya na vikao vyengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba wanachama hawa ambao hawajakamilisha malipo yao yaani Burundi, Rwanda na Kenya wachukuliwe hatua kwa kiwango ambacho hawajalipa kama Ibara ya 143 na 146 ya makubaliano (mkataba) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisimama madhubuti juu ya utaratibu wetu tuliojiwekea, tunaamini kuwa wanachama wa jumuiya hii watauona umuhimu wa michango hiyo na hivyo kuharakisha kulipia michango hiyo kwa wakati muafaka ili shabaha na malengo ya jumuiya yaweze kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa zamani wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, suala hili sasa limekuwa sugu na bado ufumbuzi wake haujapatikana. Tunaamini pia kuwa Wizara hii haihusiki sana katika suala hili, lakini kwa sababu tu wanaodai ni Watanzania wenzetu, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba hapa ni pahala pake pa kulisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Serikali iwatupie jicho la huruma Watanzania hawa waliokuwa wakifanya kazi katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliyovunjika mwaka 1977, hasa ukitilia maanani kuwa wenzao wa Kenya na Uganda wameshalipwa mafao yao yote karibu miaka 30 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tulizonazo ni kuwa Watanzania hawa hadi hii leo wamelipwa kiasi cha shilingi billion 117, ukilinganisha na shilingi billion 450 ambazo ilikuwa walipwe. Je, hizi shilingi billion 333 ambazo hawajalipwa watalipwa lini? Ni jambo la aibu kila siku vyombo vyahabari vinatoa na kuonesha taarifa za malalamiko za wastaa fu hao hadi sasa wengine wamepiga kambi katika maeneo fulani wakisubiri Serikali iwalipe. Hoja ya Waziri wa Fedha iliyowataka wastaa fu hao kwenda mmoja mmoja kwa sababu ya kutokuwepo takwimu na eti kila mmoja ana tatizo lake sio ya msingi sana kwa vile tatizo linafahamika na wahusika wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Wizara hii, kukisukuma chombo kinachohusika ili wafanyakazi hawa nao wapate mafao yao ili wapumzike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirikisho lenye matatizo, ni ukweli usiopingika kuwa hali ya dunia hivi sasa ipo katika muelekeo wa nchi zilizo majirani au kupakana kuunda

Jumuiya za kiuchumi kwa nchi hizo. Hoja zinazotolewa ni kuwa kuongeza wanachama katika Jumuiya ni kuimarisha umoja. Lakini ni vyema kujua kuwa nchi zetu zina mitazamo tofauti ya kiuchumi, kimila, kisiasa, kiusalama na kwamba hii inaweza kutuongezea matatizo mbalimbali katika nchi zetu kuliko kufikia lile lengo letu tulilolikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza ni kuwa, wakati bado nchi zetu hizi zinakumbwa na matatizo mengi ya ndani na mengine yakiwemo yale matatizo yaliyosababisha kuvunjika kwa Jumuiya hii, Wakuu wa nchi zetu wameamua kuingiza wanachama zaidi katika Jumuiya hiyo. Sisi tunaona ni vyema kwanza tukatatua matatizo tuliyonayo sisi wenyewe kabla ya kujibebesha matatizo ya wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zetu wanachama (Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda), zina matatizo mengi sana. Kenya kwa mfano, bado inapambana na matatizo ya ndani ya kikabila, mfumo wa kisiasa wenyewe athari za ukabila, kama tulivyoshuhudia hivi karibuni japo kwa kiwango kikubwa wamefanikiwa kuondoa tofauti zao katika ngazi za Bunge. Uganda nayo halikadhalika si nchi shvari. Inaandamwa na matatizo ya *Lord Resistance Army (LRA)*; ambapo habari zinazozagaa ni kuwa kundi hili limeanza tena kijiandaa kuanzisha mapigano mapya. Pia mfumo wa kisiasa umetawaliwa na nguvu za kijeshi chini ya Amiri Jeshi Mkuu. Uganda bado kuna athari kubwa za mgawanyiko wa kikabila. Tanzania vilevile ina matatizo mengi. Suala la matatizo ya Muungano sasa limekuwa “nyimbo ya kawaida” malalamiko ya Ki-Katiba nayo yamekuwa ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kisiasa kuchafuka mara kwa mara huko Zanzibar na mpasuko wa kisiasa unaozidi kila uchao ndio inazidi kuidhoofisha Zanzibar na hili ni mionganoni mwa matatizo makubwa ndani ya Tanzania ambayo ni lazima kupatiwa ufumbuzi kabla ya kujingiza ndani ya matatizo mengine ya nchi za Rwanda na Burundi. Hata huko Rwanda na Burundi hali si shvari. Lakini zaidi ni Burundi ambayo ina matatizo makubwa nchini mwake ambayo inaweza kuathiri nchi zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kabisa hali ya demokrasia katika nchi zetu za Afrika Mashariki bado ni mbovu. Ni bora na itakuwa ni uamuzi wa busara kwanza nchi hizi zingeboresha walau siasa zao kabla kuingia katika Shirikisho hasa (*political federation*) ili tusije tukaangukia katika mfumo mbovu zaidi wa kisiasa na kuzidisha matatizo. Mfano Jumuiya ya Ulaya ilishirikiana kwa mambo tofauti tofauti kwa muda mrefu na walipitia hatua baada ya hatua kabla ya kwenda na kufikia katika Shirikisho walilonalo leo hii. Lakini inashangaza kwa pupa ya kwenda kwenye shirikisho la kisiasa tuliyonayo sisi Wana-Afrika Mashariki. Kambi ya Upinzani ingelipenda kufahamu baada ya kukusanya maoni ya Wananchi ni kitu gani kinaendelea na Watanzania wanashirikishwa kwa kiasi gani katika mchakato huo unaoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Pamoja, utengamano wa pili katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni soko la pamoja. Soko hili ni kuhusu wigo wa ushirikiano kwa kujumuisha nyenzo za uzalishaji pamoja na biashara ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 76(1) cha Mkataba wa Jumuiya kinajumuisha nyanja zifuatazo za soko la pamoja.

- (i) Uondoaji wa vikwazo vya biashara;
- (ii) Uhuru wa wananchi wa Jumuiya kwenda watakako kwa kufanya kazi na kuishi sehemu yoyote ya Jumuiya;
- (iii) Uhuru wa kutoa huduma kibiashara katika Jumuiya; na
- (iv) Uhuru wa kuhamisha mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni zito sana na kwa sisi Tanzania ni lazima mambo yafuatayo tuyazingatie kwa makini ili baadaye tusije tukajilaumu. Mambo yenye ni kama ifuatavyo:-

(i) Tofauti za kiuchumi za nchi wanachama ambapo uchumi wa Kenya uko juu pamoja na maendeleo ya viwanda ukilinganisha na nchi zetu za Burundi, Rwanda, Tanzania na Uganda, Tanzania hajifikia uwezo wa kushindana na Kenya katika sekta hii na hivyo basi, ni hofu yetu kuwa Tanzania inaweza kugeuzwa soko la bidhaa za Kenya. Je, Tanzania imejiandaaje kuingia katika ushindani huu wa kibepari? Je, muda wa matayarisho (*grace period*) wa miaka mitano itatosheleza kwa Tanzania na Uganda kufikia hatua ya Kenya ukitilia maanani kuwa muda huo unakaribia kumalizika na bado hatujafanya chochote? Kambi ya Upinzani ingependa kupata tathmini ya kina ya hali halisi ili tunapofanya maamuzi yaye maamuzi yaliyokwishafanyiwa kazi na yenye maslahi kwa nchi na kwa wananchi wetu.

(ii) Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda wana uhaba wa ardhi nzuri yenye rutuba wakati Tanzania bado kuna maeneo makubwa ya ardhi yenye kufaa kwa shughuli za kilimo na ufugaji wa kisasa. Hofu ya Watanzania ni uwezekano wa ardhi hii kuvamiwa na wageni kutoka nchi jirani na kuleta migongano ya ardhi, jambo ambalo ni tatizo kubwa na wakati mwengine huwa ndio sababu ya mapigano baina ya watu au makabila. Hapa ni lazima kuwe na sheria itakayolinda haki za ardhi kwa Watanzania. Je, Sheria zetu zimeandaliwa kwa kiasi gani kukabiliana na hali hiyo?

(iii) Uwezekano wa wageni kujinufaisha na rasilimali zetu asilia kutokana na uwezo wao mkubwa zaidi wa kimtaji na uwezo wa kifedha kuwekeza katika uvunaji wa rasilimali hizo kuliko sisi Watanzania. Bado nchi zetu hizi hazina ukweli na uaminifu.

Kenya kwa mfano mara kadhaa hutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kama vile ni vya kwao.

(iv) Hofu kwa vijana wa Kitanzania kukosa ajira rasmi kutokana na ushindani wa soko la ajira, hili pia linachangiwa na mfumo wetu wa elimu na udhaifu wa lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa Kitanzania. Madhara yake ni kuongezeka umasikini na vijana wetu daima watakuwa na kazi duni nchini mwao. Je, hili ndio lengo letu la kujiunga na Jumuiya ili kuwakosesha nafasi vijana wetu?

(v) Kukosekana kwa kitambulisho rasmi kinachomtambulisha raia wa Tanzania (*National Identity*) nalo ni tatizo kubwa sana. Wakati baadhi ya nchi wanachama kama vile Kenya na Uganda tayari wanawatambua raia wao wote kwa vitambulisho vya uraia, bado Tanzania hatujahakikisha mikakati hii.

(vi) Watanzania wana hofu kuwa raia wa nchi jirani ambazo pia zina migogoro kama vile Rwanda na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (*DRC*) kuzagaa nchini. Hii itazidisha maovu ambayo tunapigana nayo.

(vii) Kila nchi hadi sasa inatumia sarafu yake, sarafu ambazo zinatofautiana sana kithamani. Kwa mfano thamani ya sarafu ya Kenya ni zaidi ya mara kumi na tano kithamani ukilinganisha na ile ya Tanzania. Vivyo hivyo sarafu ya Uganda hailingani na ile ya Kenya au Tanzania au ya Burundi au ya Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu hizi na nyingi nyinginezo ambazo hatukuzieleza, bado zinatufanya sisi Kambi ya Upinzani na Watanzania walio wengi kuona kuwa bado Shirikisho hili lina matatizo mengi ambayo ni vyema yakatatuliwa kidogo kidogo na kwenda taratibu katika suala la kukamilisha shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayotekelizwa nchini, *Tripitite Agreement on Road Transport* ya mwaka 1998 umeweka nguvu kwa Serikali ya Tanzania kubuni miradi ya barabara (Dar-Mutukula 1000 km, Biharamulo-Mwanza 500 km, Arusha – Namanga 900km na Nyamkazi-Sumbawanga, Tunduma 900 km). Miradi wa reli pia ulibuniwa chini ya mpango huu kwa kukarabati reli zilizopo, kubadili reli zilizopo kwa kuongeza upana mkubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mwingine wa Ziwa Victoria unaohusu usalama wa uchukuzi, mradi wa kuendeleza makazi ya wananchi waishio pembezoni mwa ziwa na mradi wa utunzaji wa mazingira wa Ziwa Victoria. Hapa ningelifikiria kuwa, kwa Tanzania iliyomaniki, pia ingewajali Watanzania wenzao walioko Pwani kwa kuibua mradi salama wa usafiri baharini kwa mwambao wa Mombasa, Tanga, Pemba, Unguja, Dar es Salaam na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana na kutia huzuni kwamba miradi yote hii kwa jina la Jumuiya kwa Tanzania ni kwa Tanzania Bara tu bila ya kujadili kuwepo kwa Zanzibar kama ni sehemu mojawapo kati ya nchi mbili zilizoungana pamoa na kufanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa faida inayopatikana kutoka Jumuiya hii kwa Zanzibar haipo na hivyo basi kuonesha dhahiri jinsi Zanzibar inavyoumia kutokana na kutoshiriki kikamilifu katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana katika kipindi kilichopita Kambi ya Upinzani ilitaka kujua hadi hii leo, ni vipi Zanzibar inafaidika na Shirikisho hili kwa yale mambo ambayo sio ya Muungano na kila upande wa Muungano kuyashughulikia peke yake kama vile barabara, kilimo, elimu, uvuvi, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia kuwa eti miradi kadhaa kutoka Zanzibar imekubaliwa kuwasilishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa hatua zaidi. Miradi hiyo ikiwemo:-

- (a) Tathmini ya watumishi na nguvu kazi;
- (b) Ujenzi wa bandari mpya ya maruhubi;
- (c) Upanuzi wa uwanja wa ndege wa Zanzibar;
- (d) Mradi wa kuzalisha umeme wa upepo; na
- (e) *Program* za eneo huru la mlipuko wa magonjwa ya mifugo, kunyanya teknolojia ya usafiri wa mazao ya kilimo, karantini ya mimea, maendeleo ya kilimo cha mwani na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa program hizi zote kwa Zanzibar ndio kwanza zinakwenda kuwasilishwa kwa kuzingatiwa, sijui *program* hizi zitaanza baada ya miaka mingapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi niliyoitaja hapo juu, ambayo imependekezwa na *SMZ* kabisa haikutilia maanani suala la kuibua mradi Kisiwani Pemba ambao utasaidia kuondoa umasikini pamoja na kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mkubwa wa kufanya eneo la Ras Mkumbuu Kisiwani Pemba kuwa ni bandari kuu na mlango wa meli zinazokwenda au zinazotoka sehemu nyingi za ulimwengu. Mradi huu ni wa zamani na ulikwishafanyiwa uchunguzi na kuonekana kuwa eneo hilo linafaa kwa shughuli hizo pamoja na kuwekwa chelezo cha kutengeneza meli, bandari ya kuchukulia mafuta, maji na kadhalika. Suala hili pia lilizungumzwa sana katika Jumuiya hii ya Afrika ya Mashariki. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni sababu zipi zilizoufanya mradi huu kusahauliwa, na je, haoni kama ni busara kwa Serikali kuuweka mradi huu kwa sababu ni mkubwa? Unakidhi mahitaji ya kuwekwa katika mradi, utasaidia kuondoa hali duni za watu wa Kisiwa cha Pemba, utaongeza pato la Taifa na

utafungua lango kwa kuleta meli nyingi kubwa za kigeni kwa ajili ya matengenezo, kuweka mafuta, kuweka maji pamoja na kufanya eneo la kupakia na kupakua makontena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba ya Kirafiki ya Kiuchumi (*Economic Partnership Agreement*) sote tunajua kwamba umoja wa nchi za Ulaya (*European Community*) na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (Burundi, Kenya, Rwanda, Tanzania na Uganda) walitiliana saini mkataba ambao ulihakikisha (*guarantee*) uondoaji wa ushuru (*duty free*) pamoja na mgawanyo wa bure (*quota free access*) wa kwenda Umoja wa Ulaya kwa mizigo inayosafirishwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki isipokuwa kwa sukari na mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapenda kujua Tanzania katika mpango huu imefaidika kiasi gani ukilinganisha na Kenya, Burundi, Rwanda na Uganda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mkataba huo ndio hatua ya kupelekea katika mchakato kamili wa kufikia *EPA* (*Economic Partnership Agreement*) kwa lengo la kuunganisha soko la pamoja la ukanda huu pamoja na ule wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*Reginal Intergration*) na *Intergration* ya Afrika ya Mashariki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili na tukitathmini hali halisi ilivyo hivi sasa, kwa Jumuiya hii, hali ya wasiwasi imeshaanza kufunika miyo ya Watanzania walio wengi. Umoja wa Forodha uliotiwa saini tarehe 01Januari, 2005 ndio uliopewa kipaumbele kama ndio mkakati mkubwa wa kuelekea shirikisho hili. Ibara ya 75(7) ya mkataba wa Jumuiya inasisitiza:-

Kuwepo na uhuru zaidi wa biashara za nchi hizi bila ya nchi kuingiliana na mwenzake;

Kuendeleza zaidi uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi hizi za Jumuiya;

Kuendeleza uwekezaji wa ndani na wa nje pamoja na biashara ya mipakani; na

Kuendeleza zaidi uchumi wa nchi zetu pamoja na kuwa na viwanda mbalimbali kwa lengo la kustawisha nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo haya bado yanatofautiana baina ya nchi zetu. Bado nia za nchi hizi haziko sawa. Kwa mtazamo wa Kambi yetu, mambo yafuatayo yana mashaka:-

Kenya ambayo iko mbele kimaendeleo kwa viwanda na kiuchumi, haina nia njema ya kuziinua Burundi, Rwanda, Tanzania na Uganda kwa kuwa na uwiano sawa. Kwa Mfano tu, hili lipo wazi katika muda waliopewa Tanzania na Uganda wa miaka mitano kuwa ni muda wa kujiweka sawa (*grace period*), muda huu ni mdogo sana, usiotosha kuziinua nchi hizi kiuchumi. Hawa wenzetu, Burundi na Rwanda walioingia katika Jumuiya hivi juzi, nao watapewa muda gani?

Kenya bado inavutia kwake tu, hasa katika suala la mizigo inayotoka Tanzania katika magari ya Tanzania ambapo; magari hayo hulazimishwa kupakuwa mizigo mpakani na kubewa na magari ya Kenya, kwa kisingizo tu kuwa devera huyo wa Tanzania hana *International Driving Permit (IDP)*.

Mbao zinazotoka Tanzania (Ludewa) kwa mfano zinasafirishwa hadi Kenya na zinapofika Kenya mbao hizo hupigwa mihuri ya Kenya ili zionekane kuwa mbao hizo ni mazao ya Kenya.

Kuna taarifa za kukua kwa Unyanyasaji wa wafanyabiashara za mipakani (*cross boarder traders*) siku hadi siku. Je, haya na mengineyo mengi yatatatuliwa VIP ili shirikisho hili lioneckane kuwa kweli ni la nchi wanachama? Je, Serikali inazo taarifa hizo na imezichukulia hatua gani hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo, Tanzania au Watanzania bado ni wavivu wa kufanya kazi. Upungufu huu wa lengo (*lack of seriousness*) utatugharimu sana. Mizigo iliyoko bandarini Dar es Salaam, kwa mfano inachukua wiki tatu ili iweze kutolewa; wakati mizigo kama hiyo ikiwepo Bandari ya Mombasa, basi ni siku moja au mbili tu ili iweze kutoka. Hatima ya hili ni kuwafanya wafanyabiashara wetu watolee mizigo yao hiyo Mombasa na hivyo kuinufaisha zaidi Kenya.

Hata wakati wa matatizo ya Kenya hivi karibuni, Watanzania hatukuonekana kuichukua nafasi ya utendaji katika Bandari ya Dar es Salaam licha ya Bandari ya Mombasa kuwa na matatizo makubwa. Haya yote yanatuthibitishia kuwa ni lazima matatizo tulionayo katika nchi zetu tuyatature kwanza ili tunapoingia katika Shirikisho hilo, basi iwe matatizo hayo madogo madogo hayapo. Zaidi, hii inathibitisha vile vile kuwa mwenendo hasa unaotakiwa kufuatwa ili kuingia katika Shirikisho hilo ni kidogo kidogo ili kutoa nafasi kwa nchi husika kumaliza matatizo yaliyopo nchini mwao. Kambi ya Upinzani, inaunga mkono dhana ya Dhirikisho la Afrika Mashariki kama moja na nguzo imara katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho imara litazaa matunda kwa kutupatia utulivu wa hali ya kisiasa, ulinzi na usalama wa pamoja, kujenga uchumi wenye nguvu, pamoja na kuwa na kauli moja yenye nguvu (*strong bargaining power*). Lakini ili kufikia huko tunapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

- (a) Nchi yetu ianze kuweka mikakati ya kujandaa kiuchumi na kiushindani katika soko huria kwa muda wa kipindi kisichopungua miaka 10 toka sasa huko tukifanya tathmini ya mikakati hiyo;
- (b) Tuboreshe mfumo wetu wa elimu na kuwaanda vijana wetu kiushindani wa soko la ajira la pamoja mapema na haraka iwezekanavyo;

- (c) Kwanza tujenge demokrasia ndani ya nchi zetu na kutatua migogoro ya kisiasa na kijamii iliyomo ndani ya nchi zetu kabla ya kuharakisha kuunda Shirikisho litakalokuwa na mizozo mengi; na
- (d) Serikali itoe vitambulisho vya uraia kwa Watanzania wote wenye haki hiyo kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza hatua muhimu za kufatwa ili tuweze kujenga Shirikisho lililo imara katika mtiririko ufuatao:-

- (i) Kuanzishwa kwa eneo la biashara huru (*Free Trade Area*);
- (ii) Kuwepo kwa Umoja wa Forodha (*Customs Union*);
- (iii) Kuwa na soko la pamoja (*Common Market*);
- (iv) Kuanzisha utangamano wa kiuchumi (*Economic Intergration*) ambapo sera za kiuchumi na masuala ya fedha za nchi wananchama huwa sera katika nchi wanachama; na mwisho
- (v) Kuundwa kwa Shirikisho la kisiasa (*Political Federation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo Shirikisho la kisiasa ni hatua ya mwisho ambapo nchi wanachama zitakuwa zimejidhatiti kiuchumi na kisiasa kutokana na kuwepo kwa uhuru wa kuingia na kutoka kwa watu na bidhaa zao baina ya nchi wanachama, kuondolewa kwa vikwazo vya ushuru katika biashara baina ya nchi wanachama, kuwa na soko kubwa la pamoja na kuwa na sera za kiuchumi zenye kuafikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Tunapoamua hatma ya Tanzania na watu wake, ni vyema tukawashirikisha wananchi wenyewe na maamuzi yao yaheshimiwe. Jumuiya au Mashirikisho ya aina hii sasa yanaundwa kila uchao, na sisi Watanzania tusijitenge kwa hilo. Jambo la msingi ni kutazama kwa undani zaidi vipi wananchi wetu watanufaika au kuathirika kutokana na Jumuiya au Mashirikisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayoendelea duniani yamesababisha viongozi wa wananchi kuwa katika hali ya utata. Ni lazima tuwe na mpango kamili wa kuwaelimisha wananchi wetu juu ya mambo muhimu ya zamani ilipoanzishwa Jumuiya hii, vilevile kuwaelimisha na mambo yaliyopo na yale yanayotabiriwa kuja hapo baadaye.

Ni kweli kuwa viongozi wetu wana nia na dhamira ya kweli kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki. Lakini zaidi tunapaswa kuzitambua changamoto zilizopo mbele na kujua ni ushirikiano wa aina gani utakaoleta ufanisi zaidi na kwa maana nyingine kuondoa matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tujue hasa ni kwa nini Afrika Mashariki yetu imebakia maskini na kuandamwa na migogoro? Ni mambo gani hasa yanayoathiri siasa, uchumi na Utamaduni wa eneo hili? Vipi tunazitumia fursa tulizonazo na vipi tutakabiliana na vikwazo vinavyoweza kujitokeza hapo baadaye? Ni lazima tujue tunaelekea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo, basi tutazame matatizo yaliyomo katika nchi yetu na tuanze kuyatatua ili kutuepusha kuingia ndani ya Shirikisho huku tukiwa na matatizo ndani ya nchi yetu. Pia, lazima tuhakikishe kuwa yale matatizo yaliyosababisha kuvunjika jumuiya hii hapo awali, yote yamepatiwa ufumbuzi kabla ya kuendelea na Shirikisho kamili. Tuwe na msimamo wetu wa kuwa na Shirikisho ambalo litatuletea faida kwa wananchi wetu kwa maslahi ya vizazi vyetu na nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na ninaomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary kwa umahiri wako mkubwa katika kuwasilisha hotuba hii na kutekeleza kwa kuiwikilisha Kambi ya Upinzani. Nashukuru na kukupongeza sana.

Waheshimiwa Wabunge, katika orodha ambayo iko Mezani kwangu, ninao wachangiaji watatu. Mchangiaji mmoja hajawahi kuchangia hata siku moja ndani ya Bunge hili, kwa hiyo, nitampa nafasi ya mwanzo naye ni Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda. Lakini atafuatiwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa.

Kwa hiyo, hao ndiyo wachangiaji ambao wameshaomba kuchangia mada hii. Bila kupoteza muda, kwa sababu muda tunao wa kutosha kabisa, basi naomba nimwite Mheshimiwa Thomas Mwang'onda na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ajiandae, atakuwa mchangiaji wa pili.

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuweza kutoa maoni yangu kwa hoja iliyo mbele ya Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Awali ya yote, nilitaka kwanza *ni-clarify* tu kwamba nimeshawahi kuchangia Bungeni labda kwa kikao hiki cha bajeti nilikuwa kweli sijapata muda wa kuchangia.

MWENYEKITI: Ni kweli Mheshimiwa Thomas Mwang'onda kwa ajenda ambayo inaendelea ya uchagiaji wa bajeti, bado una nafasi yako kabisa kama mtu wa kwanza. Lakini najua kwa ajenda nyingine nyingi zilizopita nyingi ulishafanya hivyo.

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa

Jumuiya ya Afrika Mashariki na ya Kati, ndugu yangu aliyenifundisha kazi na kuniachia madaraka kwenye Umoja wa Vijana wa CCM akiwa kama Katibu wa Uhamasishaji wa Umoja wa Vijana wa CCM, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala na mwenzake ambaye mimi ninamwita *uncle* Mheshimiwa sana, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed kwa kazi nzuri waliyofanya wakishirikiana na watumishi wengine wa Wizara hii ambayo kwa kweli ni mpya kabisa katika nchi yetu, nadhani umri wake ni unaanza pale tu tangu tumeanza Awamu hii ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Lakini kabla ya kuendelea, nina kila sababu tena ya kutumia nafasi hii ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mawili makubwa ya muhimu. La kwanza, nilikuwa sijapata nafasi ya kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *Africa Union* kwa maana ya Umoja wa Afrika, kazi ambayo amekuwa akiifanya kwa umahiri bila woga, kwa kujiamini, na amekuwa akiendelea nayo vizuri sana. (*Makofi*)

Lakini vilevile naomba nimpe nyongeza ya pongozi zile kwa kazi kubwa waliyoifanya Kenya wakishirikiana na Rais Mstaafu Ndugu Benjamin William Mkapa kuhakikisha kwamba mgogoro wa Kenya unakwisha. (*Makofi*)

Ndugu zangu, jambo lile halikuwa dogo, lilikuwa na moto mkubwa sana, uliowaka na kuitikisa sio Kenya tu, bali hata dunia. Nadhani Kenya kwa mara ya kwanza waliweza kutawala *CNN* japo sio kwa jambo zuri. Kazi hiyo waliifanya vizuri na wakaimaliza na kutujengea heshima kubwa sisi Watanzania kwa kuona kwamba tuna Rais ambaye kwa muda mfupi tu ametumia busara zake na kutokana na kulelewa katika mazingira ya amani ya nchi anayotoka ya Tanzania akahakikisha kwamba jambo lile linakwisha vizuri na kwa ufasaha na mpaka leo Wakenya wale wana amani kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri, kama ninavyoona wachangiaji tupo watatu, Wizara hii tunaweza kusema ni ngumu kidogo, kwa maana ya kwamba haina mambo ambayo tuna-*deal* nayo kila siku. Kwa hiyo, nitajitahidi sijui nitachukua muda gani, lakini nikichukua dakika tano au kumi ninaomba tu mniwie radhi. Wizara yenye ilivyo ni machachari kweli kweli! Kwa maana ya kwamba ni Wizara inayo-*deal* zaidi na mambo ambayo yanavuka zaidi kwenye mipaka ya nchi yetu. Lakini hata hivyo, ninapata msukumo mkubwa wa kuchangia kwenye Wizara nikiamini kabisa pamoja na Wizara hii kugusa mambo ambayo yanagusa zaidi masuala ya mipaka ya nchi yetu, lakini yanatuhusisha moja kwa moja kama Watanzania na tuna kila sababu ya kuona tunafaidika na yale yanayofanyika na Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kuelezea wasiwasi wangu hasa kuhusu uelewa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali yetu na zile Serikali nyingine zote ambazo ni wanachama, tupo watano, kuna Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda na Burundi zote hizi zinaongozwa na Ilani za Uchaguzi na Ilani za Uchaguzi hizo ili ziwe na

maana zina wapiga kura nyuma yake. Sasa Ilani ya Uchaguzi inayoongoza Taifa la Tanzania ni ile ya CCM, ndiyo tunayoitambua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini CCM haiko CCM kama sisi wenye labda Wabunge ama wa -NEC na kadhalika. Tunaamini kabisa hata zile kura za CCM zilizotupa ushindi, yule mgombea wetu wa CCM wa Urais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliwahi kukiri kwamba hata Wapinzani nao walimpigia kura. Kwa maana hiyo, suala la Wizara ya hii linagusa *a wide spectrum* ya wananchi wetu. Lakini nashukuru nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwamba katika hotuba yake amekiri kwamba lipo tatizo la uelewa katika kuhakikisha kwamba Wizara hii taratibu zake na Jumuiya kiujumla inafahamika kwa wananchi wa kawaida.

Hivyo, ninajiuliza, pamoja na kuwa Mbunge wa kuteuliwa ambaye ninagusa maeneo mengine sana ya Kitaifa, japo bado ninaendelea kuomba mialiko, mnisaidie kushirikiana. Lakini ninamfikiri mkulima wa Kyela kule Mbeya, namfikiria mkulima wa pale Uyole Mbeya Mjini, kuna maeneo pale watu wanalima viazi na kadhalika. Nafikiria wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wote hao ndiyo wanafanya Ilani hii iweze kufanya kazi ndani ya Serikali yetu, wanaitambua Jumuiya ya Afrika Mashariki? Wanatambua faida zake? Wanafikiwa vipi ili kuweza kufaidika? Au Wizara hii ni kama urembo?

Lakini nashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri ameonyesha kulitambua hilo na ana nia ya kulifanya kazi. Nilitaka kuelezea uhusiano wa Iringa na Mbeya. Iringa na Mbeya ingawa tuna Wanyakyusa na makabila mbalimbali pale, Wanyiha, Wasafwa, lakini wenzetu wa Iringa nadhani kuna Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Iringa hapa Wakinga, wale wamekuwa ni *one of the major investors* kwa pale Mbeya Mjini. Ukienda kuna hoteli nyingi sana pale Mbeya Mjini ambazo Wakinga wamefanya uwekezaji mzuri sana na kutunyanya kihotelii, karibuni Mbeya jamani mtaona hali ilivyokuwa njema pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nafikiria katika misingi hii, labda yapo makabila mengine au watu wengine kutoka Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda na Tanzania yenye labda uwekezaji huu kwa kiwango fulani ungeweza kuwa mkubwa zaidi, ungeweza kuwa na nafasi kubwa tukapata uwezekaji ambao hatuupati. Kwa hiyo, *it is an issue of informing the society*, kuielezea jamii kwa ufasaha zaidi. Hili limekuwa ni tatizo kama tunaweza tukapata wawekezaji wakatoka kule Iringa Wakinga wale wakafanya kazi nzuri, nina hakika Wajaluo wengine wa kutoka Kenya wanaweza wakafanya hivyo hivyo. Nina uhakika na Wakikuyu nao wanaweza wakaja wafanya hivyo hivyo kwa sehemu mbalimbali za Tanzania.

Kwa hiyo, nasema *issue* ya uelewa ni muhimu sana na bado Wizara inaonekana kama ipo lakini labda ni ya wasomi zaidi na nimeona katika hotuba hii wamegusia sana eneo la Ziwa Victoria pale. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa mnayofanya kuhakikisha kwamba wale wenzetu Wahaya, Wasukuma kwa maana wale wanaozunguka lile Ziwa Victoria na wale wanaotoka Musoma wanafaidika na kuwepo kwa ushirikiano baina ya nchi zetu hizo tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba *we can still extend that*, tunaweza tukaongeza ushirikiano ule ukaenda mbali zaidi ukagusa hata maeneo mengine ya pembezoni. Hata ndugu zangu Wamakonde nao wakapata faida ya ushirikiano huo wa Afrika Mashariki na ya Kati. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri amelisema hili na ameliombea fedha pia katika namna ya kuelimisha jamii yetu na mimi nimwambie tu katika hili kipengele hicho nitamuunga mkono kabisa kuhakikisha kwamba Watanzania tunafaidika zaidi na kuwepo kwa Ushirikiano huo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na pendekezo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kamala na mwenzake Naibu Waziri kwamba hebu wajaribu wakaliangalie hili, ni utaratibu tuliojiwekea Afrika Mashariki kuhakikisha kwamba tunasoma bajeti zetu kwa siku moja na tuliona lilitaka kuleta matatizo kidogo *in terms items of statistical information* hapo kwa siku za nyuma, lakini sijui kama hili lipo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika
muda wa mzungumzaji)*

Loh! kengele ya kwanza! Nimechukua muda mrefu kuliko nilivyokuwa nategemea, lakini ngoja nijitahidi nimalizie kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na pendekezo la bajeti ya zamu kwa nchi Wanachama wa Afrika Mashariki kwamba mbali na zile bajeti zetu za ndani, tunaweza kuwa na bajeti ambazo labda kila mwaka *zina-deal* na nchi mbili ili tukapata fedha za ziada kwa ajili ya wananchi ili nao waone kabisa ni namna gani Wizara hii inavyofanya kazi na wanafaidika na kuwepo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nataka kuongelea suala la Reli ya Kati. *Research* niliyoifanya nimekuta nchi kama Uganda ama Kenya zinashirikiana, kuna Reli kule zinaandaliwa, zinajengwa, kuna wale wengine Wakenya wanakwenda mpaka Sudan, lakini wenzetu wa Rwanda wana hamu sana ya kushirikiana na sisi kwa masuala ya miundombinu na tunesema hapa kuna programu ya pamoja ambayo ameitaja Mheshimiwa Waziri ambayo tunaiita *Joint Infrastructure Programme*. Nilikuwa nadhani suala hili tunaweza tukalitumia tukafaidika. Rwanda, wale wanafanya kazi vizuri sana kwa upande wa biashara, tunaweza tukafaidika na kuwepo kwa ubora kwa njia ya reli kati ya sisi na Wanyarwanda kama zinavyofanya nchi nyingine.

Lingine kwa haraka haraka nilitaka niseme suala la migogoro ya kisia. Napenda niunganishe kwa pamoja na ule wa Kenya na ule wa Zimbabwe. Mgogoro wa Zimbabwe nautaja kwa sababu unaonekana unachukua sura ya Kiafrika kwa ujumla. Lakini ninataka niseme sisi kama *EAC* tunaweza kabisa maana hata Waislam na Wakristo nao husema kwamba anaposali mtu mmoja peke yake Mungu anashuka lakini hashuki sana kama wanapokuwa wamekusanyika watu wawili. Kwa hiyo, nilikuwa nataka niseme, *EAC* tuangalie wanapokwenda wenzetu, tusiwe na hofu, tuwaelekeze wanapokosea.

Mimi nimesikitishwa sana na kauli ya Mheshimiwa Rais Robert Mugabe kabla ya Uchaguzi alipotamka na sikuona sauti yoyote kutoka *East Africa*, labda hapo juzi kidogo akikemea kitendo cha kusema, na hii ni *undermining of the democracy* kabisa, kwamba hata akishindwa kwenye uchaguzi ule yeye bado atabaki kuwa Rais. Tukiliruhusu hili, linaweza likaja likasogea likafika Tanzania, likafika Kenya na nchi nyingine. Nilidhani tulipigie kelele na kwa mfano ule ule tuliangalie pia lililotokea Kenya. Nashukuru tu Mheshimiwa Rais wetu alifanya kazi kubwa kama nilivyosema hapo mwanzo kuhakikisha kwamba hayo mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *message* ninayotaka kuitoa hapa ni kwamba tuwe wakali zaidi hasa pale tunapohisi kuna *undermining of the democracy*, demokrasia inapotaka kutetereshwa. Maana hata wenzetu wa Afrika Kusini walikuwa wabishi kidogo, lakini baada ya kuona kwamba kidogo kuna kuteleza kwa mwanamapinduzi mwenzetu ilibidi walirekebishe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho tuliwahi kukijadili kwenye Kamati yetu – lakini nadhani nikukumbushie, tena ni michango ya nchi wanachama, bado nchi nyingine wanachama wanachelewa kuchangia. Naomba tujipongeze Watanzania, sisi hatuchelevi. Tunachangia vizuri sana kwenye Afrika Mashariki. Lakini bado wenzetu wanachelewa. Sasa chelewa chelewa utakuta na mwana sio wako. Nilikuwa naomba sana hili suala la vikwazo kwa wale wanachama wanaonekana ni wazito hebu tuwabane zaidi. Tutilie mkazo zaidi tuwabane zaidi ili waweze kuchangia na kutokurudisha nyuma zaidi. Kwa sababu muda bado dakika mbili au tatu naweza nikamalizia *point* ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa haraka haraka, nadhani ndiyo namalizia, kwani kengele ya kwanza imeshalia. Lilikuwa ni suala la uwekezaji kutoka kwenye *Region* hiyo ya *East Africa. Opportunities* za ndani. Wenzetu wa *European Union* wana upendeleo maalum kwa nchi wanachama. Mtanzania utakapotoka hapa uende uka-*invest* kwenye nchi ya Ulaya ni tofauti na Mgiriki au Mwitaliano akienda pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umekwishapita. Nilikuwa na hamu sana ya kuendelea. Basi, naomba nilazimike kuunga mkono hoja na kumtakia kila la kheri Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Thomas Mwang'onda kwa mchango wako. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na yeye aweze kuchangia.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nami niungane na mse maji wa kwanza kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri na timu yao ya Wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa katika matayarisho ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwanza niende kwenye ukurasa wa 30 wa hotuba ya Waziri unaozungumzia demokrasia na haki za binadamu. Msingi mkubwa wa chombo chochote kile ni ile misingi ambayo mmekubaliana kuiweka na kuisimamia. Nianze na hili suala la michango. Hili jambo tunaliona kama ni dogo, lakini ndiyo msingi wa kwanza mnapokubaliana yale masharti kwamba ni lazima mtayaifuata. Sasa kama Jumuiya haikujivekea misingi kwa wale ambao hawatekelezi masharti hayo, basi lazima tutapata matatizo makubwa mbele ya safari. Kwa hiyo, naomba kabisa hili suala la kufuata yale masharti ambayo tumekubaliana kwa mujibu wa *chatter* zile, basi ni vizuri yakasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni suala zima la demokrasia. Msingi mkubwa wa ushirikiano ni namna gani katika nchi au katika wanachama mnaposhirikiana, mambo ya lazima ya masharti ya lazima ya kufuatwa. Moja katika mashirikiano haya ni kwamba nchi zetu zitatawaliwa na utaratibu wa kidemokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama sisi wenye ndani ya Afrika Mashariki bado hatujauheshimu utaratibu wa kuwa na utawala unaotokana na ridhaa ya wananchi kwa maana uchaguzi ulio huru, haki, wazi na usawa. Basi hilo nalo ni tatizo kubwa la kutupeleka mbele katika ushirikiano wetu. Tumepata tatizo hapa la Kenya juzi, tumelishuhudia, ilikuwa mgogoro mkubwa sana na bahati mbaya nchi wanachama nchi wa Afrika Mashariki tulikwenda kufanya suluhu, lakini hatukufanya haki. Haki hatukufanya, tuliona kabisa demokrasia imepindishwa, lakini tukashindwa kusimama kidete kiasi cha kwamba tukafikisha mahali wenzetu tukasema, basi wakae washirikiane, wazungumze.

Nasema sio utaratibu mzuri sana. Mkitaka kuwa na utaratibu mzuri, lazima msimame kwenye haki na hili ndilo lililotukuta. Hata Mugabe juzi, tunaishia tu kusema hatukutambui na kadhalika. Lakini *from the beginning* hatukusimamia haki inavyotakiwa na haki kubwa ni haki ya raia, uhuru wake wa kuchagua kiongozi anayemtaka na huo uchaguzi wake uheshimiwe.

Sasa kama hili halipatikani, nafikiri bado safari yetu ya kushirikiana itakuwa ni ndefu sana kwa sababu ili maendeleo yawe endelevu, kunahitajika kuwa na amani na utulivu katika nchi. Sasa leo Kenya kwa kipindi fulani walirudi nyuma tu kutoptaka na matatizo waliyoyapata. Tumepata matatizo Zanzibar, vile vile tumerudi nyuma na bado matatizo hayakutatuliwa, kama mwenzangu sasa hivi aliyetangulia kusema kwamba kwa Mugabe alisema haondoki kabisa. Hata Zanzibar tumeambiwa kwa sababu Serikali imepinduliwa, haitoki kwa karatasi. Haya maneno yamesemwa hapa Tanzania. (*Makofii*)

Haya maneno yamesemwa hapa Tanzania. Nasema haya siyo mambo mazuri. Siyo kitu *health* katika jamii ambayo inajaribu kujenga demokrasia iliyo ya kweli. Tumekubaliana, Katiba ipo, Sheria zipo, tuziheshimu na tuzifanyie kazi na sote tusimame kidete pale zinapovunjwa taratibu hizo. Hili lilikuwa ni jambo moja ambalo nilitaka kulisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilitaka tupate tathmini sasa kwa kiwango gani hii mikataba yetu ya ushirikiano sheria zetu na taratibu zetu zinaheshimika. Bila kupata hiyo tathmini hatuwezi kujua ni mambo gani ambayo tunahitaji kuyasahihisha. Kwa mfano, hili suala la miradi ya maendeleo. Ukiangalia huko nyuma katika *East African Community* ya mwanzo iliyovunjika, tulikuwa Kenya walikuwa na manufaa zaidi kuliko Tanzania. Lakini tujiangalie sisi wenyewe ndani ya Tanzania: Je, tunaigawa miradi hii kwa uwiano?

Tulikuwa katika Bunge hili tukizungumzia Bajeti ya Miundombinu, tulikuwa na watu wa Kusini wakilalamika kuwa watu wa Magharibi wanapata zaidi. Haya ni mambo muhimu sana kwa sababu hivi ni viashiria vya kuweza kuvunja umoja wa aina yoyote. Sasa mimi nilifikiri ni jambo la msingi sana kuliangalia hili. Kama hatukuviangalia hivyo tutapata matatizo makubwa na kwa maana hiyo naungana kabisa na hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani na nampongeza Mheshimiwa Abubakar kwa kuelezea suala la mradi wa Mkumbuu Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo ni wa miaka mingi sana. Umefanyiwa upembusi yakinifu, umekamilika, ukaratibwa. Lakini imekuwa taabu sana na taabu kila mradi unaokwenda Pemba. Hata mara hii kwa mfano bajeti ya Zanzibar asilimia 25 tu ya miradi ya maendeleo imepelekwa Pemba. Asilimia 75 haikwenda. Sasa nasema, hivi ni viashiria ambavyo inaweza kusababisha katika nchi tukapata matatizo. Mimi nilifikiri Mheshimiwa Waziri kwa hili atusaidie sana, huu mradi ukifanikiwa na hasa nimesikia Pemba kuna mafuta, tukiyachimba gati itafanya kazi vizuri zaidi. Tusaidie kwa hili limalizike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nilitaka kuzungumzia suala la tathmini. Tathmini ya kwanza ambayo naiomba sana mimi. Hapa katika Bunge letu la Afrika Mashariki tuna Wabunge wanaotoka katika nchi zetu hizi za Jumuiya. Lakini bado kila Bunge lina taratibu zake za kuwapata Wabunge kuingia Bunge la Afrika Mashariki.

Nafikiri hili haliwezi kutusaidia sana. Kama tumejenga chombo ambacho Wabunge wake watatokana na utaratibu wowote ambao unafika kule, nafikiri ile *chatter* ingewekwa *very clear kwamba* huu utaratibu hata zile Kanuni zilizoko ndani ya Mabunge yetu lazima zioane katika nchi zetu tatu, nchi zetu ambazo ni wanachama.

Kwa mfano juzi tumesikia Uganda wamekuka utaratibu wamekwenda Mahakamani wakatenguliwa nasikia baadaye wame-*appeal* hapa na sisi tulikuwa na matatizo hayo, tumekwenda Mahakamani, bado kesi iko Mahakamani.

Mimi nafikiri kwa sababu hatujakuwa na utaratibu wa aina moja. Mnapoanzisha chombo cha aina moja kama hiki kunahitajika utaratibu wa kuwapata viongozi wake wote unaowiana katika nchi zinazohusika.

Mimi nafikri hili linahitajika kufanyiwa utafiti ili kama ni *chatter* ina matatizo kama ni Kanuni zetu zina matatizo, tuoainishe Kanuni hizi ziwe na mfumo wa aina moja ili tuondokane na matatizo ambayo tunayo hivi sasa. Tumepata matatizo Kenya wakati

ule Wabunge, Bunge likawa haliendelei. Kuna matatizo ya Uganda hapo, hapa sisi bado tuna kesi *any thing can happen*. Sasa nasema haya ni matatizo kwa sababu hatukufanya uchambuzi juu ya *chatter* yenyewe, juu ya Kanuni tunazotumia: Je, zina uwiano wa kuwapata Wabunge wa Afrika Mashariki? Nafikiri hilo linatakiwa tulifanyie tathmini.

Lakini vile vile tumeanzisha Mahakama za Afrika Mashariki. Mimi nafikiri *it is a high time* kwa mambo ambayo yanahusu Afrika Mashariki tuyapeleke katika Mahakama ya Afrika Mashariki badala ya kutumia Mahakama zetu ndani ya nchi. Nafikiri nalo hilo litakuwa, hiki ni chombo tunakijenga na Taasisi zake ili zionekane zinafanya kazi na zinahudumia wale ambao wanazotumia Taasisi hizo. Katika hizi kesi za Wabunge wa Afrika Mashariki waende kwenye Mahakama za Afrika Mashariki. Nafikiri nayo hiyo ingeweza kutusaidia kama tu tutakuwa na utaratibu wa aina moja katika Jumuuya yetu ya Afrika Mashariki. Hilo lilikuwa nafikiri ni jambo moja ambalo linahitaji kufanyiwa kazi na tupate tathmini yake na tuone kwamba linafanyiwa kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni suala la uvunjaji wa haki za binadamu. Tunayo Mahakama ya Kimataifa pale Arusha. Imefanya kazi nzuri. Sasa hivi timesikia Burundi wameanzisha ya kwao na kadhalika. Mimi nafikiri kama ni Jumuuya ya Afrika Mashariki, tunahitaji kuwa na Mahakama inayohusika na masuala haya ya uvunjaji wa haki za binadamu katika Afrika Mashariki ili sasa viongozi wajue kwamba huwezi ukamipulate katika Mahakama yako ulio nayo ndani ya nchi. Kwa sababu nayo hiyo inasaidia sana ukishafanya makosa halafu ukapelekwa ndani ya Mahakama yako ndani ya nchi nayo kuna wasiwasni wa aina fulani unaingia upatikanaji haki.

Lakini ukipelekwa katika chombo ambacho kiko juu ya ile nchi yako, kidogo yule mhusika anajenga imani na jambo hilo. Mimi nilifikiri *it is a high time* kwamba hizi Mahakama za Afrika Mashariki kama kuna kiongozi yejote kavunja haki za binadamu katika nchi hiyo tumpeleke kama vile ambavyo wanapelekwa *The Hague* katika Jumuuya ya Taifa. Mimi nafikiri utaratibu utatusaidia katuondoa hapa tulipo ili wananchi wawe na imani sasa kwamba haki zetu zinaweza kulindwa.

Inasikitisha sana kuona leo nchi zetu za Kiafrika watu tunawaua sisi wenyewe, raia, ni zaidi kuliko hata pale tulipokuwa wakoloni. Leo ukichukua idadi ya watu wa Zimbabwe waliouliwa na Mugabe uki-*compare* na Smith aliyoyafanya ni vitu viwili tofauti. Ameua uchumi, ameua watu, ameua kila kitu. Nasema ni aibu kwa Afrika na hatuwezi kuendelea na utaratibu huu. Ni aibu hata yaliyotokea hapa kwetu vile vile. Nasema ni lazima tufike mahali Waafrika tuji-*address* kama sisi kweli ndiyo tulidai uhuru. Tulidai haki kwa wakoloni, basi zile haki na uhuru tuloudai, tunaziendeleza kwa uzuri kwa watu wetu. Tuna matatizo mengi sana sisi wenyewe Waafrika. Mimi nafikiri tunahitaji kuya-*address*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiri hayo yangeweza kutusaidia katuondoa hapa tulipo.

La mwisho, kawaida yangu huwa sizungumzi sana. Ningombwa sana Wizara iangalie kwa upana sana suala zima la rasilimali za Tanzania, kama kuna jambo ambalo Tanzania litaingia kwenye ugomvi ni kuachia rasilimali za Tanzania Watanzania

wenyewe wasifaidike. Kwa hiyo, suala la ardhi kwanza kukabidhiwa Watanzania wenyewe ni la msingi kabisa. Hili lisiwe na ubishi wala lisiliwe na utata. (*Makofî*)

Pili, rasilimali nyingine lazima tuhakikishe wageni wanapokuja wanaingia ubia na Watanzania, tukiacha hilo kulitekeleza, Tanzania itaingia katika ugomvi mkubwa. Hivi sasa tuna ugomvi wa wakulima na wafugaji hapa hapa Tanzania. Sisi wenyewe kwa wenyewe ugomvi upo wa wafugaji na wakulima, basi tutakapoingia na wageni wakachukua ardhi na rasilimali ugomvi utakuwa mkubwa sana. Mimi nilifikiri hii ni *area* moja ambayo Serikali lazima ikazane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tatizo letu sisi wenyewe Watanzania tuko wazito katika kufanya maamuzi. Tutawalaumu wenzetu wa Kenya, Uganda, sisi ni wazito wa kufanya maamuzi. Kupata *decision Tanzania is a night mare. The whole process* ya Serikali na kadhalika kupata maamuzi ni tatizo la msingi. Kama hili hatujalelekeza tutasema Kenya wametupa miaka mitano, watatupa tena 10 wakati wao wanaamua sisi bado tunapiga danadana tutapata matatizo. Kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Upinzani kwa kuunga mkono hoja hii ya leo. Basi naomba nimwite Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. Nafikiri na yeye anajiandaa kuunga mkono hii hoja. Mheshimiwa Mnyaa karibu sana.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo na mimi kuchangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu. Mimi sijui kama nitaweza kuiunga mkono, sidhani. Lakini labda nianze na uchambuzi wa hii hoja yenyewe. Tukitazama hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoiwasilisha hapa Bungeni, kwa ujumla inazungumzia mambo ya Sera, Mipango inayopangwa kutekelezwa, inaomba bajeti na sehemu alizotembelea. Huo ndiyo ujumla wake.

Ukitazama hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati *of course* lazima iambatane na ile ya Mheshimiwa Waziri, inatoa maoni ya Kamati na inazungumzia utekelezaji wa Wizara hii katika kipindi kilichopita na mipango inayokuja. Lakini pana tofauti kubwa sana ya hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukilinganisha na hotuba hizi mbili na hii tofauti ukubwa wake na mantiki wa tofauti hii ni mzito, hasa ukitilia maanani hotuba ya Kambi ya Upinzani, imechambua matatizo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo hotuba ya Waziri haijafanya hivyo. Imechambua matatizo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, matatizo ya nchi hadi nchi za Jumuiya na kutoa mapendekezo nini, cha kufanya ili twende vizuri katika Jumuiya hiyo tunayoitaka ya Afrika Mashariki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, tofauti hizo ningeomba Waziri anayehusika, ndugu yangu Mwenyekiti azingatie, aangalie vizuri maoni ya Kambi ya Upinzani ambayo yanatoa mwelekeo wa kuwa na Jumuiya madhubuti tukiondoa hizi

dosari. Hizi dosari zimezungumzwa hata zile za kwetu wenyewe nchini, pia Kambi ya Upinzani imezifafanua ili tuwe na Jumuiya nzuri. Huo ni mchango wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ambayo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amegusia kidogo, lakini mimi nataka nigosie kwa lengo lingine vile vile ni suala la Wabunge wa Afrika Mashariki au upatikanaji wa Wabunge wa Afrika Mashariki. Katika mtindo uliopo hivi sasa, ni kwamba kila Bunge la nchi mwanachama ndiyo lina utaratibu kwa kutegemea kanuni zilizopo za kuwapata Wabunge wa Afrika Mashariki. Migogoro iliyotokea kaizungumza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Sasa nini cha kufanya?

Kwa ufupi na kabla ya kusema nini cha kufanya, inatia aibu kuona kwamba mfumo wetu tulio nao sisi Tanzania kwa mfano wa kuwapata Wabunge wa kuwakilisha Afrika Mashariki unatia aibu pale inapokuwa suala hili katika Kanuni zetu na tunavyowapata Wabunge ni kichekesho, hasa kwa kutilia maanani, tuchukue mfano uliopo hivi sasa, kwamba Wabunge wa Afrika Mashariki wanaotoka Tanzania, nchi ambayo ni ya Vyama vingi, uwakilishi wa Vyama vingi uliomo, kwa mfano *CUF*, ina Wabunge 32 ndani ya Bunge hili.

CHADEMA ina Wabunge 11 ndani ya Bunge hili. *UDP* ina Mbunge mmoja. Lakini Bunge hili lilipofanya uteuzi au uchaguzi wa kupata uwakilishi wa Tanzania kwenda Afrika Mashariki, Chama cha Wananchi *CUF* kinacho Wabunge 32, Chama cha CHADEMA kinacho Wabunge 11, vyote havikuwakilisha katika Afrika Mashariki, kinawakilishwa na Chama cha *UDP* chenye Mbunge mmoja na maamuzi hayo ni ya Bunge hili. Hatuwezi kuhoji maamuzi ya Bunge, lakini utaratibu uliotumika sivyo. (*Makofi*)

Hili sasa *solution* yake ni Katiba yenyewe ibara ya 50 Katiba ya Afrika Mashariki ifanye utaratibu iandaye utaratibu ambao nchi itapata Wabunge wenyewe uwakilishi ambao una uwiano wa vyama vya upinzani na vyama vinavyotawala. Itoke kwenye katiba yenyewe ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Waziri nafikiri umeshalichukua hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, hii miradi inayotekelawa kikanda. Tumepata taarifa hapa, inasema hivi karibuni ndiyo Zanzibar nayo imeingizwa na hapo mwanzo kwanza miradi inayotekelawa kikanda Zanzibar haimo na hivi karibuni ndiyo imeingizwa kutakuwa na mradi wa bandari ya Makurubi na hii bandari na *Airport*. Lakini kama alivyosema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Pemba imeachwa kabisa na huo mradi wa Mkumbuu na Rasi Mkumbuu, Naibu Waziri wa Wizara hiyo ya Afrika Mashariki anajua *advantage* ya rasi hiyo, anajua faida ya rasi hiyo, anajua mipango ya rasi hiyo toka enzi ya ukoloni mpaka ikaingizwa katika mipango ikajadiliwa na Jumuiya na kwa nini isiingizwe? Ni kitu ambacho kinacheckesha sana. Hili ni suala la kufikiriwa, sitaki niendelee zaidi.

Lakini hata hivi karibuni, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri alijibu swalilinalohusiana na hiyo hiyo miradi ya Afrika Mashariki na akataja mlolongo wa miradi, lakini ikakosekana hata meli ambayo itaweza kuunganisha nchi hizi, kuunganisha

Bandari ya Mombasa, Tanga, Zanzibar, Pemba, Dar es Salaam na Mtwara. Ikatajwa miradi ya barabara na reli tu. Mipango hiyo ya Afrika Mashariki ikiwa hivyo ndivyo ilivyo ina matatizo. Kwa sababu usafiri wa baharini ndiyo usafiri unaotegemewa kukuza biashara kwa kiwango kikubwa. Meli ndiyo yenye uwezo wa kuchukua bidhaa kwa wingi au makontena kwa wingi kuliko usafiri wa barabarani labda na reli nayo ina uwezo huo. Kwa hiyo, ili kuimarisha hii mipango na miundombinu ya Afrika Mashariki mradi wa kutafuta meli ambayo itaunganisha bandari hizo ulikuwa ni wa lazima. Hatuoni katika mpango wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili Mheshimiwa Waziri atupatie maelekezo atupatie ufanuzi, vinginevyo itatupa taabu kidogo kufahamu sisi wengine. Mimi nilitaka Mheshimiwa Waziri akija akifanya majumuisho yake atufafanulie hizi Wizara ambazo sio za Muungano, Kilimo, Uvuvi, Afya, Zanzibar inawakilishwa vipi kule? Huwezi kutuambia tunashirikiana tu na Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano inashirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar. Kwa hiyo, tunashirikiana. Hiyo siyo *solution*. Tunataka Wizara ya Afrika Mashariki, Zanzibar inawakilishwa vipi kwa zile Wizara ambazo sio za muungano. Atupe mfano mzuri, atupe mipango mizuri inawakilishwa vipi. Tujiridhishe, hii kuburuzana, kidogo inachokesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafanyakazi wa Afrika Mashariki, tunaambiwa hapa sio sehemu yake vizuri, liko Wizara ya Fedha kwa sababu Jumuiya ilikwishakufa, lakini kuna kitu kimoja ambacho ningeshauri Wizara hii ya Afrika Mashariki kuhusu suala la wafanyakazi, ikiwa makisio ya Watanzania kulipwa ilikuwa ni shilingi bilioni 450 na mpaka leo wamelipwa shilingi bilioni 117.

Hizo shilingi bilioni 333 ambazo hapa wakiulizwa wahusika wanassema hatuna takwimu, inakuwaje wafanyakazi kutoka Tanzania, Serikali ya Jamhuri ya Muungano isiwe na takwimu halisi za watu hawa? Ni aibu! Sasa kama Jamhuri ya Muungano haina takwimu za waliokuwa wanafanya kazi Afrika Mashariki, basi hii Wizara ya Afrika Mashariki iliyopo hivi sasa itoe hizo takwimu. Kwa sababu kumbukumbu ziko na hizo nchi wanachama ndiyo ikiwa ni pamoja na Kenya na Uganda na Tanzania itoe takwimu iwapatie Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili hili suala, kadhia hii ya wafanyakazi wa Afrika Mashariki imalizike. (*Makofsi*)

Mheshimiwe Mwenyekiti, naomba nzungumzie suala la wafanyakazi katika Wizara hii. Katika Mkutano wa Kumi, kama kumbukumbu zangu ziko sahihi, Mheshimiwa Ali Ameir aliuliza swali hapa Bungeni la kuhoji kwa nini Wizara hii ya Afrika Mashariki ambayo ni ya Muungano hakuna wafanyakazi kutoka upande mwagine wa Muungano wa Zanzibar. Jibu alilopewa na Mheshimiwa Waziri wa Muungano wa wakati huo Mheshimiwa Hussein Mwinyi, ilikuwa ni kwamba matangazo yanapelekwa, nafasi zinatangazwa, lakini Zanzibar hakuna wasomi.

Kwa kweli nilisikitika na linasikitisha, na likaishia hivyo hivyo tu. Nikapata bahati nzuri, nilipotoka nje nikakutana na Mheshimiwa Waziri wa Muungano wakati ule Mheshimiwa Hussein Mwinyi, nikamwambia sikuridhika na jibu ulilomjibu Mheshimiwa Ali Ameir. Haiwezekani kusema kwamba mnapeleka majina, Serikali ya Mapinduzi

Zanzibar haileti majina kwamba wanataka kuajiri katika Wizara hii ya Afrika Mashariki, wanataka waajiri watu kutoka upande mwagine wa Jamhuri ya Muungano, lakini kila wakipeleka barua, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haipeleki majina na akajibu kwamba hakuna wasomi. Hawatimizi viwango vinavyohitajika. Nikamwomba Mheshimiwa Waziri wa Muungano wa wakati ule Mheshimiwa Mwinyi, nikamwuliza nikamwambia hilo sikubaliani nalo. Niambie mimi nikuletee majina mangapi ya watu wana-*qualification* ya hizo unazohitaji. Akaniambia niletee na ukiniletea sisi tutawaajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimpelekea majina ya watu zaidi ya sita au kama sita hivi ambao mpaka *PhD level* wamo, watu wenye *qualification* ambazo zilihitajika. Labda Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki atujibu: Je, amepata *list* hiyo kutoka kwa Waziri mwenzake ambaye sasa hayuko katika Wizara hiyo? Je, hawa watu wataajiriwa lini, tutawaona? Kama kikwazo ni *qualification*, hao watu wana *qualification*. Kutakuwa na kikwazo gani tena kama hawawapati kutokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sisi tumeshawaaletea *list*, mbona mpaka leo hatujaona hizo ajira zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masuala ambayo yakiachiliwa yakiendelea, haya ndio hiyo mipasuko midogo midogo mpaka kutatokea nyufa mpaka nyumba inaanguka. Tusiachilie, tusiruhusu, haya matatizo madogo madogo yanakirihisha. Hatuwezi kuambiwa Zanzibar hakuna wasomi wakati watu wako Mitaani, *taxi driver* na wana elimu, hawana kazi. Tusiruhusu kwamba lazima tupate watu wanaotoka upande wa chama kimoja. Tukiendelea na mtindo huo, mwisho hatutaendelea. Maana lazima apatikane mtu apelekwe Jumuiya ya Afrika Mashariki awe anatokana na upande wa chama kimoja. Ikitakiwa hivyo, kweli, wengi watakosa nafasi. Lakini watu wako na tunataka tuone kwamba hii Wizara ina sura ya kimuungano. Sio nyote mkae humo mnatoka upande mmoja. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru. Ahsante. (*Makofifi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Mnyaa. Hivi umeunga mkono? Naomba Waheshimiwa Wabunge, Msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwisho mchana huu kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, pamoja na Wataalam wote ambao wameandaa hii bajeti. Lakini niseme tu kwa utangulizi kwamba bajeti ya Wizara hii ni finyu sana. Kwa malengo tulikuwa nayo katika nchi yetu kwa kweli kazi zilizopo na kwa pesa zilizokuwepo hazikidhi haja. Lakini ndio hali halisi, bajeti imeshapangwa na hatuna budi kuipitisha. Lakini sasa ni changamoto kwa Wizara hii. Kwanza kujitafutia bajeti kubwa, wana jukumu hilo, wana changamoto hiyo. Kwa sababu wao kusukuma mambo katika Afrika Mashariki na kukuza uchumi katika nchi moja za Afrika Mashariki sisi kama Tanzania hatuna

budi kufanya kazi ya ziada hatimaye uchumi wetu ukiwa mzuri na hatimaye bajeti ya Wizara hii iweze kuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kwanza miradi ya maendeleo. Nchi hizi tatu za kwanza za Afrika Mashariki na sasa tumepata nchi mbili nyingine za Rwanda na Burundi, tumeongezeka. Kwa hiyo, kazi zimeongezeka, biashara zimeongezeka, majukumu yameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo inatekelezwa katika jumuiya hii kwa nchi moja moja, lakini kama ni mradi wa Afrika Mashariki halafu inapobainisha kwamba mradi huu utatekelezwa Tanzania na mwekezaji amepatikana kwa ajili ya kuwekeza hapa. Lakini ni mradi wa Afrika Mashariki, utaratibu wake nimeuona, lakini siyo *healthy*. Ni sawasawa tu na kuiambia kwamba Tanzania ndiyo inatafuta mradi wenyewe.

Lakini katika kikao cha pamoja nina hakika kila nchi itavuta kwake. Mimi naona bado tunahitaji *structure* nzuri zaidi. *Formula* nzuri zaidi ya kushirikiana sisi nchi za Afrika Mashariki kubainisha miradi pamoja na kwamba uko utaratibu huo. Lakini nasema siyo *health* kwa sababu kila nchi itavuta upande wake japokuwa *priority* ukitazama mafanikio mazuri ya mradi ule unatakiwa uende Tanzania, lakini kwa vile Kenya pia wanaona watapata maslahi kidogo, wao watasema na sisi tunautaka huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mantiki kubwa ya mradi ule kunufaisha Afrika Mashariki pengine ungehitajika ufanyike Tanzania zaidi. Nitoe mfano mmoja, sisi Tanzania tumepata mkopo wa *MCC, Millennium Challenge*. Miradi mingi iliyokuwepo ya *MCC* kwa upande wa Tanzania kuna mradi ambao utaunganisha na nchi jirani ya Kenya ambayo ni barabara ya kutoka Tanga kwenda Horohoro. Barabara ile ikishakamilika, sisi tunapata wasiwasi kama Tanzania hatutafaidi zaidi kuliko watakavyofaidi Kenya. Pamoja na kwamba mradi wa *MCC* unatekeleza kwetu na barabara itajengwa kwetu. Lakini watafaidika zaidi Kenya kuliko sisi kwa sababu gani?

Kwa sababu barabara ile ikishakuwa ya lami na ni nzuri, Bandari yetu ya Dar es Salaam na matatizo yake yaliyokuwepo sasa hivi na Bandari ya Tanga iliyokuwepo sasa hivi ambayo huwezi kuegesha meli kubwa na kupakua mizigo, tunashindwa *ku-compete* na Bandari ya Mombasa. Sasa hiyo *competition* iliyokuwepo kati ya Bandari ya Dar-es-Salaam na Mombasa, nina hakika wafanyabiashara watapeleka mizigo yao isafirishwe katika Bandari ya Mombasa, kuliko kubaki Dar-es-Salaam na matatizo ya *congestion* yaliyokuwepo pale Dar-es-Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiingia katika suala zima la soko la pamoja, kuna masharti tumewekewa hapa, kuondoa vikwazo vya kibashara, uhuru wa wananchi kwenda wanapotaka *East Africa*, uhuru wa kutoa huduma kibashara *East Africa*, uhuru wa kuwekeza mitaji, sasa tukishaweka uhuru huo hatuwezi tukamkataza mfanyakibashara asipeleke mizigo yake ikasafirishwa kwenye Bandari ya Mombasa kwasababu barabara tayari ni nzuri ni ya lami. Popote utakapotoka kutoka Mbeya, utafika mpaka Mombasa kwa barabara ya lami. Utatoka Dar-es-Salaam utafika mpaka Mombasa kwa barabara ya lami.

Kwa hiyo, hii tayari naona ni kikwazo, lakini nasema hii miradi ya Afrika Mashariki, pamoja na kwamba Serikali ya Tanzania ina mpango wa kujenga Bandari ya Tanga ili kupunguza mzigoto uliokuwepo pale Dar-es-Salaam. Tanzania ina mpango wa kujenga Bandari ya Mtwara kusaidiana na Bandari ya Mombasa. Tanzania inajenga sasa Bandari ya Bagamoyo ili kusaidia Bandari ya Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi kama Afrika Mashariki na hii kama Wizara ya Afrika Mashariki mnapotafuta wawekezaji ili kuja kuwekeza katika miundombinu kwa mfano. Pamoja na kwamba Tanzania inatafuta mwekezaji kwa ajili ya Bandari ya Tanga na Mtwara, ninyi mmefikia wapi kusaidiana na Serikali hii ya Tanzania katika miradi ya Afrika Mashariki, kwa sababu bandari itakayojengwa Tanga, itatusaidia sana katika kuongeza mapato hapa Tanzania. Pamoja na kwamba sasa hivi Kenya katika Bandari ya Mombasa wana mpango kabambe wa miaka mitano kuimarishe Bandari ya Mombasa ambayo itaweza kupokea *super tankers* kutoka Japan, kutoka Amerika, kwa ajili ya matumizi mbalimbali na ni meli kubwa, sisi bado hatuna *facility* hiyo hata katika Bandari ya Dar-es-Salaam.

Lakini Bandari ya Mwambani ambayo itakuwepo Tanga, kina chake inaweza ikachukua meli kama hizo, lakini tukikaa kimya na hatuchukui hatua za makusudi ambazo ni *aggressive* tutabaki hivi hivi, tutashindwa sisi ku-*compete* na ndugu zetu wa Kenya na sisi kama Tanzania, bahati tuliyopewa, ninyi mnafahamu kwamba tunapakana na nchi zaidi ya tano. Sina haja ya kuzitaja zile ambazo zinapendelea sana kupokea mzigoto yao kutoka Bandari ya Dar es Salaam, Kongo, Rwanda, Burundi na Uganda. Hizo peke yake Bandari ya Dar-es-Salaam peke yake haitoshi. Bandari ya Tanga na Dar-es-Salaam, haitatosha, Bandari ya Mtwara peke yake na hizi nyingine hazitatosha. Tuna *facility* ya kubebea mzigoto mingi na ikatosheleza hizi nchi ambazo nimezitaja, sikutaja Malawi, sikutaja Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia kwako nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, kwamba hebu jaribuni kuwa *aggressive* kidogo katika kutafuta miradi ya uwekezaji hasa katika miundombinu ili kuweza kuisaidia Tanzania katika miradi hii ambayo itawainua wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu Tanzania hivi sasa tunashindwa *ku-compete* na ndugu zetu majirani. Ni kwa sababu *factor* ziko nyingi, moja ni *tarrif* ya umeme. Pamoja na kwamba kule Kenya wana matatizo ya umeme, lakini *still* tarrif yao iko *reasonable* kwa ajili ya kuhamasisha watu wa viwanda na biashara ili kukuza ule uchumi.

Leo Kenya wanajitegemea kibajeti kwa asilimia 95, tayari sisi hapo tumeachwa mbali sana. Lakini wamefanya miujiza gani? Haiwezekani Kenya ika-*compete* na Tanzania katika ardhi ya kilimo, haiwezi ika-*compete* na Tanzania katika eneo la bandari ambalo ni kubwa, haiwezi ika-*compete* na Tanzania katika vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme, lakini *still* Kenya imetupita kwa sababu wao wako *aggressive* na nikisema *aggressive* nina maana kwamba wako tayari mpaka kupigana kuhakikisha

kwamba mradi ule wanauchukua. Wako *determined*, hawaoni haya. Sisi tukiambiwa kidogo aah, basi sisi majirani tutawaachia ninyi, tusiende hivyo. Kila mmoja avute kwake, lakini pamoja na hayo, tunashirikiana kwa utaratibu ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni *sector* nyingine ambayo nasema kwamba katika *sector* ya viwanda tunashindwa ku-*compete*, lakini sisi bado tunaweza kuzalisha umeme. Pamoja na maporomoko ya maji mengi ambayo hayajatumiwa kama *Stiglass Gorge* na mengine mengi, lakini tuna mikaa ya mawe, tuna gesi sasa hivi, hivi tunashindwaje kuanzisha miradi ya umeme na tukawaambia ndugu zetu wa Afrika Mashariki, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, kwamba tutakuwa na *megawatts* kadhaa za kuwauzieni kutokana na rasilimali ya gesi tuliyokuwanayo, kutokana na rasilimali ya mkaa wa mawe tuliyokuwa nayo ili hatimaye na sisi tuweze ku-*compete* na tukuze uchumi wetu.

Sasa nashauri kwamba miradi mingi ambayo Serikali yenewe ya Tanzania inatafuta, lakini na vilevile Afrika Mashariki, kama Wizara ya Afrika ya Mashariki, tujitahidi na sisi tutafute wawekezaji *serious* kabisa ambao wataweza kuingia katika miradi hii na hatimaye tuweze ku-*compete* vizuri na twende vizuri na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema leo Rwanda, ambayo ni nchi ndogo kabisa na imetoka kwenye matatizo makubwa sana, lakini tayari imekwishatupita Tanzania katika mambo mengi sana. Siwezi kusema kwamba tunalingana kiuchumi, lakini wamekwishakuwa *advanced* katika *sector* fulani fulani ambazo Tanzania bado tuko nyuma na wao ndio wametukuta sisi. Tumewasaidia katika matatizo yao, tumepokea wakimbizi wao na hatimaye sasa hivi wametuacha nyuma wao wanasonga mbele. Nilikuwa nataka kusositiza tu kwamba Wizara hii ya Afrika Mashariki, itusaidie katika kutafuta wawekezaji ili na sisi tuweze ku-*compete fairly* na hatimaye tuweze kujitegemea katika bajeti yetu wenyewe ili twende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana na nina unga mkono hoja. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru wale walioomba kuchangia. Tayari wote wamepata nafasi ya kuchangia na msemaji wetu wa mwisho amekuwa Mheshimiwa Rished, lakini tutakaporudi mchana tutaanza moja kwa moja na Mto hoja, kwa maana ya Naibu Waziri, atapata nafasi ya kuchangia. Kwa mujibu wa kanuni, ye ye anatakiwa achangie kwa dakika 15 lakini Waziri, saa moja. Ila wao wenyewe wanaweza wakakubaliana wanagawanaje huo muda ili waweze kumalizia hoja yao. Mheshimiwa Zitto, unachangia hii au hutachangia?

MHE. KABWE Z. ZITTO: Ndio, nitachangia.

MWENYEKITI: *Okey*, basi nitakupa nafasi baada ya matangazo haya, kwa sababu bado muda wangu unaniruhusu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaendelea, naomba niseme wale Wabunge, ambao wako kwenye Jimbo lao la Uchaguzi hapa ndani, niliwatambulisha mchana ila hawakuwepo, wengine basi naomba niwatambue. Yuko Mheshimiwa Amani Kabourou, naona hayuko hapa ndani sasa hivi na Mheshimiwa Janet Mmari, naona hayuko hapa ndani sasa hivi.

Waheshimiwa Wabunge, nafasi inatosha. Tulikuwa tunafanya mawasiliano na Mheshimiwa Zitto Kabwe, alikuwa anafikiri *either* achangie hoja hii ama hoja ya madini, kwa hiyo, amekuwa akinianidikia *note* vijiji vingi mpaka vimenichanganya hapa. Sasa maamuzi yake ya mwisho yamekuwa ni nini? Sasa kama maamuzi yako ya mwisho ni ya kuchangia hoja hii, sina *objection* kwasababu muda wangu unaniruhusu, nitakupa hiyo nafasi ya dakika 15, umalize halafu jioni tutaendelea na utaratibu mwingine. Sasa namwita Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ni kweli nilikuwa najaribu kufikiria kama nichangie hoja hii au nisubiri kwa sababu ya utaratibu wetu wa kwamba ukishachangia mara kadhaa hupati nafasi ya kuchangia sehemu nyingine, lakini tuna taratibu tu nyingine nitajaribu kufanya jinsi gani ya kufanya kuweza kutoa maoni yangu kuhusiana na hoja itakayokuja ya Wizara ya Madini. Kwa kuwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kashaunga mkono hoja hii, katika masuala ya kiitifikasi, siwezi kuipinga hoja hii.

Kwa hiyo, naungana mkono na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa ajili ya kuunga mkono, lakini pia Mheshimiwa Waziri anayeongoza Wizara hii ni kijana mwenzangu na sisi vijana ni lazima tuungane mkono. Bahati nzuri leo mchangiaji wa kwanza kuchangia alikuwa ni kijana mwenzetu pia. Kwa hiyo, tunaendelea tu kuwapa moyo watu wa Wizara ya Afrika Mashariki, kwa ajili ya kuendelea kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu, kwamba kwa mara ya tatu sasa, kwa maana ya bajeti ya 2006/2007, 2007/2008 na 2008/2009 nimepata nafasi ya kuchangia Wizara hii. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, mpaka tutakapomaliza kipindi hiki cha Bunge, niwe nimechangia kila bajeti ya Wizara hii, kwa sababu mimi ni muumini mkubwa sana wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ninaamini kabisa kwamba Jumuiya hii itatusaidia sana kama eneo letu hili huko tunakokwenda.

Napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais Paul Kagame wa Rwanda, kwa kupewa dhamana hiyo na viongozi wenzake katika mukutano uliofanyikia Kigali na vilevile Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda, kwa kuwa Mwenyekiti wa *Council of Ministers* ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, ningependa tuangalie kwamba hivi sasa tunafanya *rotation* ya Wenyeviti wa Jumuiya na kwa mujibu wa taratibu ambazo zipo sasa. Nadhani baada ya Rais Kagame, atafuata Rais Nkurunzinza na baadaye Kiti kitakuja kwa Rais wa Tanzania. Kwa maana hiyo ni kwamba ukiangalia Rais wa Tanzania ataweza kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hii mwezi Juni, 2010.

Nadhani ni muhimu Wizara ya Afrika Mashariki ya Tanzania ijaribu kwanza kuangalia uwezekano wa kuandaa ajenda yetu kwamba utakapokuwa Mwenyekiti wa Jumuiya, ni nini itakayokuwa ajenda ya Tanzania ndani ya Jumuiya, ili muda wote huo ambao sisi ni Wenyevititweze kuwa tuna ajenda ambayo tunataka kuitekeleza na baadaye tuweze kuitolea ripoti na ndio jinsi ambavyo wenzetu katika Jumuiya ya Ulaya wanafanya. Kwamba mtu anajua kabisa baada ya miaka mitatu Rais wetu atakuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Ulaya, anaweka ajenda kwamba sisi tunataka tutekeleze suala hili. Kwa hiyo, inakuwa ni rahisi sana mambo mbalimbali kuweza kutendeka.

Sifahamu kama Rwanda, wana ajenda lakini sisi bahati nzuri tutakuwa Mwenyekiti, wakati tunaanza kutekeleza mwaka wa kwanza wa soko la pamoja, *Common Market*. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuweze kuangalia zile changamoto ambazo ziko kwenye *common market* na Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Abubakar, amezungumzia zile changamoto ambazo tunapaswa kuziangalia ameziorodhesha nydingi sana ambazo inabidi Wizara iziangalie. Sisi tu- *identify* moja au mbili au tatu ambazo zitafanya ajenda ya Tanzania ili mpaka tutakapokuwa tumemaliza Uenyekiti wetu tuwe tumefanya kitu fulani kwa ajili ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kutoa tu taarifa kwa Wizara hii kwamba pale Kigoma tuna jengo la muda mrefu sana linaitwa *Kaizof*. Lile jengo lilijengwa na Wajerumani kwa ajili ya Mfalme wa Ujeruman na hivi sasa tunalifanya matengenezo.

Napenda kutoa pendekezo kwamba katika *summit* ambayo Rais wetu atachukua Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kuwa tuna nchi mpya kama Burundi ambayo imeingia katika Jumuiya na Rwanda ambayo pia ni jirani zetu, ningependekeza sasa tuondokane na tabia ya *summit* zote kufanyikia Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Summit* ijayo ambayo ni Rais wetu atakuwa Mwenyekiti, ifanyikie Kigoma. Itatusaidia sana kwa maana ya kuupandisha Mkao ule, kuutangaza katika eneo la Afrika Mashariki, lakini pia itatusaidia sisi wenye watu wa Kigoma kama Wizara itakuwa imetukubalia tuanze kijiandaa mapema kwa ajili ya masuala kama ya mambo kama ya *accommodation*, matayarisho ya Marais, watacaa wapi na masuala kama hayo? Kwa hiyo, nilikuwa naomba nitoe pendekezo hili kwa Wizara, ijaribu kuliangalia na mkitukubalia sisi watu wa Kigoma tutafanya kazi kuweza kupata heshima hiyo, tuweze kupata nafasi ya kuweza kujitangaza katika eneo letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la umoja wa forodha. Kambi ya Upinzani imetua mapendekezo fulani na mojawapo limesema kwamba tufanye tathmini kuweza kuangalia toka tumeanza umoja wa forodha mwaka 2005 mpaka sasa ambapo tunajiandaa kuingia kwenye soko la pamoja, nchi yetu imeweza kufaidika namna gani. Nilikuwa naangalia hapa takwimu ambazo ziko kwenye hotuba ukurasa wa 43 wa hotuba ya Waziri. Mwaka mmoja kabla ya Umoja wa Forodha kuingia na mwaka mmoja baada tulikuwa tuna hali mbaya sana ya kibiashara kati ya sisi na wenzetu wa nchi nyininge kwa maana ya Uganda na Kenya.

Lakini nimeona takwimu za mwaka 2007 tuna mahusiano chanya ya kibiashara kwa maana ya *positive balance of trade* kwamba *export* zetu ziliwa ni dola 120,000,000/= na *import* zetu kutoka katika eneo hili ni dola 106,000,000/=.

Kwa hiyo, hii inaonyesha kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo tunafanya vizuri. Kwa hiyo, tathmini ambayo Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ameipendekeza ni muhimu ifanyike ili tuweze kujua ni maeneo yapi haya ambayo tunafanya vizuri ili tuweze kuongeza nguvu kwa sababu hili ni jambo la msingi sana kama tumeweza kuwa na *positive balance of trade* na Kenya, kama tumeendelea kuwa na *positive balance of trade* na Uganda na sasa hivi Rwanda na Burundi ambao kimsingi ni masoko yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme, maana kuna Mbunge mmoja alisema hapa kwamba Rwanda na Burundi sio soko na kadhalika. Rwanda ina jumla ya watu 10,000,000 msione ni nchi ndogo, ina watu wengi sana. Burundi ina jumla ya watu milioni 7.8, kwa hiyo, hili ni soko la watu 18,000,000 na ni soko la watu ambao wanatumia. Wanyarwanda wanatumia sana, Warundi wanatumia sana.

Kwa hiyo, tuone haya maeneo ambayo tuna *positive balance of trade* na Kenya na Uganda na tujaribu kuona huko Rwanda na Burundi ni maeneo yapi ambayo tutaweza kuongeza nguvu ili tuendelee kuwa ni watu ambao tunafaidika na umaja huu na tuwahamasisho wafanyabiashara wetu waweze kuchukua hizo fursa sasa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri, achukulie kwa umakini sana, yaani *very seriously*, pendekezo ambalo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, katika Wizara hii amelitoa kuhusiana na tathmini ya wapi ambapo tumefika katika suala zima hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa napenda tuweze kuangalia kwa sababu Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Rwanda na Burundi bado hazija-*accent* kwenye ile *protocol* ya Umoja wa Forodha.

Nadhani kuna umuhimu mkubwa sana wa nchi hizi ziweze kusaini itifaki hii mapema. Ninasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mwenyewe ni mdau, anatoka kwenye Mkoa ambao unapakana na nchi tatu ambazo ni wanachama wa jumuia, Rwanda, Burundi na Uganda.

Sisi Kigoma tunapakana na Burundi na tuna mipaka miwili ambayo tungeitumia vizuri ingeweza kutusaidia sana. Kuna kule Mabamba kwa Mheshimiwa Kijiko. Mpaka ule wa Mabamba ungeweza kusaidia sana watu wa Kibondo katika shughuli za kibiashara kwa sababu watu wa Burundi wanakuja kununua bidhaa zao, mpaka mbolea wanakuja kununua upande wa Tanzania. Tuna mpaka wa Kagunga ambao ungeweza kusaidia sana. Hivi sasa kuna mchakato wa ujenzi wa soko, siwezi kuliita ni soko la kimataifa, lakini ni soko ambalo linaweza likasaidia sana biashara kati ya Burundi na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kwa sisi watu wa Kagera najua huwezi kusema wewe mwenyewe kwa sababu ni Waziri, naomba nikusemee na mimi ambaye natokea Kigoma na Wabunge wengine wote wa Kigoma, kwamba kuna umuhimu wa kuwaomba wenzetu wa Rwanda na Burundi, waweze kusaini itifaki hii

mapema ili na sisi tuweze kufaidika na biashara ya mpakani bila vikwazo kama jinsi ambavyo wenzetu wa Namanga wanavyofaidika.

Tungependa sana mipaka ya Kagunga na mipaka ya Mabamba kule Kibondo, wananchi kule waweze kufanya biashara bila vikwazo vya aina yoyote. Wanapata taabu sana hivi sasa na bahati mbaya kule ni mpakani, kuna wanajeshi, wanajeshi wanawasumbua wananchi wanapotaka kuuza bidhaa zao, laki ni wakishaingia kwenye hii itifaki itaweza kusaidia sana kuweza kuokoa hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la soko la pamoja, *common market*. Nafahamu kwamba tayari wale washauri wameshatoa ile *proposal* ya *common market* na tayari Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje imejadili na ninadhani hatua hii ya *common market* ndiyo hatua tunasema *sensitive* sana. Ni hatua nyeti sana ya umoja. Baada ya hapo, umoja wa sarafu na umoja wa kisiasa ni vitu ambavyo vitafuata tu, lakini eneo ambalo ni tete sana ni eneo la *common market*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba watafute njia yoyote ile wajaribu na kwa sababu tuko hatua za mwisho na *negotiation* zimeanza, wafanye uwezekano wa kukutana na Wabunge wote na Wabunge wa Afrika Mashariki, wanaotoka Tanzania, tuje tukutane hapa Wizara itueleze mipango ikoje. Wabunge wetu ambao wako katika Bunge la Afrika Mashariki, nao pia wapate fursa kwa sababu hivi sasa hakuna fursa ambapo Wabunge wa Afrika Mashariki wanakutana na wapiga kura wao kama mwenyewe Mwenyekiti, alivyosema na kuwaeleza kuna changamoto zipo ambazo zipo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata wasiwasi kwamba wakati mwingine Wabunge wetu wanakwenda kule, ni vizuri wanatetea *National Interest*, ni vizuri sana, lakini pia sio wakati wote. Ni lazima mwonekane kwamba ninyi mnavutia tu Tanzania, kwa sababu ni lazima mfanye *strategic engagement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wabunge wetu wajiepushe kidogo na ile hali ya kupingana tu labda na Wakanya au na Waganda, kwasababu iko siku watawahitaji katika maamuzi fulani ambayo yatakuwa na faida na nchi kwa hiyo hiyo *strategic engagement*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa suala hili la *common market* Wizara na Wabunge, tuweze kukutana, tuweze kuzungumza na kuweza kuona ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukashughulikia suala kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwasababu kuna mapendekezo la mapato ya Jumuiya, sasa yatokane na uwezo na ukubwa wa uchumi wa nchi au labda sehemu fulani ya *VAT* ichangie katika Jumuiya. Haya ni mambo ambayo lazima tuweze kuyajadili vizuri. Katika miradi inayokuja sasa, kwa kuwa Ziwa Tanganyika liko *shared* na Tanzania na Burundi, muweze kuangalia miradi ambayo inaweza ikaingia katika Ziwa Tanganyika. Naungana mkono na Mheshimiwa Mnyaa, pia kuhusiana na miradi ya kule Pemba, maana Pemba ndio inayopakana na Mombasa zaidi, kwa hiyo, ni muhimu sana kuweza kuwa na miradi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la kuwa na *Foreign Policy Coordination*. Nadhani twende mbele kidogo, tuwe na *common foreign policy*, tuwe na *common defence and security policy*, ni muhimu sana. Matatizo ambayo yalitokea Kenya yalisababisha mgawanyiko mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka kwamba Rais wetu alichelewa kumtambua Rais Kibaki, mpaka matatizo ya Kenya yalipokwisha, lakini Rais Museveni, ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa *East African Community* akamtambua Rais Kibaki na ikaonekana ni kwamba huu ni uamuzi wa Afrika Mashariki, wakati ulikuwa ni uamuzi wa Uganda peke yake na uliweza kusababisha hata matatizo ndani ya Kenya. Kwa hiyo, nilikuwa ninaona kuna umuhimu mkubwa tusiwe na *foreign policy coordination*, tuwe na *common foreign policy* ili kuweza kuhakikisha kwamba maslahi yote ya mambo ya nje yanayokuwa *shared* na nchi zetu yanajadiliwa kwa pamoja na kutolewa maamuzi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la Wabunge wa Afrika Mashariki. Mimi nadhani nakubaliana kabisa na watu ambaao wanatoa mapendelekezo kwamba tuangalie mfumo wa uchaguzi huu. Njia moja ya kufanya Jumuiya ya Afrika Mashariki ifahamike kwa wananchi ni kutumia mfumo wa *propositional representation*, kuchagua Wabunge wa Afrika Mashariki. Kama nchi inatakiwa kuwa na Wabunge tisa, kila Chama kiweke orodha yake ya Wabunge tisa, kinaipelea Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Vyama vinakwenda, vinafanya kampeni, kila Chama kinaelezea msimamo wake kuhusiana na Afrika Mashariki, wananchi wanapiga kura. Mnaangalia *percent* ya kura ambazo kila Chama kimepata, mnawagawa wale Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hapa ni lazima tuangalie na tusitoe tu majibu mepesi kwenye suala la mahusiano kati ya nafasi ya Zanzibar na nafasi ya Jamhuri ya Muungano. Kuna umuhimu mkubwa sana, Wabunge wanaokwenda kwenye Bunge la Afrika Mashariki waweze ku-*reflect* sura ya kisiasa ya Zanzibar. Ni muhimu sana na wala nchi haitakuwa imeathirika chochote kwa sababu huyu mtu atakapokwenda kule hatakwenda kutetea *CUF* au *CCM*, hatakwenda kutetea Zanzibar *as* Zanzibar, atakwenda kule kuongeza nguvu kwa *United Republic*. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana suala hili, tuondokane na ile tabia tu ya kutoa majibu tu ilimradi kutoa majibu, hapana. Tujaribu kuangalia kwamba ni vipi ambavyo sura ya Wabunge wetu kule inaweza ikawa *reflected* kutohana na hali ya kisiasa ilivyo Zanzibar.

Ni muhimu sana na vilevile kuangalia tunaliweka Baraza la Wawakilishi katika hali gani? Kwa sababu ni ukweli kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo sio ya muungano yanajadiliwa katika Bunge la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tutafute njia yoyote ile ambayo inaweza ikalifanya Baraza la Wawakilishi au Kamati ile inayohusika na *Regional Intergration* ndani ya Baraza la Wawakilishi ili iwe *properly brief* na iweze kushiriki katika masuala haya ya Afrika Mashariki. Lengo letu ni kuwa na *United Republic* ambayo ni ya amani, watu tunapendana, tunashirikiana, kwa hiyo, tusitafsiri kila kitu kama ni matakwa ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliyotaka kuyazungumza nimeyamaliza. Nashukuru sana, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote wa Tanzania walio katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Katibu Mkuu wao - Juma Mwapachu. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe na leo naona nikushukuru kwasababu umetambua uwepo wa Mheshimiwa Waziri ambaye ni kijana mwenzetu, lakini ukasahau kutambua hata Mwenyekiti, anayeongoza Kikao leo, naye ni kijana mwenzako pia. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niwape tangazo moja. Nimeletewa sasa hivi kutoka kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Spika, anaomba mpitie kwenye *pigion holes* zenu kuna kadi maalum zimewekwa huko kwa ajili ya *invitation*. Kwa hiyo, nisingependa kusema zaidi. Ninaomba kila mtu aipitie kadi yake mwenyewe, ataaelewa amealikwa wapi na nani na kwa wakati upi. Kwa hiyo, ni vizuri tukapitia hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kuwasikiliza wachangiaji ambao walijiorodhesha kwa ajili ya hoja hii, ninaona nitoe sasa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wakajipange vizuri, wakatafakari hii michango ya Waheshimiwa Wabunge na hivyo watakapokuja jioni waweze kuwa na maneno ya kujenga mahusiano yetu haya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, baada ya kusema maneno hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ZUBEIR ALI MAULID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nawaomba Wabunge wenzangu, waiunge mkono na kuipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nishauri Wizara hii juu ya suala linalohusu miradi ya miundombinu ambayo iko chini ya Wizara hii hasa barabara ambazo zimelenga kuiunganisha Afrika ya Mashariki. Nashauri isimamiwe vizuri hasa ile inayohusu upande wetu Tanzania kuna baadhi ya wananchi wanaohisi miradi hii ni nadharia zaidi kuliko utekelezaji halisi. Ni vema Wizara hii ikasimamia ili kuifuta dhana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kufahamu juu ya uharakishwaji wa uanzishwaji wa (*Fast Tracking*) Shirikisho, umefikia wapi? Je, kabla hatujaelekea huko, ni utaratibu gani utakaotumika kupata ridhaa ya wananchi juu ya suala hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri sana mnayofanya kuhakikisha ushirikiano wa nchi zetu tano za Afrika Mashariki unaenda vizuri kwa faida ya wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nchi hizi tano zina ushirikiamo mzuri sana kupitia “*East African Local Government Association*” (*EALGA*) Kenya wakiwa na “*Association of Local Authorities of Kenya*” (*ALGAK*), *Uganda Local Government Association (ULGA)*, *Rwandese Association of Local Government Authorities (BALGA)* na tunategemea Burundi kujiunga na Muungano huu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ndicho chombo hasa kinachowawakilisha wananchi wa nchi hizi. Kinatakiwa kiwe na uwakilishi mkubwa ndani ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Waziri, huoni kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa Muungano huu kupata nafasi katika ofisi za Afrika Mashariki na kupewa nafasi ya kushiriki kwenye mambo yote kwa niaba ya wananchi wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana juhudi zinazofanywa kutafuta miradi mbalimbali kwa faida ya wananchi wetu kama vile miradi ya barabara, bandari na kadhalika. Naomba sana jitihada nyingi zifanyike ili kuhakikisha maendeleo yanawafikia wananchi wote.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2008/09 kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala kadhaa ninayoona yanafaa kuangaliwa kwa karibu na Serikali yetu.

Kwanza, ni suala la matumizi ya lugha ya Kiswahili hatika chombo hiki cha pamoa cha *EAC*. Ibara ya 137 ya Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inatamka kuwa:-

“Lugha rasmi ya Jumuiya ni Kiingereza na kwamba Kiswahili kitaendelezwa kuwa lugha ya Jumuiya”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hii, miaka minane tangu Jumuiya ianzishwe, Kiingereza bado ni lugha rasmi ya Jumuiya na hakuna mkakati wa wazi wa kukiendeleza Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hatua ya kwanza ya kuendeleza lugha yoyote ile ni kuitumia, naiomba Serikali ya Tanzania ichukue hatua za makusudi kuzishawishi nchi wanachama kuanza kutumia lugha ya Kiswahili sambamba na Kiingereza kwenye shughuli za Bunge la Afrika ya Mashariki na Sekretarieti. Jumuiya itenye Bajeti kwa ajili ya ukalimani kwa nchi ambazo zitapata matatizo kwa kuanza katika kutumia Kiswahili.

Ni aibu kwa eneo linalotambulika Kimataifa kuwa chimbuko la Kiswahili na ambalo nchi mbili (Kenya na Tanzania) zinatumia au kutambua kuwa Kiswahili ni lunga ya Taifa, kuendelea na Kiingereza kama lugha rasmi pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mwaka jana Bunge letu liliridhia mabadiliko yaliyopendekezwa na Mkataba wa Afrika Mashariki kuhusu Mahakama ya Afrika Mashariki. Uamuzi wetu ambao uliendana na uamuzi wa Bunge la Uganda na Serikali ya Kenya, ulipingwa Mahakamani na Chama cha Wanasheria cha Afrika Mashariki. Ni vema, Mheshimiwa Waziri alielezee Bunge hili hatua ya kesi hiyo na uamuzi tuliochukua kama Bunge.

Aidha, kwa kipindi kirefu tangu Jumuiya ianzishwe, wananchi wa Afrika Mashariki wamekuwa wakidai marekebisho ya Ibara ya 27 ya Mkataba ili kupanua uwezo wa Mahakama ya Afrika Mashariki ili Mahakama hiyo iwe Mahakama ya Rufani ya Afrika ya Mashariki. Huu ni muda muafaka kwa Mheshimiwa Waziri kulielezea Bunge hili maendeleo katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mwaka 2010, bidhaa za Kenya zitaanza kuingia Tanzania bila ushuru (*zero tariffs*). Kwa kuwa Watanzania tunajisahau sana mithili ya watu tusio kwenye hali ya ushindani, Serikali imejiandaa vipi kuboresha na kuongeza bidhaa tunazosalisha nchini ili ziweze kushindana na bidhaa za Kenya na viwanda vyetu visife? Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ina mikakati gani ya pamoja na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuwaandaa Watanzania kuhimili ushindani na wasiishie kuwa soko la Kenya na Uganda?

Aidha, mwezi Septemba 2009, tunategemea kuwa na kura ya maoni kuhusu uanzishwaji wa sarafu moja ya Afrika Mashariki. Wakati tunaona harakati za kuwaanda wananchi kuhusu zoezi hilo zilifanyika Kenya na Uganda, Serikali yetu inafanya nini kuwaelimisha wananchi kuhusu hatua hiyo muhimu?

Kwa kumalizia, *East Africa Single Transit Visa*, ilitakiwa iwe tayari kufikia Novemba, 2006. Ni nini hatua ya uamuzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa nasubiri kwa hamu maelezo kuhusu masuala hayo niliyoyaeleza, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitarajia kuwa baada ya Rwanda na Burundi kujunga kwenye Umoja huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ungeimarika. Kinyume chake, *we are experiencing strange members*. Uchu wa madaraka

unaonyeshwa waziwazi na Marais Yoweri Kaguta Museveni na Mwai Kibaki wa Kenya kiasi cha kuibea demokrasia ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kunauweka mstakabali wa Umoja huu mashakani. Kunahalalisha kabisa mashaka ya Tanzania (wananchi wake) juu ya hoja ya ‘fast tracking’ kuwa na Serikali moja. Marais hao wawili wako tayari kabisha kuweka kando Katiba za nchi zao na hata kuifungia demokrasia kabatini ili waendelee kubakia madarakani maisha yao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa suala la kuwa na Serikali moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki liwekwe kando ili kunusuru amani na utulivu wa Tanzania ambayo ni lulu kwetu. Umoja uendelee kwenye nyanja za uchumi wa mashirikiano mengine.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka kadhaa sasa tangu “*Guidelines for trans boundary EIA for the East Africa countries*” ziandaliwe na jopo la wataalam kutoka Kenya, Uganda na Tanzania (nami nikiwa mmojawapo), lakini hadi leo, nijuavyo mimi *guidelines* hizo hazijawa *adapted* kwa ajili ya matumizi. Kutoruhusiwa kutumika *Guidelines* hizo, kunaendelea kuruhusu matumizi ya rasilimali zilizo mipakani kuendelea kutumika bila utaratibu mzuri. Ni nini kinazuia ku-*adapt guidelines* hizo na ni lini zitakuwa *adapted*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile *EIA Guidelines* zilizozungumziwa hapo juu zilihushisha nchi tatu tu za Afrika ya Mashariki (Kenya, Uganda na Tanzania) na kwa kuwa vile vile nchi nyingine mbili (Burundi na Rwanda) zimejiunga na Jumuiya; ni lini “*EIA guidelines*” hizo zitahuishwa ili kuhusisha nchi hizo mbili?

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujua mambo machache kuhusu Wizara yako hii. Kwa kuwa wewe Waziri ni Mbunge wa Mkoa wa Kagera, ni lini utamaliza au kuingilia kati mgogoro wa mpakani wa Bubale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa katika nchi hii kupenda kumaliza migogoro ya nchi jirani ya kwetu tunashindwa, hivi nini hasa tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ulinzi hasa mipakani ni zoezi la kudumu kabisa kuliko kuweka Kambi za muda. Zinatakiwa gharama kubwa kwenye mipaka yetu mfano Ngara, Kigoma, Mrongo, Benako, Mtukura, sehemu hizo tukiwa na ulinzi wa kudumu itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpaka wa Mtukula sio mzuri hasa kwa wafanyabiashara. Kuna magari makubwa na msongamano mkubwa, inakuwa vurugu sana, naomba vifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uvuvi Mkoani Kagera hasa Ziwa Viktoria, vijana wengi kipato chao kilikuwa ni ziwa hilo, hivi ni kwanini Wizara hii isiweke mkakati wa kuwa na soko au kuleta mwekezaji mwenye kuwa na zana za kutosha? Mwana Kagera hafaidiki na ziwa hilo analiona kwa macho tu lakini sio matuzi yake. Kuanzia biashara au mboga, mambo yote hata kimoja hakuna, je, huo ni uungwana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikutano inayofanyika ya wafanyabiashara pamoja na makongamano yote, kwa nini na Wabunge tusishirikishwe ili kuwaelimisha wananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha bandari, ni lini Bandari ya Kemondo, itaimarishwa na wananchi wafaidike na bandari hiyo muhimu sana kwa Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo, nitaomba nipewe majibu niridhike kwenye moyo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami pia nitoe mchango wangu mfupi katika hoja hii muhimu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri pamoja, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa ujumla, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie suala la soko la samaki, hasa usafirishaji wa samaki kwenda nje. Ni kweli Tanzania tumekuwa na soko kubwa na muhimu kutokana na samaki wetu wakubwa watokao Ziwa Victoria. Tatizo, imefika mahali tumewasahau Watanzania watumiaji wa samaki hawa hasa walioko karibu sana na Ziwa Victoria, kwani samaki wote wazuri na wakubwa wamekuwa wakisafirishwa wote na bei kuwa juu sana, hivyo kusababisha wananchi Watanzania kukosa hitaji muhimu la mboga ya kila siku badala yake wanaambulia mifupa tu. Naomba Wizara ijaribu kuangalia ni jinsi gani itawasaidia wananchi kupata samaki hawa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosoma Waziri katika hotuba yake, ni kweli Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanikiwa kuleta suluhu nchini Kenya na kusababisha Kenya kuwa na amani. Ninachotaka kusema ni kwamba kwa kuwa Rais aliweza kutatua mgogoro wa Kenya ni kwa nini ameshindwa kumaliza tatizo la mpasuko wa Zanzibar? Vile vile ni kwa nini ameshindwa kabisa kuweka msukumo wa ziada kumaliza mazungumzo ya muafaka kati ya CCM na CUF? Naomba waziri atueleze atoe ufanuzi, tatizo hasa ni nini?

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Jumuiya kwa kufanikiwa kuongeza nchi mbili zaidi (Rwanda na Burundi) kama wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni hatua muhimu sana ambayo pamoja na mambo mengine, inaweza kuongeza ukubwa wa soko letu na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni hatua muhimu sana

ambayo pamoja na mambo mengine, imeweza kuongeza ukubwa wa soko letu na Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha, je, kwa kiasi gani utekelezaji wa Itifaki hii umeathiri mapato ya kodi za ushuru kwa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Soko la Pamoja, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, haionyeshi waziwazi, ni lini hasa utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja utaanza baada ya Itifaki hiyo kuridhiwa na Bunge letu ifikapo mwezi Juni, 2009?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bunge la Afrika Mashariki, *Constituencies* za Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, ni Mabunge ya nchi zao. Sina hakika kama Mabunge ya nchi za Afrika Mashariki yanapata taarifa za kutosha ya kazi zinazofanywa na Wabunge wa Afrika Mashariki. Nashauri kuwepo na uhusiano wa karibu baina ya Wabunge wa Afrika ya Mashariki na Mabunge yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera Moja ya Fedha (*Common Monetary Policy*), je, Itifaki hii, inatarajiwa kutekelezwa lini? Mpaka sasa matayarisho yake yamefika wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *EPA* (*Economic Partnership Agreement*), naipongeza Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kufanikiwa kufanya mazungumzo ya *EPA* chini ya mfumo wa Jumuiya yetu. Aidha, ninapenda kufahamu ni tahadhari gani zinazozingatiwa katika majadiliano ya utekelezaji wa Mkataba huu ili kuinusuru Jumuiya yetu isije kuwa ni soko la bidhaa za viwanda vya Ulaya na hivyo kuuwa viwanda vyetu? Vilevile, ni kwa kiasi gani Mkataba huu utaziruhusu bidhaa zetu ambazo kwa kiasi kikubwa ni mazao ya kilimo kujunga katika masoko ya Ulaya bila vikwazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki. Benki hii ni muhimu sana kwa Maendeleo ya Afrika Mashariki. Kwa bahati mbaya (kwa mtazamo wangu), hatujaweza kuitumia Benki hii ipasavyo! Nashauri Jumuiya iangalie uwezekano wa kuitumia benki hii hasa katika kutafuta fedha nyingi zinazohitajika toka Masoko ya Fedha Ulimwenguni (*International Capital Markets*) pamoja na *International Financial Institutions* kama *ADB World Bank* na kadhalika na kuzielekeza fedha hizo katika kugharamia miradi mkubwa ya miundombinu ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nguvu za Benki hii ambayo ina-support ya nchi zote za Jumuiya, hazijatumiwa ipasavyo. Tukiwa na mipango mizuri, tunawenza kuigeuza benki hii ikawa na nafasi nzuri ya kutuletea maendeleo kama ilivyo *European Investment Bank*, tuichangamkie fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dr. Kamala, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed

Aboud (Mb), Katibu Mkuu, Ndugu B. Mahiza na Wakuu wote wa Wizara kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunaelewa kuwa mwaka huu, nchi zetu na dunia kwa pamoja, zitakumbwa na uhaba mkubwa wa chakula. Ni vizuri kwa kutumia utaratibu wa Jumuiya, tukaandaa mkakati endelevu wa kuratibu usafiri na ubadilishanaji bidhaa na mazao ya chakula kwa nchi wanachama ili kuzuia utaratibu wa sasa wa magendo mipakani. Pamoja na taarifa ya majirani zetu kuwa na upungufu wa chakula, lakini mara nyingi majirani zetu huijandaa zaidi katika hali hiyo na kuweka maghala ya vyakula mipakani mwetu na wao ili wapate urahisi wa kubeba chakula chetu kupeleka nchini mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa mradi wa pili wa mradi wa utunzaji mazingira katika Ziwa Victoria ambao ulikuwa unahuusisha pia miji 10 kila nchi kupatiwa maji, chini ya ufadhili wa *UN-HABITAT*, bado naona unasuasua, labda kuna matatizo ya utekelezaji wa baadhi ya masharti. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina kwa nini tangu ukubaliwe miaka zaidi ya minne bado hali ya utekelezaji siyo ya kasi kama tulivyotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya mipango ya Jumuiya yetu, itagemea sana kwa kiasi kikubwa jinsi wanachama wanavyoheshimu na kutekeleza wajibu wao kwa kulipa ada zao na michango mingine. Mheshimiwa Waziri asaidie tujue kuna nini wanachama wengine wameshindwa kutoa hata robo ya michango hii na Kanuni zinasemaje kwa asiyetekeliza makubaliano ya msingi ya kuendesha Jumuiya hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya watumishi waliokuwa wa Afrika Mashariki yanaendelea kuwa kero nchini. Je, Waziri anaweza kuendelea kulifafanua suala hili ili kila mmoja wetu na wananchi watendewe haki na pia kupunguza malalamiko na maandamano ambayo itatuletea simanzi mara tuonapo wazee wakiendelea kukimbilia Ikulu mara kwa mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nadhani anatambua kuwa wananchi wetu wa Tanzania, wanaogopa ushirikiano wa kisiasa, sababu ni wasiwasi wa kukuta wenyeji (wazawa) kuja kunyang'anywa ardhi yao. Kwa nini suala hili lisiwekwe kisheria mapema ili ardhi iendelee kumilikiwa na wananchi na wageni wanaotaka maeneo wawe chini ya migongo ya wanachi wetu wenywewe kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Afrika ya Mashariki zianze sasa kuwekwa katika mfumo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Nalisema hilo ili Waziri atamke wazi kuwa kati ya barabara tano (5) kuu ambazo zilipendekezwa, orodha ya zile ambazo zimeanza ni zippi na zimekabidhwaa kiasi gani cha fedha kwa kila moja, pia kuonyesha barabara nyingine ni zippi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano barabara ya Tunduma – Sumbawanga, je, kwa sasa ni sehemu ya barabara *E.A* ambayo itagharamiwa na *MCC* au ni fedha za wahisani kwa Tanzania na siyo sehemu ya *E.A*? Au ikiwezekana Mheshimiwa Waziri awe anaelezea mipango ya miradi ya *E.A* awamu kwa awamu, ili wananchi wetu waanze kuelewa nini kinagharamiwa na *E.A*. na nini cha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazidi kumpongeza Waziri kwa jinsi anavyojitahidi kila mara kuelezea matukio mbalimbali ya Jumuiya yetu. Azidi kuifanya kazi yake kwa misingi ya kutoa elimu kwa umma bila kuchoka.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba ya Waziri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni ili kurahisisha maendeleo ya watu wa nchi hizo. Tayari kuna *Customs Union* na tunaelekea kwenye *Common Market* na *Common Currency*, cha kushangaza bado ushirikiano wa kibishara kati ya Kenya na Tanzania una vikwazo vingi. Bidhaa kuingia Tanzania ni rahisi sana lakini bidhaa za Tanzania kwenda Kenya, kuna *trade barriers* nyingi sana, magari yanacheleweshwa mpakani na wakati mwagine bidhaa kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bia za Tanzania hazipo Kenya kwa wingi kwa sababu *Tanzania Breweries* wamekula njama na *Kenya Breweries* kuwazuia wafanyabiashara kupeleka Kenya bia za *Tanzania Breweries*. Naomba tabia hii ikemewe kwa nguvu zote. Naipongeza Serengeti Breweries kwa kuingia vizuri kwenye soko la Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Waziri akemee hii tabia ya *Tanzania Breweries* kuunda mkakati wa *Quoter System*, waache ili biashara iwe huru. Kuwe na *fair practice* na *fair competition*. Mheshimiwa Waziri analielewa suala hili, naomba alimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Diodorus Kamala (Mb), Naibu Waziri Mohamed Aboud (Mb), Katibu Mkuu na watendaji wake wote, kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada zote zinazofanywa na Wizara katika kuendeleza mchakato na uimarishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda nitoe changamoto yangu katika suala la utunzaji wa mazingira katika Ziwa Victoria ambayo sasa ipo katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa mazingira katika Ziwa Victoria, ni muhimu sana kwani itasaidia kulinda rasilimali zilizomo, matumizi ya maji na hata utunzaji wa mazingira kwa kudhibiti uchafu iwe taka ngumu au majitaka ambayo yanasmusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la elimu kwa umma lipewe kipaumbele cha haraka sana. Kuwe na ushirikiano wa kutosha hasa kwa kushirikisha Waandishi wa Habari na kupatiwa elimu ya nini lengo la mradi huo na jinsi gani Waandishi hao wanatavyoweza kutumia vyombo ya habari katika kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema katika utoaji wa elimu hii, ukawashirikisha wanasasa wa maeneo husika kwani kwa kutumia majukwaa ya kisiasa ujumbe utawafikia walengwa. Pia si vibaya kama kutakuwa na njia mbalimbali za mawasiliano kama vikundi vya maigizo, ngonjera, kwaya na hata michezo ya kuingiza kuanzia ngazi za shule hadi kwa jamii yote hii, ili kusambaza ujumbe huo. Yote haya ni katika kunusuru uharibifu wa aina mbalimbali wa mazingira ya Ziwa Victoria kwani ziwa hili ni muhimu kwa Tanzania na nchi zinazozunguka ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya mradi wa mazingira ya Ziwa Victoria, napenda niiombe Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, itoe ushirikiano kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi katika kuhuisha Mitaala ya Elimu ili kuweza kuhimili ushindani hasa katika masomo ya Sayansi ambayo shule zetu nyingi bado zina uhaba wa Walimu na vifaa vya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwanzo iliundwa 1967, ilikuwa na wanachama wane na kuvunjika mwaka 1977, Zanzibar ilikuwa mwanachama. Bila shaka Zanzibar ilikuwa ina haki sawa na wanachama wengine taabau fursa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauliza kuitia Wizara hii, Tanzania ingepoteza nini kama Zanzibar nayo ingekuwa mwanachama peke yake? Hii ni taasisi ya kiuchumi, Zanzibar ingeweza pia kufaidika kama wanachama wengine licha ya leo inaonekana Zanzibar hadi isemewe. Zanzibar na Tanzania kwa ujumla wake ingekuwa na nguvu za uamuzi wa Bunge na Afrika kwa kura 18. Nadhani suala ni Katiba iliyotufikisha hapa kwa vile Katiba ni kitu cha kubadilika, ibadilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa 19 wa hotuba ya Waziri, Jumuiya imojiwekea programu mbalimbali, imeshindikana katika programu kuwepo kwa usafiri wa baharini. Hili linavunja moyo Zanzibar na wananchi wanaoishi ukanda wa bahari ya Hindi. Ninaomba Waziri anieleze kwa nini katika programu hizo usafiri wa baharini haumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. MANJU S.O. MSAMBYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uanachama wa Rwanda na Burundi, kama nilivyokwishaeleza katika michango yangu katika bajeti mbili zilizopita (2006/07 na 2007/08), siafiki kwa Rwanda na Burundi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuaweka kama tulivyofanya, tumekaribisha matatizo toka nchi hizo na kuyaleta kwetu. Tunafahamu fika kuwa watu wa Rwanda na Burundi, wamebobea katika mapigano na fujo. Hivi tunawakaribisha ili wahamishie matatizo yao huku kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua fika kuwa kwa wale watokao Magharibi mwa Afrika Mashariki, tumepakana na Rwanda na Burundi, ambapo makabila ya huko yanashabihiana na yale yaliyoko Afrika Mashariki lakini yanatofautiana kwa tabia. Tanzania kwa mfano hatuna tabia ya fujo lakini kwa upande wa Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Rwanda, tumekuwa tunapokea wakimbizi toka Rwanda na Burundi. Wakimbizi hawa ni matokeo ya uvunjifu wa amani katika nchi hizo. Hata hivyo, wakimbizi hao huku wakiwa katika hifadhi ya Watanzania, wamekuwa ni chanzo cha ujambazi na mauaji kama wahifadhiwa, Warundi na Wanyarwanda hawa hawakuogopa kuonyesha tabia yao halisia; inakuwaje wanapokuwa wanachama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Warundi wanaongea lugha inayofanana na kushabihiana na Kiha kinachozungumzwa na Kigoma, Warundi hawa wamekuwa tatizo kwa wakazi wa Kigoma kiuongozi, kiutawala na kisasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa tatizo la wageni kuingilia mfumo wa uongozi wa siasa na utawala, ni vyema sasa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kutoa vitambulisho vitakavyowaweka bayana wageni hawa kuingilia siasa za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuvunja Kanuni za Jumuiya – Uganda. Napenda nimwombe Mheshimiwa Waziri atueleze uhalali upo wapi wa bajeti ya kuendesha Sekretarieti ya Afrika Mashariki wakati bajeti hiyo haikupita kihalali? Nasema haikupita kihalali kwani Wabunge wa Uganda katika Bunge la Afrika Mashariki ambalo lilipitisha bajeti hiyo hawakuwa na uhalali wa kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari ilikuwepo taarifa Wabunge wale wa Uganda walikuwa wamesimamishwa na hawakuwa na uhalali wa kuwa washiriki katika kuitisha bajeti ya Sekretarieti ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, aeleze ni kwa uhalali gani bajeti hiyo itafanya kazi wakati sehemu ya washiriki katika kuitisha bajeti hiyo wakati hawakuwa na uhalali wa kisheria?

Wabunge wa Uganda walismamishwa kule kwao lakini wakaruhusiwa kushiriki kuitisha bajeti ya kuendesha Jumuiya. Naomba hapa tupate maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kuchangia bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Kamala, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed Aboud, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuimarisha Umoja wetu wa Afrika Mashariki pamoja na kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa *African Union* kwa kazi kubwa aliyofanya ya kumaliza mgogoro wa Kenya juu ya matokeo ya uchaguzi wa Rais na hatimaye sasa Kenya ni salama na vyama vya siasa vyote vimeridhika na uamuzi wa Odinga kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya kutembelea Afrika Mashariki, napenda kuishauri Serikali kuwa, kutokana na umaja wetu wa nchi tano za Afrika Mashariki, ni vizuri sasa sheria zikalegezwa kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza nchi za wenzetu ambazo raia wao wana vitambulisho vya nchi zao, naiomba Serikali zoezi la vitambulisho vya uraia, lifanywe haraka ili tuenze kutembelea nchi hizi bila *Passport* bali tutumie vitambulisho. Hii itasaidia Watanzania kutembelea nchi jirani pamoja na kufanya biashara bila matatizo, kwani upatikanaji wa *Passport*, ni mgumu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna tatizo la uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, muda unatofautiana kati ya nchi hizi. Ni vema muda ufanane ili Bunge liwe linaanza mara baada ya uchaguzi kwa nchi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Mungu awape nguvu, busara na afya njema ili waweze kutekeleza malengo yao ipasavyo.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala (Mb), Mheshimiwa Mohamed Aboud (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii, kuwapongeza Wabunge wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa kutoka Tanzania kwa kuwalisha ilivyo sera ya nchi katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie yafuatayo katika hotuba ya Waziri. Kwanza, bado tunahitaji muda zaidi kuhusu kutimiza itifaki ile ya shirikisho kwani

mionganini mwa wanachama (nchi) bado hatujaweka usahihi wa mambo, mfano mzuri bado tabia ya wananchi wetu hazilingani hasa kuhusu amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, elimu mionganini mwa Watanzania iendelee kutolewa ili waelewe nini maana ya Jumuiya na nini faida za Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, suala la ardhi libaki kama sheria ilivyo kwa kila nchi, ili pasiwepo mwingiliano na ardhi ya Watanzania kuja kuporwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ushuru wa forodha, uendane kwa usawa kwa kila nchi, usiwepo usafiri wa kuangalia daraja, haiwezekani baadhi ya bidhaa kutoka nchi mwanachama zitozwe ushuru lakini bidhaa za nchi nyingine wanachama zisitozwe ushuru (huu ni ubaguzi na wala hauonyeshi ushirikiano wa dhati).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, matumizi ya pasi za kusafiria bado utaratibu haueleweki, Mtanzania akienda Kenya lazima apitie Uhamiaji lakini iweje Wakenya wawe na uwezo wa kuingia nchini bila *passport*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, vipi kuhusu Rwanda na Burundi kuhusu uanachama wao katika Jumuiya? Tunafahamu wakuu wa wanzilishi kwenye kikao cha juu kabisa (*Summit*) walishakubaliana na kujiunga kwao sasa mbona ushiriki wao haujaanza hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Wizara iongezee idadi ya wafanyakazi wake wenye taaluma ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoweza kujitekeza kwa *member states*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HAMZA A. MWENEGOHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Diodous B. Kamala (Waziri), halikadhalika Naibu Waziri, Katibu Mkuu na pongezi hizo ziwafikie wataalamu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Wizara hii ni chombo kipyaa katika Tanzania, imeonyesha dhahiri kwamba ina muda kughughulikia masuala kadhaa ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya kuungana nchi hizo za Afrika Mashariki, ni vema maelezo rasmi juu ya Afrika Mashariki yakatolewa, ni nchi zipi hizo? Hii ni kwa sababu ninaona kuna uwezekano wa nchi kadha kuomba kuungana na shirikisho hili halafu zikawa na uhusiano na nchi zingine, hivyo nchi hizo zikawa mguu mmoja ndani na mguu mwingine nje ya shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni suala la miradi ya Afrika ya Mashariki. Miradi hii ni vema ikapimwa na kujadiliwa kwa makini. Pengine ni vema zaidi kama miradi hiyo ingetolewa taarifa katika Mabunge ya nchi zao. Hii itatoa taarifa ya miradi hiyo siyo tu kuwekwa wazi kwa wananchi kwa

ujumla na wadau mbalimbali ambao wataweka mikakati ya kushiriki katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni bandari zetu. Wakati sasa umefika kwa Watanzania kuona kuwa kuna umuhimu wa kutumia bandari zetu katika uchumi wa kijiografia. Nchi zote ambazo zimo katika Jumuiya hii, ni Tanzania na Kenya tu ambazo zinapakana na bahari. Tanzania ndio pekee ambayo inapakana na maziwa makubwa ya maji ambayo tunaweza kuyatumia katika kukuza uchumi wetu. Katika upanuzi na ujenzi wa miundombinu hii, tunaweza kuzishirikisha nchi jirani ili kuwa na uwezo mkubwa wa kifedha kupanua na kujenga bandari za Tanga, Mtwara na Dar es Salaam ili kutuwezesha kuchukua bidhaa za Kongo, Burundi, Rwanda na nchi zingine za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu ni kubwa sana, basi hatuna budi kuigawa nchi hii katika *zone*. Hizi *zone* zote zinaweza kujengewa bandari za nchi kavu. Hizi ndizo ambazo zingeharakisha sana kuingiza na kutoa bidhaa mbalimbali na mizigo mikubwa ya nchi za majirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu ni kuwa na Mahakama Kuu ya Afrika Mashariki. Hii itasaidia kutoa haki kwa nchi zetu na hata nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi za nchi za Afrika Mashariki zisiingizwe katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ardhi zao ziwe za wananchi wao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. BATILDA S. BURIAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, (Mb), Waziri wa Afrika Mashariki na Naibu wake, Mheshimiwa Mohamed Aboud, kwa hotuba nzuri ya bajeti na kwa jinsi walivyoweza kuelezea mafanikio ya Wizara hii kwa kipindi cha mwaka mmoja na mipango ya utekelezaji wa program mbalimbali kwa kipindi cha mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, ninapenda kujielekeza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 23. Nadhani kwa bahati mbaya, maelezo yote yaliyotolewa katika kichwa cha habari, sekta ya maji, kimsingi yanahusu mazingira. Hivyo basi ili kuipa uzito wa sekta hii ya mazingira, ni vizuri ikajionesha wazi na siyo chini ya sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa sekta ya mazingira, ni sekta mtambuka na hivyo basi inajitokeza katika sekta zote. Hata hivyo, mazingiara huwa inasimama yenye we pia kama sekta husika. Hivyo basi, masuala ya utunzaji wa mazingira katika Ziwa Victoria, ni masuala ya mazingira na programu hii ipo chini ya uratibu wa mazingira na siyo sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba siku zijazo tuwe wazi zaidi katika kutambua sekta ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. FELIX N. KIJKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri, napenda kutamka wazi kuwa, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuiunga mkono hoja, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalamu, kwa hotuba yao nzuri ambayo kwa hakika, inatoa mwanga kwa Watanzania kujua shughuli za Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza msukumo wa kuikuza lugha ya Kiswahili kwenye mikutano ya Jumuiya hali ambayo imeijengea sifa nchi kwa kuikuza lugha ya Taifa. Ni katika mtiririko huo sasa hata katika Bunge la Afrika Mashariki lugha ya Kiswahili inatakiwa itumike tofauti na lugha ya Kiingereza inayotumika na kuficha *identity* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuiongezea Wizara hii fedha za utendaji na hasa baada ya kuzingatia kuwa ni Wizara mpya ambayo inatakiwa kutoa mafunzo kwa wananchi ili utendaji wake uweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwango vya kibashara, naona kuwa ni tatizo kubwa ambalo ufumbuzi wake ni kuondoa vikwazo hivyo ili wafanyabiashara wawe huru kufanya biashara bila vikwazo vilivyopo.

MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa hotuta yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ijihusishe pia na ukuaji na malezi ya vijana wa Afrika Mashariki katika maeneo ya elimu, maadili na mila za Waafrika. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kujenga msingi imara wa umoja na maendeleo endelevu kwa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huu, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wataalamu wote, kwa kuandaa bajeti nzuri ya Wizara hii muhimu kwa nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili husema ‘umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu’. Lengo la Wizara hii ni ili hatimaye itufikishe katika umoja halisi wa nchi zetu.

Hivyo Wizara hii, ina wajibu mkubwa wa uundwaji wa shirikisho utakapofika ili tuweze kufaidika kiuchumi. Hivyo lazima mazingira ya kiuchumi na kisiasa yaboreshwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nchi wanachama, moja kati ya hofu za Watanzania, ni kuingia katika shirikisho nchi zenye matatizo yasiyokwisha kama vile Burundi, Rwanda na Uganda. Hoja hii ni kweli lakini kwa kuwa suala la shirikisho ni la muhimu sana basi tuandae masharti ya kwamba wale wote watakaomba uwanachama sharti kubwa liwe ni utulivu wa nchi, demokrasia ya chaguzi na utawala bora. Hivyo itawafanya kama kweli wanataka kujiunga na shirikisho, wataandaa mazingira ya maelewano kwanza kwao. Hili likifanikiwa, itakuwa ni kichocheo cha kuzifanya nchi hizo ziwe na utulivu wa kisiasa. Kwa sababu hiyo, Tanzania itapaswa kutatua tatizo la mpasuko wa kisiasa Zanzibar. Hali hii italifanya eneo hili kutozalisha wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizounda muungano wa Soviet iliyosambaratika, zimeshawishika kujiunga na nchi za Magharibi baada ya kuboresha mazingira ya kisiasa kwao. Lazima tukiri kuwa Rwanda, nchi ambayo wameuawa zaidi ya watu laki moja katika mauaji ya Kimbali, leo wameungana na kutengeneza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Ardhi, Tanzania ina eneo kubwa na zuri kwa ajili ya kilimo ambapo sehemu kubwa haijali limwa tofauti na nchi kama Kenya ambayo ina kinyang'anyiro cha ardhi. Kama tunataka shirikisho la kweli lazima Sera na Sheria ya Ardhi ibadilishwe ili iwe ni ya Mtanzania tu mwenye fursa na haki ya kumiliki ardhi. Wageni wote watakaotaka kuwekeza lazima wafanye ubia na Watanzania wenyewe ardhi. Rasilimali ya mgeni iwe ni fedha na kwa Mtanzania iwe ni ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivi sasa tunawakaribisha wageni nje ya Afrika Mashariki kuwekeza, kwa nini basi tuogope kuwakaribisha majirani zetu Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi? Wakuliwa wa Zimbabwe waliposambaratishwa, wengi wao walikwenda Msumbiji, Nigeria, Zambia ambapo wanazalisha kwa wingi na kukuza uchumi wa nchi hizo. Wakulima hao hawakuona umuhimu wa kuja kuwekeza Tanzania, labda kutokana na Sheria ya Ardhi katika uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho, naipongeza Serikali kwa kuanza na utaratibu wa kuanzisha vitambulisho vya uraia. Ni mfano mzuri kwa nchi nyingine kama Kenya na Uganda. Hii ni hatua nzuri ya kila nchi kutambua watu wake kwanza. Shirikisho la Afrika Mashariki, halina mipaka ndani/kati ya nchi hizo, lakini lazima litakuwa na mipaka nje ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wastaa fu, suala la wastaa fu limekuwa "Donda Ndugu". Ni mwaka mmoja sasa wastaa fu hao wanadai haki zao. Wenzao wa Kenya na Uganda wameshapewa haki zao miaka mingi, Tanzania inaonekana nchi ya ajabu. Tunaomba suala hili limalizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi, miradi ya Afrika Mashariki ielekezwe Pemba ambako Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imeitelekeza. Barabara zote ni mbovu. Tunaomba pia mradi wa Mkumbuu sasa ni wakati muafaka kuuanzisha.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kuupongeza uongozi wote wa Wizara hii, nikianzia na mchapa kazi na kiongozi mahiri Mheshimiwa Waziri Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed Aboud, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalamu na watendaji wao wote, kwa kuwasilisha bajeti yao mbele ya Bunge lako Tukufu kwa umahiri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni nchi yenye mfano mzuri ndani ya Jumuiya yetu hii ambayo kila siku inakua kutokana na umahiri wa kiongozi wetu wa juu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, anayesifika kwa umahiri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangazwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanalinganisha uchaguzi wa Kenya na Zimbabwe kwamba ni sawa na uchaguzi wa Zanzibar kwa mifano ambayo iko tofauti kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi wa Zanzibar, Chama Tawala kilishinda kwa viti 31 na Upinzani viti 19. Wasimamizi wa Kimataifa, pia wamekiri kuwa uchaguzi wa Zanzibar ulikuwa huru na wa haki, leo tamko la kusema uchaguzi wa Zanzibar haukuwa wa haki linatokea wapi au kwa kuwa Upinzani haukushinda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono tamko la AU la kutoutambua ushindi wa Rais wa Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Meshimiwa Rais, kwa uteuzi wa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ambao kwa pamoja wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauweka katika lugha ya maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, swalii la kwanza, kwa kuwa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, wana vivutio ambavyo baadhi ya nchi inapakanina/inashirikiana, mathalani Mlima Kilimanjaro na Maziwa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, je, Wizara ya Afrika ya Mashariki, ina mkakati gani wa pamoja wa kuweka vivutio na vipeperushi ili kutangaza rasilimali hizo tulizobarikiwa na Mungu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile baadhi ya nchi, mathalani Kenya, inajitangaza kuwa Mlima Kilimanjaro uko Kenya, nasi mara nyingi, tunaishia kunung'unika, ni vyema basi Wizara yetu ifanye utafiti na kusimamia jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, *Port* ya Holili. Siku hizi Holili pamekuwa mahali maarufu sana pa kuingizia mizigo kutoka Bandari ya Mombasa. Ukiuliza kulikoni? Jibu linakuwa ni wepesi na uharaka wa kuondoa mizigo bandarini Mombasa. Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuboresha huduma zetu katika kituo cha Holili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu, ukurasa wa nne, aya ya tatu inayozungumzia gharama za kituo cha Holili.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika kipindi cha jioni na tunaendelea na ratiba yetu ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na sasa kwa sababu wachangiaji wote walikwisha changia, tunaanza moja kwa moja na watoa hoja.

Mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Naibu Waziri, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri na baada ya hapo tutaingia kwenye hatua itakayofuata.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia kukutana hapa leo na kutuwezesha kusoma hotuba yetu ya bajeti kwa Wizara yetu hii. Aidha, natumia nafasi hii kwanza, kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kunitfea kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nataka nimhakikishie yeye na Watanzania wote kwamba, nitafanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa na kutumia uwezo wangu wote, kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, ili nitekeleze majukumu yangu ipasavyo. Aidha, nawapongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutekeleza majukumu yao ya kuliongoza Taifa letu. (*Makofi*)

Natoe shukrani maalum kwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, kwa ushirikiano mkubwa anaonionyesha kwangu, pamoja na ushauri wake na maelekezo ambayo yananisaidia sana katika utendaji wangu wa kazi. Nawashukuru pia Watendaji wetu, wakiwemo Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Wafanyakazi, kwa ushirikiano wao mkubwa kwangu. (*Makofi*)

Nachukua fursa hii, kuishukuru sana Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, kwa ushauri nasaha na ushirikiano mkubwa, wanaotupa siku zote katika kutekeleza majukumu yetu. Vilevile nampongeza sana ndugu yangu, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, kwa usomaji wa taarifa ya Kamati asubuhi ya leo. (*Makofi*)

Aidha, nampongeza sana Waziri Kivuli na Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani, kwa upande wa Wizara hii, kwa maoni. Maoni yake yamekuwa mazuri na yametupa nguvu sana. Pia namshukuru Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni, kwa jinsi alivyoanza vizuri na kuunga mkono hoja hii. Nawaomba na wengine wote, watunge mkono ili tuipitishe hoja hii vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote katika Bunge hili Tukufu, kwa namna ambavyo wanashirikiana nasi na wanavyotusaidia ili tuweze kutekeleza vizuri wajibu wetu. Naamini ushauri wao kwetu ni dira ya utendaji kazi wetu. Aidha, shukrani maalum ziwaendee Waheshimiwa Wabunge, waliochangia katika Wizara hii kwa kuzungumza na pia kwa maandishi; wametupa moyo sana na ushauri wao umetupa nguvu mpya ya kufanya kazi zetu. (*Makofii*)

Nimalizie kwa kuishukuru sana familia yangu na hasa mke wangu Afife na watoto wote, kwa uvumilivu wao kwangu, maana muda mwangi nakuwa sipo nao, mazoea ambayo huko nyuma hatukuwa nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa kuwa Waziri wangu ataeleza kwa kina na atajibu hoja mbalimbali ambazo zililetwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nielezee upande wa miradi inayotuhusu Tanzania na hasa ile ya upande wa Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Miradi ya Afrika Mashariki, ambayo inatekelezwa na Afrika Mashariki kama ilivyoeleza hotuba yetu ya bajeti asubuhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge mbalimbali waliochangia hoja hii kwenye suala la Miradi akiwemo Msemaji Mkoo wa Upinzani, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, walizungumzia sana suala la bandari hasa za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Sisi kwa upande wetu, tunakubaliana sana na ushauri huo na kwa kuwa ni jana tu hapa tulimalizia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Miundombinu na alielezea kwa kina, namna watakavyoimarisha bandari hizi, kwa hiyo, sisi tunaunga mkono jitihada zile ambazo zinachukuliwa kisekta.

Tunaamini pia maeleo yenu mliyoyaeleza ili kuziimarisha bandari hizi. Tunahitaji sana kuziimarisha barabara zetu, reli zetu na miundombinu ya umeme. Nakubaliana sana na hoja hizo ambazo zinatupa moyo sana kwa upande wetu.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, upo Mpango wa Barabara unaojulikana kama *East African Road Network Project*, ambapo katika matarajio ya kujenga barabara 12628 kwa upande wa Tanzania; tunategemea kuwa na kilomita 6800 kwenye *corridors* tano ambazo ni Dar es Salaam, Dodoma, Isaka, Biharamulo, Mwanza, Musoma Sirari, Tunduma, Iringa, Dodoma, Arusha, Namanga, Nyanakazi, Kasulu, Tunduma, Horohoro, Tanga, Saadani, Bagamoyo na nyaginezo. Nataka niwahakikishie kwamba, tunajitahidi sana kusimamia maslahi ya Tanzania katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki.

Vilevile kwa upande wa reli, upo mpango mkubwa wa kuendeleza reli, yaani *Railway Development Master Plan* ya Afrika Mashariki. Nia yake kubwa ni kuziendeleza bandari hizi ili ziweze kutekeleza wajibu wake vizuri wa kulisaidia Taifa letu.

Hali kadhalika, mpango wa kuimarisha huduma za umeme ambazo zimo katika Mpango wa Afrika Mashariki, zitekelezwe kwa kina na Waziri anayeshughulikia Sekta hiyo, Mheshimiwa William Ngeleja, pale atakapokuja kuwasilisha hotuba yake ya bajeti.

Mimi leo najikita zaidi katika miradi ya upande wa Zanzibar. Miradi hii ilizungumziwa sana na Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Kwa upande wa Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, yeye alizungumzia suala la kucheleva kwa Miradi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba, katika kuandika Miradi hii kuna vigezo vyake. Kwanza, lazima uwe na *study* iliyokamilika na lazima utimize vile vigezo vya Afrika Mashariki. Kwa msingi huu, kabla ya kuwasilishwa kuna kazi kubwa ya kufanya hizi *study*. Kwa hiyo, kusema kweli hatuwezi kuwalaumu SMZ kwamba, wamechelewesha hii Miradi, lakini kutokana na *process* nzima mpaka ufikie pale ambapo unatakiwa Mradi ukamilike na uweze kuwasilishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, ninapenda kuchukua fursa hii, kuipongeza sana SMZ kwa hatua ambayo kwa sasa imefikia. Ninaamini miradi mingine huko mbele itakuja. Kwa hiyo, kwa kuwa wapo katika *process* ya kufanya hivyo, nakuomba tu tuungane katika jambo hilo.

Hata hii Miradi ya upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi sasa imo kwenye hatua za awali, yaani hatua za *study* na hatua nyingine. Hivi karibuni tu, Viongozi wetu Wakuu walikuwepo kule Kigali kuitisha kuharakisha huu Mpango wa Maendeleo katika Nchi za Afrika Mashariki, tupo katika jitihada hizo. Kwa hiyo, bado hawajachelewa na wamekuja kwa wakati, tutajitahidi kushirikiana na wenzetu wa Zanzibar ili Miradi yao iwe katika upandeleo maalum.

Cha msingi ningependa niwakumbushe ndugu zangu wa Zanzibar kwamba, jambo muhimu hapa ni kuendelea kuimarisha Muungano wetu na kuimarisha umoja wetu. Nchi nyingine hizi kama Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya, wana hamu kubwa ya kutumia fursa ambazo zipo Tanzania. Kwa upande wa Zanzibar, fursa hizi sisi kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano, tunaweza kuzitumia vizuri sana. Kwa hiyo, ni jambo la msingi sana kuziona zile fursa zilizopo na tukazitumia chini ya Kivuli cha Jamhuri ya Muungano na wakati huo huo kwa zile fursa ambazo zitatumika kwa upande wa Zanzibar pekee, tutaendelea kuzitumia kwa upande wa Zanzibar pekee. Jambo la muhimu sana kuendelea na suala la Muungano ili litusaidie katika kuimarisha maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Miradi mingi sasa ilitoka upande wa Kisiwa cha Unguja, lakini haikuwa na maana kwamba, ni kwa sababu ya kusahau Miradi iliyotoka upande wa pili wa Pemba. Miradi ya upande wa Pemba pia tunayo ilioletwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama ule Mradi wa *Karume Airport* wa Pemba.

Miradi hii ambayo sasa hivi imetangulia kama Mradi wa Maruhubi pale Zanzibar, Mradi wa *Zanzibar Airport*, Mradi wa *Wind Power Plant* na Miradi ya Kilimo ni kweli inafanyika katika Kisiwa cha Unguja. Msingi wake mkubwa, wametazama *priority* kwamba, miradi hii sasa hivi ikifanyika, itazidisha kujenga mahusiano na kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, jitihada zinachukuliwa katika kuimarisha Miradi kwa upande wa Pemba. Hivi sasa kuna Miradi ya *MCC*, ambayo itajenga barabara za Pemba. Vilevile kuna miradi ya *ADB* itajenga barabara za Pemba na miradi mbalimbali. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inachukua hatua kufanya hivyo.

Kwa hiyo, ile Miradi mingine ambayo itakuja kwa upande wa Afrika Mashariki kupitia Pemba, nina hakika SMZ wataendelea kufanya hivyo ili kuleta uwiano ulio mzuri katika nchi nzima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kila mmoja aweze kufaidika na Miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Bandari ya Mkumbuu Pemba, nakubaliana kabisa na ushauri uliotolewa na Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Afrika Mashariki kwamba, upo umuhimu wa kuwa na bandari katika maeneo mazima ya Mwambao wa Afrika Mashariki. Kwa kuwa Mradi huu unahusiana na Miradi ya Zanzibar, sisi tukachokifanya upande wetu, wajibu wetu ni kuchukua maelezo haya na kuwasiliana na wenzetu kwa upande wa Tanzania Zanzibar, kwa maana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kueleza haya maelezo ambayo yamewasilishwa ili kwa upande wa Zanzibar waweze kuuangalia Mradi huu kwa wakati huu, utasidia vipi uchumi wa Zanzibar na utasidia vipi harakati za kuleta maendeleo Kisiwani Pemba na Zanzibar kwa ujumla. Kwa hiyo, jitihada yetu kubwa ambayo sisi tutaifanya ni kuhakikisha kwamba, haya maelezo ambayo yamewasilishwa kwetu, tutawasiliana na wenzetu ili kulieleza jambo hili.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, jambo hili si tatizo kwa sababu kwetu sisi Miradi ya Bandari tunaipa kipaumbele. Kwa hiyo, kwa upande wa Afrika Mashariki, kuhusiana na Miradi ya Bandari kwetu ni jambo moja ambalo tunalipa umuhimu sana. Lakini pia na wao wenzetu wa Zanzibar, itabidi watazame katika mipango yao ya kiuchumi, taratibu zao zilivyowekwa baada ya pale ndiyo Miradi kama hii itawasilishwa upande wetu tuweze kuisogezza mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Miradi hii ya usafiri wa meli katika Mwambao wa Pwani, jambo hili lilizunguzwa sana na Mheshimiwa Mnyaa. Kwanza, Serikali zetu mbili zinahimiza sana suala zima la uwekezaji katika Sekta hii ya Maji ya Bahari na hatua mbalimbali zimejitokeza katika Sekta hii. Hivi sasa utaona meli mbalimbali zinaanza kuchukua abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam, Zanzibar na Pemba na zipo baadhi yake vilevile zinafanya usafiri kati ya Pemba na Tanga. Sasa jambo hili tuendelee tu kushirikiana kuwatafuta wawekezaji ambao watakuwa tayari kufanya *operations* hizi baina ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba na Mombasa, kwa sababu ni jambo ambalo tayari lipo katika Sera za Serikali zetu zote mbili na lipo katika *priority* ya nchi yetu kwamba, eneo la usafiri wa majini lipewe umuhimu wa aina yake.

Kwa hiyo, kwa msingi huo, katika eneo hilo upo umuhimu wa sote kushirikiana katika kutafuta wawekezaji ili wajitokeze kuwekeza katika maeneo hayo.

Kwa upande wa Afrika Mashariki, hivi sasa tunafanya utafiti wa kina kuhusu suala hili la kuimarisha bandari zetu na kuimarisha usafiri wa majini. Utafiti huo unafanywa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na *Tanzania Ports Authority*. Ninaamini mara tu tathmini hii itakapomalizika, basi itatuelekeza vizuri, hatua gani tuchukue ili kuendelea kuuimarisha Ukanda huu wa Pwani. Nia yetu ni kuimarisha maisha ya Watanzania wote na kuleta uwiano katika nchi yetu ili Watanzania wote waishi katika maisha yaliyo bora zaidi. Kwa hiyo, nia yetu kubwa vilevile ni kuongeza pato la Watanzania na Wananchi wanaoishi katika Ukanda huo wa Pwani na kuhakikisha usalama wao wanaposafiri katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, msingi wetu mkubwa baada ya tathmini hii, tutajitahidi kuhakikisha kwamba, hatua mbalimbali zinachukuliwa kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda wangu, itabidi nifanye haraka kidogo kwa sababu muda unaonekana unanivutavuta sana.

Kuhusu suala la wastaifu wa Afrika Mashariki, ambalo limechangiwa sana na Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. Serikali imechukua hatua nyingi sana kwenye suala hili na hivi karibuni tu yalitolewa maelezo ya kina na Wizara ya Fedha na Uchumi. Jitihada ambazo zimechukuliwa na Wizara ya Fedha na Uchumi, tunaziunga mkono ziendelee ili kulimaliza tatizo hili na wananchi wetu wasiendelee kusumbuka. Naamini dhamira nzuri sana iliyopo ya Serikali yetu kuhakikisha, ifanye uhakiki wenyewe uhakika na wale ambao wana haki ya kupata haki zao waendelee kupata haki zao na kila jitihada itachukuliwa kuhakikisha kwamba, wastaifu hawa hawapati matatizo zaidi ya haya ambayo wamekwisha yapata. Mheshimiwa Waziri, alilielezea vizuri jambo hili kwa hiyo tunaunga mkono jitihada hizo na ziendelee.

Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, alielezea suala la utunzaji wa mazingira katika Ziwa Victoria. Zipo hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa kuhusu kuliendezea Ziwa Victoria, ikiwemo Mradi wa Utunzaji wa Mazingira katika Ziwa Victoria. Upo pia Mradi wa Kuendeleza Makazi ya Wananchi wanaozunguka eneo la Ziwa Victoria. Mradi huu ambao utagharimu shilingi milioni 65, nia yake itakuwa ni kuendeleza wale wananchi wanaoishi katika Mwambao wa Ziwa Victoria ili wasisumbue mazingira na vilevile waweze kujijendezea vizuri, kwa kujipatia kipato zaidi na kuendesha maisha yao vizuri zaidi.

Kwa upande wa Mheshimiwa Paul Kimiti, alizungumzia sana kuhusu magendo ya mipakani. Napenda nimhakikishie kwamba, Sheria za Nchi zipo kuhusu magendo ya mipakani hasa kwa chakula. Kwa kuwa alifikiria kuwa sasa hivi kutakuwepo na upungufu mkubwa wa chakula hapa nchini kwetu na inawezekana mwanya huu ukatumika kwa nchi jirani kununua chakula kwa wingi kutoka Tanzania, Sheria zipo zitakazotumika kuhakikisha kwamba, hali hiyo haitoeki. Kwetu sisi naona jambo hili ni

changamoto, kwa sababu ni *comparative advantage*, kama tutafanya bidii ya kulima zaidi na kuweza kuwauzia Wananchi wa Afrika Mashariki na Ulimwengu, itakuwa ni jambo la muhimu sana. Kwa hiyo, hapa ningependa kuunga mkono jitihada za Wizara ya Kilimo, zinazochukuliwa katika kuhakikisha kwamba, tunajitosheleza kwa chakula na vilevile tupate ziada ya chakula na kuuza nje. Nafikiri tuendelee kuungana mkono na wenzetu wa Wizara ya Kilimo ili jitihada zaidi za kuhakikisha kwamba, uzalishaji unakuwa mkubwa na tuweze kuuza nje zifanyiie, tusaidie katika kuongeza pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Ali Khamis Seif, alizungumzia kwamba Tanzania ingepoteza nini kama Zanzibar ingeingia katika Jumuia ya Afrika Mashariki? Mheshimiwa Ali Khamis Seif ni kwamba, tunaingia kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu wa kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki ni utaratibu wa nchi, ndio unaokuwa na haki ya kujiunga kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jana mlimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa akijibu swalí alieleza kwamba, Tanzania ni nchi moja kwa maana hiyo Zanzibar imeingia mle kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, utaratibu huu kama nilivyosema mwanzo, yapo maslahi makubwa ambayo Tanzania Zanzibar itayapata chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile kwa upande wa Zanzibar, kwa yale mambo yasiyo ya Muungano, inayo haki yake na inayapata vizuri sana, kwa sababu ushiriki wao unakuwa unakaribishwa vya kutosha ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunashirikiana vizuri kuanzia ngazi ya Wataalamu, Makatibu Wakuu na Mawaziri. Ushiriki wao ni wa kuigwa mfano na mimi napenda niwapongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kazi hiyo ambayo wanaifanya kuuimarisha umoja wetu huu.

Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, alizungumzia suala la malezi kwa vijana wetu; waige maadili ya Kiafrika na iwe ni sehemu ya Afrika Mashariki katika suala hilo. Hili ni shauri zuri, tutalichukua kwenda kulifanyia kazi ili vijana wetu wote wawe na maadili ya Kiafrika. Ninaamini Mheshimiwa Waziri, atakuja kuelezea vizuri zaidi, wakati atakapokuwa akielezea suala la Lugha ya Kiswahili itakavyoanza kutumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivi sasa hatua mbalimbali zimeshaanza kuchukuliwa ili kufundisha Lugha ya Kiswahili katika nchi wanachama. Mheshimiwa Waziri, atakuja kulieleza kwa kina suala hili na ataliezea pia kwa upana namna tunavyothamini mila na tamaduni za Kiafrika katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kupigiwa kengele ya pili, naomba tena nichukue nafasi hii, niunge mkono hoja hii. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na kuwataka wote kwa pamoja, tuijishe hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa usalama na utulivu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mchango wako katika hoja hii.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Waziri mtoha hoja na yeze aweze kutoa maelezo kulingana na hoja zilizoletwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, karibu tafadhali. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naanza kuwaomba, kwa hoja zile ambazo sitaweza kuzitolea ufanuzi hapa, itakuwa ni kwa sababu ya muda, basi kwa wakati muafaka tutaandaa majibu kwa maandishi na kuhakikisha Waheshimiwa Wabunge wanayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwatambua wale waliochangia kwa kuzungumza. Nianze na aliyuwalishwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Kabwe Zitto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumepata wachangiaji wengine 22; mbali na wale saba waliochangia kwa kuzungumza, naomba kwa ridhaa yako niwatambue waliochangia kwa maandishi: Nao ni Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Zainabu M. Vulu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Emmanuel J. Nchimbi, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud na Mheshimiwa Shally J. Raymond. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, nawashukuru wote kwa michango yao. Michango hii itatusaidia sana katika utendaji wetu wa kazi wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupitia hoja za Kamati ya Bunge si kwa nia ya kuzijibu ni kwa nia ya kutambua kwamba, wamesema, tumesikia na tutazifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ya Bunge imetoa ushauri mzuri kwamba tunapoelekea kwenye soko la pamoja, itakuwa jambo la busara kuhakikisha kwamba, ardhi ya Tanzania tunailinda ili iweze kutumika kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imezungumzwa kwa njia tofauti, lakini ikimaanisha jambo lile lile. Msemaji wa Kambi ya Upinzani naye ameelezea umuhimu wa ardhi na hasa pale alipoeleza kwamba, Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda,

ukiangalia kwa haraka haraka wenzetu wana matatizo ya ardhi ukiwalinganisha na sisi, lakini vilevile wapo na wasemaji wengine waliozungumzia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu mbalimbali kuhusu ardhi, utagundua yafuatayo: Ukiangalia kiasi cha ardhi, *percentage* ya ardhi kwa kila nchi kwa ardhi yote ya Afrika Mashariki, utakuta kwamba Tanzania tuna 50.2%, Kenya wana 33%, Uganda wana 13.7%, Rwanda wana 1.5% na Burundi wana 1.6%. Ukiangalia ardhi kwa ardhi kwamba, nani ana nini kwenye ardhi hiyo, bila kujali ardhi inatumika kufanya nini, ukiangalia kwa ardhi ambayo inaweza kutumika kwa shughuli za kiuchumi, maana unaweza kuwa na ardhi lakini isitumike kwa shughuli za kiuchumi.

Ukiangalia shughuli za kiuchumi, utagundua kwamba, Tanzania tuna 60%, Kenya wana 35.5%, Uganda wana 3.3%, Rwanda wana 1.56%, Burundi asilimia zinaonyesha 00 ingawa nadhani hii ni kwa sababu ya mahesabu, watakuwa na asilimia kidogo.

Ukiangalia kwa upande wa ardhi kukaliwa na misitu ndani ya Afrika Mashariki nani ana nini, Tanzania tuna 60%, Kenya 30.27%, Uganda wana 9.9%, Rwanda 00 na Burundi 0.1%.

Kwa maneno mengine, unapokuwa unazungumza katika soko la pamoja kwamba, sasa watu wataweza kutoka sehemu moja kwenda nyingine, utakuwa unazungumzia kwamba, watatoka sehemu moja waende Tanzania, ukiangalia hizi takwimu. Ukiwa unazungumza kwamba, kuwawezesha Wana-Afrika Mashariki kwenda popote pale kuchukua ardhi na kujishughulisha na shughuli za uchumi, kwa maneno mengine unazungumzia kwamba, utaruhusu watu watumie ardhi kule ambako inaonekana nyingi. Hapa nazungumza kulingana na takwimu zinavyoonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukasema kwamba, tunapojiandaa kwenda kwenye soko la pamoja, lazima tuangalie tunafanyaje kuhusu masuala ya ardhi, kwa sababu wenzetu Kenya wana Sheria tofauti kuhusu masuala ya ardhi, Uganda Sheria zao tofauti na sisi kuhusu masuala ya ardhi, Burundi na Rwanda wana Sheria tofautia na sisi. Kwa hiyo, ni lazima tukae kwenye meza ya mazungumzo, tuzungumze na tukubaliane lile ambalo Mtanzania anaweza kulipata Kenya vilevile alipate Uganda, Burundi na alipate Rwanda, vivyo hivyo na ambalo wao wanatarajia kulipata kwetu. Watanzania lazima wawekewe mazingira ya kuwezesha kupata hicho hicho wakienda kule.

Kwa hiyo, ndugu zangu naomba niseme kwamba, ile Kamati ya Wangwe iliyokusanya maoni, ilieleza mambo mengi ya jinsi gani tuelekee kwenye Shirikisho. Kamati ile ilieza, yaani Watanzania walieleza kwamba, wana wasiwasi na masuala haya, suala mojawapo lilikuwa ni ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile katika mwaka wa fedha tunaoumaliza, Wizara yangu ilimuweka mtafiti aliybobea katika masuala haya, akatufanyia utafiti wa kina na tukapata na bado taarifa zimeonyesha kwamba, Watanzania wana wasiwasi kuhusu masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, Serikali ni sikuvi, tunajua Watanzania wanataka nini na katika mazungumzo ya kuelekeea katika soko la pamoja, tutahakikisha maslahi ya Tanzania yanalindwa likiwemo suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, Kamati vilevile imetueleza kwamba ni jambo zuri kuipanua Bandari ya Tanga. Nashukuru sana, jana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ameeleza mpango wa Serikali uliopo wa kujenga Bandari yenye kina kirefu pale Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Mpango wa Reli wa Afrika Mashariki, reli ya kutoka Tanga kwenda Arusha hadi Musoma ni sehemu ya mpango wa reli ya Afrika Mashariki. Jambo moja ambalo napenda niliseme hapa ni kwamba, utafiti umeonyesha unaposafirisha mizigo, kwa mfano, tuchukue Uganda; ikitaka kuamua kusafirisha mizigo yake kutoka Mombasa au kutoka Dar es Salaam, ikitoka Mombasa itakwenda na reli, ikifika Malaba kwenda mpaka Kampala inapanda mlima. Sasa gharama za reli kupanda mlima ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mazingira yale yanababisha, hata kama wangekuwa wanapenda kutumia Mombasa, kama tukiwapa njia mbadala ni rahisi zaidi wao kubadilika kwa sababu watapata unafuu zaidi. Hesabu zinaonyesha, ukisafirisha mizigo yako kutoka Dar es Salaam ukafika Mwanza ukaweka kwenye meli, ukasafirisha mpaka Kampala au Jinja, gharama ya kusafirisha mizigo hiyo itakuwa nafuu. Kwa maneno mengine, Mwenyezi Mungu ametupa baraka kwamba, kwa mazingira yetu ni rahisi kusafirisha mizigo kupitia Tanzania kuliko kupitia sehemu nyingine. Tunachotakiwa ni kuipanga vizuri ili kutumia mazingira haya ambayo yanatupa sisi *advantage kijiografia*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati imeshauri kwamba ni vizuri kila nchi mwanachama kuchanga. Hili ni jambo zuri, nasi tumekuwa tukilisisitiza hili na kwa kweli nchi wanachama zinajitahidi kuchanga. Kama tulivyooleza, wenzetu Rwanda wameshachangia asilimia ishirini na tano na wameahidi kwamba, watakamilisha michango yao. Kama nilivyozungumza hivi karibuni na Waandishi wa Habari kwamba, Nchi ya Burundi iliwasilisha maombi yake kwa Wakuu wa Nchi katika mkutano uliomalizika hivi karibuni na ikaeleza kwamba, hivi sasa imetoka kwenye vita, hali yao ya uchumi si nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Rais wa Burundi akaomba kwa niaba ya nchi ya Burundi kuwa, Marais wa Afrika Mashariki, waangalie jinsi ya kuisaidia Burundi wakati inajipanga vizuri, maana imetoka kwenye vita. Wakati inajipanga vizuri, iweze kuendelea kushiriki vizuri katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Viongozi wetu Wakuu, kwa busara wakaona ni vizuri Burundi badala ya kuchangia Sh. 4.5m kwa 2007/2008 ichangie Sh. 1m na kwa mwaka wa fedha unaofuata ichangie Sh. 1m, baada ya hapo iwe imeshajipanga kuchangia kama nchi nyingine zinavyochangia. Wakuu wa Nchi wakakubaliana, lakini kwa nia nzuri tu kwamba, unatambua mwenzako alikuwa kwenye vita. Nia ya Wakuu wa Nchi ni kutaka na Burundi isimame vizuri na iendelee vizuri.

Kwa hiyo, wakaikubali lakini kwa sharti kwamba, wahakikishe kwamba wanajiandaa vizuri ili siku zijazo waweze kuchanga kama nchi nyingine zinavyochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo naona ni vizuri niliseme hapa; Wakuu wa Nchi vilevile wameagiza kwamba, wakati umefika wa kuangalia ni jinsi gani sasa nchi wanachama, zichangie Jumuiya ya Afrika Mashariki, maana utaratibu wa sasa bajeti ikishaandaliwa inagawanywa sawa nchi kwa nchi. Ukiangalia Jumuiya nyingine za ushirikiano kama wetu, kwa mfano, *African Union*, nchi huchangia kulingana na uchumi wa nchi, lakini vilevile ukiangalia *European Union* pia huchangia shughuli zile kulingana na uchumi wa nchi, kadiri unavyokuwa na uchumi mkubwa, ndivyo unavyochangia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Nchi wamesema, suala hili lifanyiwe utafiti ili tuone kama tuendelee na utaratibu wa sasa au tuubadilishe. Haya yote yatategemea utafiti utasemaje, lakini vilevile itategemea na ushauri ambaa nanyi mtatupa na ambaa tutaupata kutoka katika masuala mengine, baadaye tutaamua jinsi gani tuendelee kuchangia Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam nimelizungumzia lakini vilevile tulielezwa kwamba ni vizuri Bandari ya Tanga iimarishwe, nimelizungumzia pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ametoa hoja nzuri; napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake. Hotuba yake ni nzuri, katika dunia hii, huwa tunakubaliana kwamba, kila jambo lazima ukubali kwamba, huwezi kuwa na mtazamo unaofanana kwa kila jambo kwa kila mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na dunia ambayo ina watu wanalitazama jambo kwa mtazamo ule ule, basi ujue hiyo dunia haiwezi kuwa na maendeleo. Kwa hiyo, nachukua mchango wa Upinzani, kwa jinsi walivyotazama mambo, pale ambapo walitazama tofauti na sisi ni njia mojawapo ya sisi kujiuliza kwa nini wenzetu wanatazama tofauti na sisi na kupunguza ule utofauti wa jinsi tunavyoliona jambo ili tuweze kwenda mbele zaidi. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa mtazamo wao na niseme ushauri wao tutauzingatia na tutaboresha zaidi na zaidi ili kadiri siku zinavyokwenda, watu waone kwamba, hoja zinazotolewa zinafanyiwa kazi na kwa sababu hiyo kama hawa waliopo wanaweza kuzifanyia kazi, basi ni vizuri nadhani nisiendelee kuongea zaidi ya hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alitoa hoja ya kwamba ni vizuri wachange, nakubaliana naye mia kwa mia kwamba ni vizuri wakachanga. Mkataba wetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unasema usipochanga unaweza kufukuzwa hata uanachama. Kwa hiyo, usipochanga na usipoeleza kwa nini unashindwa kuchanga, unaweza kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna hii hoja ya wafanyakazi waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wamelieleza vizuri lakini niseme Wizara ya Fedha, ilishaanza kulishughulikia suala hili na sisi kama sehemu ya Serikali, tutaendelea kuwakumbusha wenzetu ili wafanye kila linalowezekana, kuweza kumaliza tatizo hili. Kama walivyoleza Waziri wa Fedha na Naibu wake, lengo ni kuhakikisha tatizo hili linakwisha ili wenzetu waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alitoa hoja nzuri ya kwamba, Shirikisho ni vizuri liende taratibu. Napenda niseme kwamba, tulipokusanya maoni nchi nzima tuliwaambia kwamba maoni ya Watanzania yatazingatiwa na baadaye tuliyawakilisha kwenye Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uamuzi ulifanywa kwamba, tuendelee kutekeleza mkataba kama ulivyo. Kwa maneno mengine, kimsingi tunaendelea hatua kwa hatua, kwa maneno mengine, maoni ya Watanzania waliyoyatoa kuhusu jinsi gani tuelekee kwenye Shirikisho yalizingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo tunafanya nini? Wakuu wa Nchi walielekeza kwamba, wakati umefika sasa kuwa na Sera ya Viwanda na Uwekezaji katika Afrika Mashariki. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka katika mwaka 1963 kulikuwa na kitu kilichoitwa *Kampala Agreement*; ilikuwa inalenga jambo moja kwamba, kila nchi mwanachama iwe na jambo ambalo inajikita zaidi kulingana na uwezo ilionao na ndiyo maana tukawa na kiwanda cha kutengeneza matairi (*General Tyre*). Bahati mbaya, makubaliano hayo wengine hawakuyatekeleza, badala ya kuwa na *General Tyre* peke yake inayozalisha matairi kwa ajili ya Afrika Mashariki, wengine nao wakaibuka wakaanzisha viwanda na tukaanza kushindana wenye kwa wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lengo la ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki sio kushindana wenye kwa wenye, lengo ni kwa yule mwenye *comparative advantage* katika jambo Fulani, ajikite kwenye kuliendeleza hilo na mwingine ambaye ana uwezo wa jambo Fulani, ajikite kwenye kuliendeleza hilo ili tuweze kuwa na mashirika na makampuni makubwa ambayo yanaweza kuhimili ushindani wa Kimataifa.

Tukiendelea kuwa na mtazamo wa kushindana wenye kwa wenye, mipaka ya dunia itafunguliwa kwa sababu msisahau tupo kwenye *World Trade Organization Negotiations*. Mipaka ya dunia ikishafunguliwa zaidi, maana yake hatakuwepo Mkenya, Mtanzania, Mnyarwanda wala Mrundi, sote tutakwenda na maji. Kinachotakiwa ni sisi kuungana na kujipanga vizuri, tuone tunaweza kushindana vipi katika soko hili kubwa la utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, kulikuwa na hoja ya Upinzani kuhusu mazungumzo ya vijana kukosa ajira. Hili nadhani nimelizungumzia, tutalizingatia kwenye soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia ya *free movement*, tukizungumzia katika soko la pamoja kuna kitu kinaitwa *free movement*; kumruhusu mtu kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Suala la kuijuliza ni *free labour*, tukisema *free labour*, *labour*

ipi; *skilled labour, semi-skilled or unskilled labour?* Kwamba, tukuruhusu utoke sehemu moja kwenda nyingine kufanya kazi, lakini kuna swali la kuuliza; kazi ipi tunakuruhusu kwenda kuifanya? Tunakuruhusu kutoka sehemu moja kwenda nyingine kuzunguka zunguka tu au tunakuruhusu kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *European Union*, utakuta kwamba, hata wao wanapozungumza *free movement of labour*, Ufaransa anaweza kusema naruhusu *engineers* tu wa ndege ndiyo nawahitaji, kwa hiyo ni *engineers* wa ndege tu ndiyo watakaoruhusiwa kupata ajira Ufaransa. Ukienda Uingereza watasema, tatizo letu ni manesi, kwa hiyo, kwenye hili soko la ajira nitaruhusu manesi tu kutoka sehemu yoyote *European Union* waje kufanya kazi hapa. Kwa hiyo, tunaposema *free movement*, kwa kweli *free is not free, it is free in invited comma.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wangu ndiyo unavyoonyesha, hakuna *free iliyo free, it is free in invited comma.* Ndugu zangu hata hapa Tanzania, pamoja na kwamba ni nchi moja, huko tulikotoka ulipokuwa ukitoka sehemu moja kwenda nyingine, lazima uripoti kwa Balozi useme jamani, mimi leo hii nimepokea mgeni ametoka sehemu fulani amekuja hapa na ni mtu wa kawaida, hana matatizo na utaratibu ule ulikuwa unatusaidia sana hata *ku-control* vitendo vya ujambazi na vitu vingine. Kwa hiyo, hata ndani ya Tanzania humu, sio *free as free* kwamba utakwenda tu bila kufuata taratibu. Kwa hiyo, hata katika soko la pamoja, haya mambo tutayaangalia kwa makini ili tuone tutakwenda namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize hapo, ninaposema hivyo haimaanishi kwamba, Tanzania hatutaki soko la pamoja. Ninachosema, tunahitaji soko la pamoja endelevu, ambalo halitavunjika kwa sababu ya nchi moja kulalamika kwamba, soko hilo limeleta madhara kwenye uchumi wa nchi yake. Kuna mambo mawili unaweza kufanya; moja, unaweza kuachia soko la pamoja ambalo halina udhibiti, matokeo yake hata huu ushirikiano utavunjika. Kwa hiyo, ukiwa unataka ushirikiano udumu, lazima uwe makini; huo ushirikiano unaufanya namna gani vinginevyo, tunaweza kurudi kule tulikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia mapendekezo ya ndugu zangu wa Upinzani kwamba, ingekuwa vizuri tuanze na *free trade, custom union, common market* halafu twende kwenye *political integration*, si jambo bayo lakini hakitofautiani na kile kilicho kwenye Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao unasema tutaanza na *custom union*, tutakwenda kwenye *common market*, tutakwenda kwenye sarafu moja na hatimaye kwenye shirikisho la kisiasa. Kwa hiyo, nawashukuru kwa mapendekezo hayo, ambayo yanaendana kama ambavyo imependekezwa kwenye Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imetoka ya kwamba, je, Jumuiya ya sasa haitavunjika? Napenda niseme kwamba, hatutarajii Jumuiya ya sasa ivunjike kwa sababu tumetafuta mwarubaini wa kuhakikisha Jumuiya haivunjiki kama ilivyovunjika ile ya awali. Mwarubaini huo ni upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tulichogundua katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kwamba, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika, zipo taasisi zilizoendelea kufanya kazi, kwa mfano, *East Africa Inter-University Council*. Kwa sababu hiyo tumejifunza kwamba, ukitaka Jumuiya iendelee kuwepo ni vizuri zaidi kuhimiza mahusiano ya watu kuliko mahusiano ya kinadharia. Ndiyo maana tunajaribu kuangalia vitu ambavyo vinaweza kuweka watu pamoja na kuhakikisha kwamba, Jumuiya haivunjiki na ndiyo maana ukisoma mkataba unaonyesha Jumuiya hiyo tunasema itakuwa *people centred*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kitu wanaita *asymmetry principle* kwamba, katika ushirikiano huu kama nchi yoyote itasema katika kutekeleza jambo fulani imekumbwa na matatizo, basi lazima uisikilize nchi hiyo na uchukue hatua za makusudi za kusahihisha jambo hilo. Ndiyo maana tulipoanzisha Umoja wa Forodha, baadhi ya bidhaa kutoka Kenya tulisema zitaendelea kulipa kodi inayopungua taratibu, kwa sababu ya hiyo *principle ya asymmetry*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kitu kinachoitwa *geometry principle* kwamba, mkishakubaliana si lazima mambo yote yatekelezwe kwa wakati mmoja, mnaweza kutekeleza hayo mambo kwa *speed tofauti*, kulingana na kila nchi ilivyo tayari kutekeleza jambo hilo. Mambo haya hatukuyaweka kwa bahati mbaya kwenye Mkataba wa Jumuiya ya Afrika, lengo lake isitokee migogoro isiyokuwa ya lazima na Jumuiya ya Afrika Mashariki ikavunjika kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu mojawapo iliyosababisha Jumuiya ivunike ilikuwa kwamba, wengine walikuwa wanafikiri wanafuata uchumi wa kijamaa, wengine wanafikiri wanafuata uchumi wa kipebari, kwa hiyo wakati mwingine hata mkikaa kwenye vikao mnaanza kuulizana unafikiri mwenzako ni bepari na mwingine anafikiri wewe ni mjamaa. Kwa hiyo, safari hii tukasema nchi zote zinazoamua kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, lazima zifuate uchumi wa soko. Kwa hiyo, mradi wewe ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hakuna pebari wala mjamaa nyote mnafuata uchumi wa soko. Kwa hiyo, hatutarajii tena tuanze kunyoosheana vidole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile muundo wa Jumuiya haulengi kuwa na mashirika makubwa ambayo yatapelekea kuanza kulalamika kuwa nchi fulani ndiyo inanufaika kuliko nchi nyingine. Ndiyo maana kwa utaratibu wa sasa, Jumuiya inalenga zaidi kwenye kuwezesha mambo kutokea kuliko kuhusisha mashirika makubwa kama ilivyokuwa kabla, ambayo badala ya kusaidia Jumuiya kuwepo, iliishia kuvunjika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu ndugu zangu wa Kambi ya Upinzani, wametoa hoja nyingi nzuri na zote ni nzuri, tutaendelea kuzifanyia kazi moja baada ya nyingine kadiri hali itakavyokuwa inaruhusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwang'onda, namshukuru sana kwa mchango wake mzuri. Amesisitiza umuhimu wa kuimarisha reli, kuna mpango kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu wa Isaka – Kigali - Bunjumbura

lakini umesema ni vizuri tukawa na bajeti ya ziada. Naomba niseme kwamba, kuitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuna kitu tunakiita *East Africa Development Fund*, ambapo wahisani mbalimbali huwa wanachangia Mfuko huo kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ndiyo maana miradi mingi ya barabara na reli ya Afrika Mashariki, imeshafanyiwa *feasibility study* si kwa fedha za nchi wanachama, bali kwa fedha ambazo zinatafutwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivi karibuni ndiyo maana Mtaalam Mwelekezi amemaliza kuandaa mkakati wa kuimarisha reli za Afrika Mashariki na mkakati huo uliandaliwa kwa dola laki nne na hamsini elfu lakini fedha hizo zimepatikana kutokana na vyanzo mbalimbali ambavyo wafadhili mbalimbali wanaosaidia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, *ADB* imesaini Mkataba na Afrika Mashariki kutoa fedha za kufanya *feasibility studies* ya baadhi ya barabara ambazo zipo katika *East Africa Network Program*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwang'onda nakushukuru sana na niseme kwamba, hilo tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyaa naye ametoa hoja nzuri, amesema kwamba, bajeti hii ameiangalia na akasema ameona ina sera tu. Kwa kweli, naomba niseme kwamba, Mheshimiwa Mnyaa alichoona hajakosea ni kweli bajeti hii inatakiwa ijikite kwenye sera tu kwa sababu kazi yetu kubwa ni kuratibu na katika haya masuala ya utendaji lazima utambue mipaka yako ya kazi. Ukiona Waziri wa Afrika Mashariki, anaanza kuzungumzia masuala ya utekelezaji wa Miradi ya Barabara, ujue huyo ameacha kazi yake anaanza kufanya kazi nyingine. Kazi yangu ni kuratibu, kutoa sera ya masuala ya miundombinu ya barabara na kuhamasisha wapi tunaweza kupata fedha. Nikishamaliza hapo, Mheshimiwa Kawambwa anaingia kwenye utekelezaji. Haya mambo tunagawana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikija kwenye masuala la Lake Victoria, namwona Profesa kule ananiangalia. Kwenye Lake Victoria tunasema tuna *Lake Victoria Commission*, tumeweka sera jinsi gani tufanye kuendeleza Ziwa Victoria. Nimezungumzia Mradi wa Lake Victoria lakini si kazi ya Wizara yangu kutekeleza, kazi ya kutekeleza ipo kwa Mheshimiwa Profesa Mwandosya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyaa alichoona, akaona ni upungufu, si upungufu ni mafanikio na nimezingatia kuhakikisha Wizara hii injikita tu kwenye sera na si kwenye utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia ya usafiri wa baharini kwamba, ingekuwa vizuri tukaangalia. Hii ni hoja ya msingi, mara nyingi tunazungumzia Lake Victoria lakini kuna hoja ya msingi kwamba, je, huko baharini tunafanyakaje? Kuna hoja sasa tunaizingumza kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunaangalia *Lake Victoria Basin Commission* tuipe madaraka ya kuangalia masuala ya kwenye bahari au tuanzishe chombo kingine cha kusimamia masuala ya kwenye bahari? Kwa hiyo, hoja yake ni ya msingi na tutaiwekea msukumo ili tuone tunafanya nini kuhusu masuala ya bahari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imetolewa na Mheshimiwa Mnyaa kwamba, sasa Zanzibar inawakilishwaje katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mambo yasiyo ya Muungano. Kwa muundo ulivyo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kwamba, kila

nchi mwanachama hupeleka Mawaziri wake kwenye Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kadiri inavyoona inafaa. Kwa hiyo, tunapokwenda kwenye Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vya Baraza la Mawaziri; Mawaziri kutoka Zanzibar wanakuwepo. Kabla hatujakwenda kule, kama jambo fulani tunajua linaihusu Zanzibar basi tutakaa na Mawaziri wa Zanzibar na watatueleza jambo hilo kwa maslahi ya Zanzibar ili tujuu twende na msimamo upi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, wakati wote kuanzia ngazi ya Wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri, Marais, Wawakilishi kutoka Zanzibar wanakuwepo na maslahi ya Zanzibar yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja, tulikuwa na tatizo la bei ya mchele, Waziri wa Biashara wa Zanzibar akatuandikia akasema jamani eenh, tukiendelea kutumia hii *common external tariff* ya kwamba mchele uendelee kutozwa asilimia sabini na tano kutoka nje ya Afrika Mashariki, sisi wa Zanzibar tutapata matatizo makubwa. Alipotuletea leo, kesho yake tukawaandikia kwenye Jumuiya kwamba, ili tuhakikishe Zanzibar inapata chakula cha kutosha, tunaomba tupunguze hiyo kodi ya asilimia sabini na tano. Kwa hiyo, ilitekelezwa waliipokea kama imetoka Tanzania na ilibidi watekeleze. Kwa hiyo, maslahi ya Zanzibar yanalindwa wakati wote na hakuna jambo lolote ambalo linapotea kwa sababu ya utaratibu wetu huu tunaoutumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, namshukuru kwa hoja zake nzuri alizozitoa; amesema ni vizuri tuangalie *formula* mpya ya kuangalia jinsi gani tunaweza kutafuta fedha za kuendelea kujenga miradi yetu. Vilevile ametoa hoja nzuri kwamba, tuongeze kasi ya kutafuta fedha, tutaendelea kufanya hivyo ili tuitangaze miradi yetu na ndiyo maana tulikwenda hadi China kule kuomba wenzetu watusaidie na tuna mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyaa amesema, mbona hii hotuba imejaa kutembea? Kutembea ndiko kufanya kazi, maana lazima uende China ukutane nao, uzungumze nao, uwaeleze Afrika Mashariki ipo, lazima uende Brussels uwaeleze kwamba kuna Afrika Mashariki na lazima uende Marekani, uwaeleze kwamba kuna Afrika Mashariki. Kwa Wizara yetu, ukiona Waziri wa Afrika Mashariki hatembei, ujue tayari ameshindwa kazi, lazima tutembee ili kuhakikisha tunafanya kazi ya kuiendeleza hii Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la soko la pamoja, nashukuru kwamba, kuna hoja imetoka kwamba tufanye kila linalowezekana, nadhani aliitoa Mheshimiwa Zitto kwamba ingekuwa ni vizuri tuharakishe Rwanda na Burundi kutelekeza Umoja wa Forodha. Ni jambo la msingi tunalikubali, kwa sababu kibiashara tutanufaika na ndiyo maana wakati wa mazungumzo ya kuruhusu Rwanda na Burundi ziwe Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuliwaambia kwamba na sisi watupunguzie ushuru kama ambavyo wamewapunguzia Uganda na Kenya na walikubali kwamba, watapunguza kwa asilimia themanini. Waziri wa Biashara atalifuatilia hili ili tupate unafuu wa kupunguziwa asilimia themanini kwa bidhaa zetu zinazokwenda Rwanda na Burundi, kabla hawajaanza kutekeleza Umoja wa Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia hoja ya Mheshimiwa Zitto kabwe, ametoa ombi kwamba, ingekuwa vizuri Kigoma na wao wakaandaa *Summit*. Sasa ningependa anipigie makofim bahati mbaya hayupo, namwambia kwamba nakubali lakini kimsingi ningekuwa namdanganya. Naomba mnielewe vizuri, nasema ningependa anipigie makofi, ningemwambia nakubali itakuwa Kigoma, ningekuwa namdanganya kwa sababu maamuzi yote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima yafanywe kwenye vikao na kwa kushauriana nyote. Wazo ni zuri, lakini siwezi kuwaahidi ili bajeti ijayo asije kusimama hapa akasema, Mheshimiwa uliahidi hiki mbona hukutekeleza.

Mheshimiwa Zitto, kuna jambo moja ambalo amelisema kwamba, sasa Rwanda imekuwa Mwenyekiti akasema basi atakayefuata ni Burundi. Utaratibu wa nani anakuwa Mwenyekiti, tuliwaachia Wakuu wa Nchi wanapokaa wao ndipo wanaamua nani awe Mwenyekiti. Kwa hiyo, hakuna anayejua kwamba, lazima Burundi au Tanzania awe Mwenyekiti kipindi kijacho. Wakuu wa Nchi huwa wanakutana, wanaangalia wafanye nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati hii Jumuiya ilipoanza, Kenya walikaa kwenye Uenyekiti muda mrefu walikubaliana Marais kwamba, kwa busara za Mzee Arap Moi, ndiyo Jumuiya imeanza acha akae muda mrefu, alikaa muda mrefu baadaye ikaja *rotation* sasa wamekuja Rwanda, Burundi. Kama isingekuwa Rwanda na Burundi kuja Tanzania, ilikuwa inakuwa zamu yetu, lakini kama mnavyofahamu, Tanzania sio ving'ang'anizi wa kutaka madaraka, hatukuona sababu ya kung'ang'ania kwamba, lazima mtupe sisi Uenyekiti. Viongozi walikaa, wakazungumzia wakasema hakuna tatizo basi ngoja iwe zamu ya Rwanda na ikifika wakati watakaa watazungumza, inaweza kuwa zamu ya Burundi au ya Tanzania, kwa sababu katika masuala hayo kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba masuala yanazidi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imetolewa hapa kuhusu soko la pamoja. Ni jambo muhimu sana na Bunge hili tumekutana na Kamati, ingekuwa vizuri na Bunge hili tukae nanyi. Katika suala hilo, hatuna la kuchagua ni lazima tufanye hivyo, tulishaamua, tutaendesha semina hapa kuhusu masuala ya pamoja na tutaendesha semina kule Baraza la Wawakilishi, Zanzibar. Katika hilo, hatuna la kuchagua lazima tufanye hivyo, kwa sababu mwisho wa siku ile itifaki ya soko la pamoja italetwa katika Bunge hili kwa ajili ya kuridhiwa. Kwa vyovoyote vile, hatuwezi kuendelea na mambo yetu, tukawaleta wakati wa kuridhia, itabidi tukutane nanyi, tuwaeze na tutawapa hata ule utafiti uliofanyika ili nanyi muweze kujua tunapoweka msimamo fulani kwa nini tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imejitokeza kwamba, ingekuwa vizuri tukaweka utaratibu wa kuwapata Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Ndugu zangu, utaratibu wa sasa unatoa fursa kwa nchi wanachama waamue utaratibu upi watumie, jinsi ya kuwapata Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Maeneo mengine, utaratibu huu umefanya kazi vizuri lakini katika maeneo mengine haukufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna hoja kwamba, tuwe na sheria ya jinsi ya kuwapata Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hiyo sheria inaweza kuwepo, lakini jambo la msingi ni watu kujifunza kuheshimu sheria na taratibu zilizopo. Unaweza kuwa na sheria nzuri, lakini kama watu wakiamua kutoifuata yatakuwa ni matatizo. Kwa hiyo, nakubaliana na hoja hii kwamba, tuwe na sheria na hili linazungumzwa na ni matarajio yangu, uwezekano upo wa kuwa na sheria ya kuwapata Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki; lakini swali je, watu wapo tayari kuheshimu sheria na taratibu? Kwa hiyo, changamoto kubwa ni kufuata sheria na taratibu, unaweza kuwa na sheria nzuri lakini usipozifuata ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mgana Msindai, alichangia kwa maandishi alisema kwamba, kuna *Local Government Association*, ameomba ipate nafasi katika Jumuiya. Zipo taratibu mbalimbali, anaweza kupewa *observer status* lakini tumelichukua tutawasiliana nao tuone wanaweza kupata *status* ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, namshukuru kwa mchango wake wa mambo mengi, alielezea matumizi ya Lugha ya Kiswahili, akasema ingekuwa vizuri basi tuhimize Kiswahili. Tutaendelea kuhimiza na ndiyo maana tumeomba Tanzania tuwe Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili na tutalisimamia hilo ili hatimaye tufanikiwe. Vilevile tutaendelea kuwashauri wenzetu kuwa, kwa kuwa sasa Kiingereza ndiyo lugha rasmi pekee, basi ni vizuri hata Kiswahili sasa kukifanya lugha rasmi, kwa sababu hata katika *African Union* wanazungumza Kiswahili kule. Juji nilimwona Mheshimiwa Rais wetu, akihutubia kule kwa Kiswahili. Kwa hiyo, kama jambo linawezekana *African Union* kwa nini lisiwezekane katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja imezungumziwa kwamba, kuna kesi kule inaendelea, maamuzi yake yakoje, kesi ambayo ilikuwa inapinga kuanzishwa kwa Mahakama? Kesi kama inaendelea kule Mahakamani ni vizuri tukaiacha ikaendelea, lakini katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tuliendelea na taratibu zetu. Kama Mahakama itaamua vinginevyo, basi tutafanya uamuzi kwa wakati huo. Walikuwa wanajaribu kusema kwamba, taratibu zilizotumika kuanzisha Mahakama za Afrika Mashariki hatukufuata mkataba. Nisingependa kulizungumzia hili sasa isije kuonekana kwamba, naingilia uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba, tupanue uwezo wa Mahakama, waanze kusikiliza hata kesi nyingine za masuala mengine. Hivi sasa Mahakama ya Afrika Mashariki, inashughulikia masuala yanayohusiana na tafsiri ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini sasa hoja hii lazima nchi wanachama wote wakubaliane na kadiri shughuli zitakavyozidi kuongezeka, kadiri tutakavyozidi kushirikiana ni matarajio yetu kwamba tutafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya Tanzania kujiandaa katika ushindani. Mambo yote yanayofanyika hapa Tanzania, kimsingi tunajiandaa. Napenda niseme tu hatujiandai kwa sababu ya kushindana na Kenya, Uganda, Burundi wala Rwanda, tunajiandaa kwa ajili ya kushindana katika dunia ya utandawazi. Maana Kenya ni sehemu ndogo tu ya dunia hii na ndio maana tunawekeza zaidi kwenye elimu na ndiyo

maana tukapewa nishani ya nchi inayoongoza duniani kwa kuwekeza sana kwenye elimu. Ukiangalia bajeti zetu, kwa bajeti zilizopita na hii, sehemu kubwa ya fedha imeelekezwa kwenye elimu, yote hiyo ni katika sehemu ya kuijandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uamuzi tuliofanya hapa wa kuongeza shilingi mia moja kwenye ushuru wa mafuta, nia ya Wabunge ilikuwa kwamba tuwe na fedha nyingi zaidi za kutengeneza miundombinu, ilikuwa ni sehemu ya kuijandaa kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye miundombinu iliyo bora zaidi. Tunaendelea kuwavutia wawekezaji, ukiangalia takwimu zilivyo Tanzania ndiyo tunaongoza kwa kuvutia wawekezaji katika Afrika Mashariki.

Mwaka 2006, tulivutia wawekezaji wa mitaji yenye thamani ya milioni mia nne na hamsini na sita na aliyetufuata alivutia wenyte thamani ya milioni mia mbili na hamsini. Kwa hiyo, yote haya tunayafanya kwa nia ya kuendelea kuijandaa na kufanya Tanzania kuwa na uchumi ulio bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwa Mheshimiwa John Paul Lwanji, ameleta hoja kwamba, suala la Serikali moja Afrika Mashariki liwekwe kando. Tumemsikia, ameongezea kuwa kile ambacho Watanzania wengi walishasema na ndiyo maana tunesema twende hatua kwa hatua, Serikali moja ikija basi hiyo tutaitatua huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ametoa hoja nzuri, akasema kwamba, waliandaa *Guidelines for Transboundary East Africa Environmental Assessment*, naye alikuwa kati ya jopo la wataalam. Nachukua nafasi hii, kumpongeza kwa kufanya kazi hiyo nzuri na hao wataalam aliokuwa nao, lakini nimwombe kwa nia nzuri kwamba, tuwasiliane zaidi ili tuone ni jinsi gani hiyo kazi waliyoifanya tunavyoweza kui-formalize ili iingizwe katika mfumo wa kawaida, lakini nawapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja ya kwamba, je, Rwanda na Burundi itakuwaje? Tulichokubaliana ni kwamba, inapotokea jambo lolote lile, basi Rwanda na Burundi na wao wanaongezwa katika utafiti huo.

Mheshimiwa Meryce Emmanuel, ametoa hoja akasema kwamba ni vizuri kule Ziwa Victoria vijana wetu waweze kupewa fursa ya kuvua samaki. Napenda niseme kwamba, kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki tunafanya mambo mbalimbali. Moja, tumepata meli inaitwa RV Jumuiya, mojawapo ya kazi yake ni kutafiti aina ya samaki waliopo katika Ziwa Victoria na hiyo meli itatusaidia sana kuweza kupanga vizuri kuangalia ni jinsi gani tunawenza kuhakikisha tunakawa na samaki amba hata hawapendelewi katika soko la nje. Maana hivi sasa tatizo ni kwamba, wale samaki walioingizwa mle kwenye ziwa, wamewala hata samaki wengine amba walikuwa wanatumiwa na wananchi. Kwa hiyo, lipo tatizo na kama nilivyosema, Wizara yangu tunashughulikia. Nisingependa kujikita zaidi kwenye hili, atakuja Mheshimiwa Waziri wa Masuala ya Uvuvi, nadhani anaweza akawa na majibu mazuri zaidi. Ninachowezwa kusema, kwa sasa tunayo meli ya RV Jumuiya, itatusaidia hata kutafiti aina ya samaki walio mle.

Vilevile tunayo *East Africa Fisheries Organisation*, inayojitahidi kuhimiza uvuvi endelevu na kupitia kwenye *Revamp two*, bado vijana wetu wanaweza wakabuni miradi na wakaibua itakayowawezesha kufuata masharti ya kuvua katika Ziwa Victoria. Maana kuna hoja hapa wanasema kwamba, usitumie nyavu zenyenye matundu makubwa, lakini unakuta kijana yeye nyavu aliyonayo ni yenye matundu madogo, ambayo inachukua hata wale samaki wadogo. Ukitaka kumsaidia huyu, umuwezeshe apate mkopo wa kuweza kuwa na nyavu za kununua mtambo. Hilo tutalifanya na kupitia kwenye *Lake Victoria Environment Management Two*, bado vijana wetu tukiwapanga vizuri wanaweza kupata mikopo ya kuweza kuvua uvuvi wa kisasa, wakaondoka na hii kero inayoendelea. Atakuja kuelezea kwa kina Mheshimiwa Waziri anayehusika, anataka kufanya nini katika eneo hilo. (*Makofsi*)

Halafu kulikuwa kuna hoja ameitoa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, ameipongeza Serengeti kwamba, imeweza kuingia katika Soko la Kenya. Namshukuru Mheshimiwa Kimaro kwa pongezi hizi. Amenisaidia kujibu hoja kwamba, Tanzania hatuuzi chochote Kenya, kumbe Kiwanda cha Serengeti wameweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Aloyce Kimaro akasema, kuna tatizo kati ya *Tanzania Breweries* na *Kenya Breweries*, walitaka kufanya masuala ambayo hayakubaliki kibashara. Bahati nzuri, tuna *East Africa Competition Law* ambayo inaweza ikatumika kusahihisha suala hili. Mheshimiwa Kimaro, aliipongeza Serengeti kwa kuingia vizuri katika Soko la Kenya na mimi nazipokea pongezi hizi na nitaomba na wengine wawaige Serengeti kama ambavyo wameweza kuingia kwenye Soko la Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, ametoa hoja nyingi na nzuri. Ameuliza soko la pamoja litaanza lini? Litaanza Januari, mwaka 2010, kama mazungumzo yatakuwa yamekwenda vizuri. Kwa sababu mnapoanza kujadiliana, siwezi kusimama hapa nikawahakikishia kwamba majadiliano lazima yatakamilika kama ilivyopangwa. Nia yetu ni kwamba yakamilike, lakini huwezi kujua mwenzako anakuja na hoja ipi kwenye mukutano, lakini lengo letu tuanze Januari mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha kwa kweli wataalam wetu wa fedha wanasema haujaathiri fedha za upande wa mapato. Watalaam wa *TRA* ndivyo wanavyotueleza na mimi sina shida ya kuwatilia shaka. Ameuliza hoja ya msingi kwamba, tunachukua tahadhari gani tunapozungumzia *Economic Partnership Agreement (EPA)*, pamoja na *European Union*? Kuna tahadhari mbili tumezichukua; ya kwanza, kipindi cha mpito cha kupunguza ushuru ni miaka 25. Vile vile kuna kitu tunakiita *exclusion lists*, zipo bidhaa ambazo tumesema ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi hizi za Afrika Mashariki hata baada ya miaka 25 bidhaa hizo ushuru utaendelea kuwa ule ule. Kwa hiyo, ni tahadhari ambayo tunaichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tahadhari nyingine ambayo tunaichukua ni hii ya kwamba, sasa Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki, wametuagiza tuandae Sera ya Viwanda na Uwekezaji katika Afrika Mashariki, tuweze kuongeza uzalishaji ili

tutakopokubaliana wakati ule na sisi tuwe na vitu vya kuweza kuuza nje na kuachana na kununua bidhaa nyingi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba, muundo wa sekretarieti sasa tuupange kama *commission* ya *European Union*, hoja ni nzuri na inapendeza lakini ina gharama zake. Inapokuwa kuna nchi wanachama ambao wameomba kwamba wapunguziwe mchango, hawawezi kuchangia kwa ajili ya hali ya uchumi ilivyo, unapokuta nchi nyingine hazijachangia kwa asilimia 100 kama inavyotakiwa, inabidi uwe mwangalifu jinsi unavyopanua matumizi.

Kwa hiyo, nadhani kwa sasa ni mapema mno kusema tuwe na *Commission* kama ile ya *European Union*. kadiri shughuli zitakavyokuwa zinaendelea za Jumuiya, ndivyo tutakavyokuwa tunaiimarisha Sekretarieti hatua kwa hatua. Hatua ya mwisho itakuwa kutokuwa na Sekretarieti kabisa, kwa sababu kama tutafikia kwenye Shirikisho la Kisiasa kutakuwa hakuna sababu ya kuwa na hata na kitu kinachoitwa *East African Community*. Tutakuwa sasa na Serikali ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, sasa tunavyokwenda hatua kwa hatua, Sekretarieti itaendelea kuimarishwa na kubadilika. Mwisho wa siku kama tutafikia huko tunakofikiria, huenda tusiwe tena na umuhimu wa kuwa na *East African Community*, kwa sababu tutakuwa sasa na Serikali ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Sasa tutaangalia kadiri tunavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Manju Msambya, alitoa hoja nzuri alisema kwamba, bajeti tulioipitisha kule Arusha labda ni batili, kwa sababu wale wenzetu wa Uganda walikuwa na matatizo. Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unasema, kama itatokea Mbunge fulani kupoteza nafasi, basi Spika wa Bunge husika, atalieleza Bunge la Afrika Mashariki, atamweleza Spika, siku ile Spika alisema alikuwa hajapata taarifa, Sheria za kila nchi zinatofautiana. Wenzetu Uganda wana Sheria tofauti na za kwetu, zinazohusiana na masuala ya uchaguzi. Niseme tu kwa kuwa suala hili lipo Mahakamani si vizuri kuendelea kulizungumzia ili nisionekane ninaingilia Mahakama. Kwa wanasiasa unapogundua jambo lipo Mahakamani, basi ni njia nzuri sana ya kusema kwamba, suala hilo lipo Mahakamani. Hebu tusubiri Mahakama ifanye kazi yake. Mheshimiwa Msambya, aniruhusu na mimi nitumie upenyo huo kwamba, suala hilo lipo Mahakamani, hebu tusubiri uamuzi wa Mahakama utakuwa namna gani.

Mheshimiwa Msambya, amekuja na hoja akasema Rwanda na Burundi tumewapokea lakini wana matatizo, ingekuwa vizuri tuwaache. Napenda niseme *European Union* ya sasa tunayoiona ilianza kwa sababu ya kutoaminiana, ilianza kwa sababu ya kuogopana na ilianza kwa sababu ya vita. Baada ya vita ile wanaita *Napolione World War*, mtu ambaye alikuwa anaweza kumiliki chuma na kumiliki *atomic* alikuwa anaogopwa sana katika dunia. Sasa wale waliokuwa na uwezo wa kumiliki chuma, wakaanzisha kitu kinachoitwa *Steel and Iron Association* na wale waliokuwa na *atomic* kwa kuogopana mtu asitumie *atomic* kumaliza wakaanzisha *Association* inayoitwa *Atomic*. Maana mkishakuwa mnaogopana, huyu ana *atomic* na wewe una *atomic*, sasa hujui mwenzako ataamua kuitumia lini na ataitumiaje. Kwa kuogopana huko, mnaanzisha *Association* inaitwa *Atomic Association* si kwa kupendana ila ni kwa sababu

mnaogopana. Kwa hiyo, saa nyingine ukiwa na mtu unayemtilia mashaka au una wasiwasi naye, siyo njia nzuri kumfukuza, njia nzuri ni kuwa karibu naye.

Sasa Mheshimiwa Msambya, anavyofikiri kwamba labda Rwanda na Burundi ni hatari, hata kama wangekuwa hatari, njia nzuri isingekuwa kuwaweka pembedi, njia nzuri ni kuwa karibu nao. (*Makofi*)

Ndugu zangu haya mambo yanaenda yanabadilika. Juzi nilikuwa Rwanda, niliyokuwa nikiisikia ikitangazwa siyo niliyoiona nilipokuwa kule. Naambiwa vilevile hata Burundi sasa wameanza kuingia kwenye amani na wanazidi kupatana. Kuna jambo moja; mkiwa mna ushirikiano wenu, mnaendelea na mwenzenu ambaye hayupo nanyi akasema amependa mnavyofanya anataka kujiunga nanyi, basi mjue huyo anataka kujifunza kutoka kwenu, mnachotakiwa kufanya ni kumpokea, halafu mumfundishe afanye kama ninyi mnavyofanya. Kwa kufanya hivyo, nina uhakika Jumuiya ya Afrika Mashariki, itawenza kuwa imara zaidi. Kwa sababu hata Rwanda na Burundi tukisema wakae nje, yakinkeza machafuko, tutake tusitake sisi Tanzania ndiyo kimbilio lao. Kwa hiyo, ni bora tukawa nao, tukapanga nao vizuri na tukawasaidia hao wenzetu ili nao waweze kutengemaa kama sisi ambavyo tumetengemaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Juma Killimbah, kutoka Iramba Magharibi amesema kwamba, Shirikisho twende taratibu, tunashukuru na sisi tutaenda taratibu.

Mheshimiwa Felix Kijiko amesema, upo umuhimu wa kutumia Kiswahili, tunasema kwamba tutaendelea kukizingatia.

Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ametoa hoja akasema kwamba ni vigezo vipi vinatumika katika kuziruhusu nchi kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vigezo viro vingi; moja, awe jirani na sisi, lakini pili, akubaliane na mambo yetu tunayoyafanya na ndiyo maana Rwanda na Burundi tuliwaambia sisi hapa tunazungumza Kiswahili na Kiingereza; je, mpo tayari? Wakasema ndiyo wapo tayari, watazungumza Kiswahili na Kiingereza. Tuliwambia sisi Jumuiya ya Afrika Mashariki ukijiunga nasi lazima ufuate uchumi wa soko, wakasema ndiyo wapo tayari kufuata uchumi wa soko. Tukawaambia bajeti zetu huwa zinaanza mwezi Julai na kuishia mwezi Juni mtakubali kubadilisha, maana wao bajeti zao zinaanza mwezi Januari, wakasema ndiyo, wakakubali kubadilisha wataanza mwezi Julai. Kwa hiyo, tuliwaambia sisi mnavyoona tupo hivyo, mko tayari kuwa kama sisi, wakasema ndiyo, wapo tayari kuwa kama sisi, ndiyo maana tukawapokea kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, hivyo ndivyo vigezo ambavyo tunavifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage, amezungumzia suala la vijana wetu wa Ziwa Victoria; nimelizungumzia kama alivyosema Mheshimiwa Meryce Emmanuel. Nawashakuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kuona umuhimu wa kuwatetea hawa ndugu zetu, lakini kama nilivyosema, sisi kama viongozi hapa tuangalie ni njia zipi bora zaidi, tunazoweza kuzitumia ili kuwawezesha ndugu hawa kufanya kazi yao vizuri zaidi ya uvuvi na kuwawezesha kupata mboga.

Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge Viti Maalum amesema kwamba, alisikia nchi moja ilikuwa inatangaza kwamba, Kilimanjaro ipo Tanzania. Mimi labda niseme tu katika hili kwamba, kama fulani akitangaza Kilimanjaro anafanya kazi yako iwe nyepesi. Unachowea kufanya wewe ni kusema huyu bwana ni muongo, amesema ipo kwake wakati haipo kwake. Hoja ilikuwa kwamba, kuna nchi moja ilikuwa inasema Mlima Kilimanjaro upo kwenye nchi yake.

Mtu akikusaidia kutangaza hilo, wewe anakuwa amekurasishia kazi kwamba walau ametaja kuwa Kilimanjaro ipo. Kwa hiyo, wewe unapokwenda unasahihisha pale tu, kwamba Kilimanjaro uliyoambiwa iko kule haiku huko iko huku. Hapa atapenda ajue hivi ni kweli ninachoambiwa?

Ndugu zangu niwaambie, Tanzania ya sasa ni tofauti kabisa na Tanzania ya miaka iliyopita. Tanzania ya sasa, imetangazwa zaidi katika dunia nzima. Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri ya kuitangaza. Hata juzi tulikuwa na hii *Sullivan Summit*, imeitangaza Tanzania.

Zamani usingefungua *CNN* ukaiona Tanzania, siku hizi ukifungua *CNN* ukaiona Tanzania, usikimbie ukafikiri umekosea, hapana na *CNN* itakuwa inaitangaza Tanzania na ni kwa mikakati tulioiweka makusudi ya kuitangaza Tanzania.

Tutaendelea kufanya hivyo kwa nia moja tu kwamba, Tanzania tunazo rasilimali nyingi ambazo hatujazitumia vizuri, kama ambavyo tunatakiwa kuzitumia. Kwa hiyo, lazima tujitangaze zaidi na kazi hiyo itaendelea zaidi na zaidi. (*Makofsi*)

Pia Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, kutoka Chambani amezungumzia suala la ardhi; nasema tutalizingatia. Lengo letu tutakwenda kwenye soko la pamoja, lakini vilevile tutazingatia maslahi yetu.

Mheshimiwa Paul Kimiti, nakushukuru kwa mchango wako mzuri, umeuliza je, ile barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga nayo ni kati ya Barabara za Afrika Mashariki? Tunaposema Barabara za Afrika Mashariki, mtandao mmojawapo ni kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi; ni barabara ya Afrika Mashariki. Hii haimaanishi kwamba, lazima itakuwa ya Afrika ya Mashariki kama Kamala ataonekana ndiye mkandarasi anayeisimamia hiyo barabara, hapana.

Barabara ya Afrika Mashariki watekelezaji ni kupitia kwenye Wizara ya Miundombinu. Barabara nyingine nyingi kama ilivyo Arusha, Namanga, sasa tayari tumepata fedha za kufanya utafiti. Hata barabara ya kutoka Arusha unakuja Kilimanjaro unakwenda mpaka Holili nayo ukiiangalia ni ndogo na tumeipatia fedha kwa ajili ya *feasibility study* ili baadaye tuipatie fedha za kuweza kuiboresha zaidi. Bahati nzuri *ADB* tayari wameshakubali kutoa fedha za ujenzi wa barabara hii. (*Makofsi*)

Halafu Mheshimiwa Zaynab Vulu, tunakushukuru umeeleza umuhimu wa kutunza Ziwa Victoria. Mheshimiwa Diana Chilolo, tunakushukuru sana umesema kwamba,

tulegeze masharti ya kutembeleana; nakubaliana na wewe tutaendelea kuyalegeza hatua kwa hatua na ndiyo maana kwenye soko la pamoja tutaangalia eneo hili.

Waheshimiwa Wabunge, narudia tena kuwashukuruni nyote kwa hoja zenu nzuri mlizozitoa, nasema tunashukuru kwa ushauri wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukubaliane kwamba, Mheshimiwa Waziri amejitahidi kutoa maelezo. Ametoa hoja na imeungwa mkono. Sasa tunaingia hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 97 - Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Kamati ya Matumizi, nafikiri maelezo yote ya jinsi ya kutumia vitabu vyetu, kila Mbunge amekwisha kuwa mzoefu sana kwa sasa. Kwa hiyo, bila kupoteza muda, sasa namwomba Katibu atuongoze.

Kif. 1001 - *Administration and General* Sh. 1,464,840,300

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Vote 97, Progamme 10, Sub-vote 1001, item 250100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kutoa shilingi na nikiri tu kwamba, kwa asilimia 85 nimeridhika na majibu ya hoja za Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wametoa ufanuzi mzuri. Hizo asilimia 15 nilizobakia ili niridhike vizuri *hundred percent*, ndiyo ninataka ufanuzi kisera. Kwa maana hiyo, katika suala lile la hoja ya kushirikishwa kwa Zanzibar. Nimefahamu na ninaelewa kwamba, Mawaziri wanashirikishwa, Makamishna, *Directors* na baadhi ya wataalam katika sehemu mbalimbali za masuala hayo na hilo ninalielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ilikuja pale katika Wizara yenyewe na sisi tukizungumza hivi tunazungumzia kwa nia hiyo ya kuuimarisha Muungano. Kwa sababu haya manung'uniko ndiyo hatuyapendi, tunataka tuwe na Muungano ule ambao hauna manung'uniko kama Naibu Waziri alivyosisitiza na sisi ndiyo lengo letu. Kwa maana

hiyo, ajira sasa siyo utaalal; nilitaka atupatie maelezo kwa nini Wazanzibari hawashirikishwi katika vitengo mbalimbali nya mazungumzo.

Tukizungumzia ajira katika Wizara ya Afrika Mashariki, huwa tunajibiwa kwamba, Wazanzibari hawana elimu, kitu ambacho mimi sikiamini. Nikatoa maelezo na nikatoa mfano, kwa maana hiyo, majibu mengine tunayopata, wakipeleka barua Zanzibar kutaka watu; hawajibiwi au hawapelekwi kana kwamba hakuna watu wanao-*qualify*, kitu ambacho mimi sikiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kisera na kwa mfano, aliotutolea Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anajibu hoja ya Mheshimiwa Manju Msambya ya kwamba, mtu ukiwa una hofu naye, mshirikishe karibu uwe naye na usimkimbie, kwa kauli yake mwenyewe. Sasa katika Wizara hii, ikiwa hakupata wale watu ambao wanahitajika kutoka upande mmoja na upande mwingine wapo wenye *qualification*; kwa nini asiwachukue tuwe pamoa? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, atufanfulie sera gani na atafanya mipango gani ili Wizara yake iwe na sura ya Muungano? Ahsante.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maoni ya Mheshimiwa Mohamed Nyaa. Niseme mambo matatu; hii hoja ya idadi ya watumishi kwenye Taasisi mbalimbali za Muungano, tulipokuwa kwenye Kikao kinachoangalia kero za masuala ya Muungano, ambayo sasa Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Makamu wa Rais, mojawapo ya hoja iliyojiteze ni kwamba, sasa umefika wakati, tuangalie ni jinsi gani kama inawezekana, hata hizo nafasi ziwe zinaenda kwa kusema hizi ni za Zanzibar au hizi ni Tanzania Bara. Ilitoka kama hoja kwamba, sasa inahitaji ifanyiwe kazi. Kwa hiyo, uamuzi wa pale ulikuwa kwamba, jambo hili huwezi ukalichukua haraka, inabidi lifanyiwe kazi, tuone tunaweza tukalitumia namna gani. Kwa hiyo, matarajio yangu ni kuwa litafanyiwa kazi kwa ujumla. Naongelea kwa ujumla, lakini hilo la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya Wizara kama Wizara, huwa tukitangaza tunawahamasisha watu mbalimbali waombe, wakiwemo wa kutoka Zanzibar. Jumuiya iliyopita, tulipata Mzanzibari mmoja ambaye hatukumpata kwa sababu ni Mzanzibari ila alifanya vizuri kwenye *interview* na tukaomba aje, lakini bahati mbaya hakuja. Leo wataalam wangu wameniambia katika *interview* iliyofanyika juzi pale Wizarani, aliyefanya vizuri sana kwa upande wa Wachumi wamekuja kugundua ni kijana anayetoka Zanzibar. (*Makofî*)

Sasa wakati wowote tutamwandikia barua ya kumwita, wasiwasi wangu ni je, atakuja? Ninachoomba, wanisaidie na wao, tukiwa tunawapa nafasi basi wawahamasisha waje. Sasa wakati tunasubiri ile ya jumla, Waziri kama Wizara hii, naomba niwahakikishie nitakuwa ninafutilia kwa karibu. Sisi Mawaziri hatuingii kwenye *interview* ni Wataalam tu ndio wanaoingia. Nikiwa ninapata taarifa, nitawashauri wasaidizi wangu waangalie ni jinsi gani, kwa sababu mimi kama Waziri wa Afrika Mashariki, sijaulizwa mbona hatuoni hata Mzanzibari? Mimi ninasikitika zaidi kuliko ye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ninasikitika zaidi kuliko yeye. Suala hili nitalizingatia na huyo aliyefanya vizuri ni matarajio yetu atakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niseme kwamba, mbali na hao wanaoomba kazi, kuna nafasi ambazo wanaweza wakahamishwa kutoka kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wakaja kwenye Serikali ya Muungano. Nimeamua kwamba, tutaanza kuitumia njia hiyo. Ninawasiliana na Waziri mwenzake wa Masuala ya Utumishi, tuone tunaweza kufanya nini? Mimi ninasikitika zaidi kuliko Mheshimiwa Mbunge anavyosikitika. Napenda nimhakikishie kwa siku zijazo, sura za wataalam wetu pale zitabadilika. (*Makofi*)

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 97, Programme 10, Sub-vote 1001, item 250100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia Miradi ya Maendeleo. Kuna tabia ya muda mrefu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, katika bajeti yake inaingiza Miradi ya Maendeleo hasa nitaje ya barabara. Ikifika wakati wa utekelezaji hakuna. Nitatoa mfano, kuna barabara yangu ya Jimbo la Chambani kuanzia Kenya mpaka Kwamutola kila siku inapimwa kama vile mjamzito. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika mahali hata Wananchi wa Jimbo langu sasa hawaamini kama kweli SMZ inaweza kujenga barabara ile. Vilevile kuna Barabara ya Mgangando na Jimbo la Kiwani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, labda unisaidie tu hiyo miradi ya barabara ni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ama ni ajenda ya barabara katika Afrika Mashariki. Kama ni barabara za SMZ, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis hili Bunge halizungumzii Mpango wa Barabara za SMZ kama ulivyoanza kutoa maelezo. Kwa hiyo, kama ni zile barabara ambazo zimetajwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, basi labda hizo ndizo zinazopaswa kuzungumzwa, lakini siyo nje ya hapo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda utulie kwanza nakuja huko. Hii ni *introduction* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri kuna Mifuko hii ya *MCC* na *ADB*, ambayo itajenga barabara. Nadhani barabara zenyewe wanazifahamu, utafiti umefanywa, upembuzi yakinifu nafikiri vilevile tayari. Sasa nilitaka kuuliza; kama mambo yote hayo yapo na fedha za *MCC* najua zipo; wananchi wanataka kujuua vilevile pamoja na mimi Mbunge wao; ni lini zitajengwa barabara hizo? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, nitakupa nafasi tu ujibu, kimsingi ni kwamba, kama ni suala la ujenzi wa barabara, Waziri anayehusika ni wa Miundombinu. Kama ni suala la sera na hasa sera inayohusu Afrika Mashariki, Mheshimiwa Waziri amejieleza vizuri sana hapa. Mkitaka Waziri aanze sasa kujibu barabara zote zitaanza

kujengwa lini; labda Mheshimiwa Waziri unajua nikupe hiyo nafasi uweze kutoa maelezo! Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe unaweza kuwa unazifahamu vizuri zaidi.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nataka nimhakikishie kwamba, Mpango wa SMZ kuimarisha barabara za Pemba unaendelea vizuri sana. Yeye mwenyewe ni shahidi na anajua barabara mbalimbali hivi sasa zimejengwa Pemba, zikiwemo zile za Mkoani Chake; Ole kwenda Konde na kwenda Micheweni. Vilevile hizi barabara za MCC, kuna barabara ya MCC na fedha tayari zimetengwa kama ile barabara ya Mzambarauni - Pandani - Finya, Finya - Winga - Mapovu - Mzabarauni, Ipangani - Kangani, Chwale - Konjani na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mradi mkubwa sasa hivi wa kusambaza umeme kutoka Tanga kupitia usaidizi wa Serikali ya Norway, nadhani SMZ imekwishafikia hatua zote. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Salim Hemed Khamis kwamba, hatua zitachukuliwa pia kwenye barabara yake. Upo mpango wa kujenga hiyo barabara alioizungumzia ya Chambani, inayofadhiliwa na ADB na SMZ wenyewe. Kwa hiyo, naomba avute subira, shughuli hizo zinachukuliwa hatua. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 247,556,400
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 6,252,803,100
Kif. 1004 - <i>Trade, Finance and Investment</i>	Sh.739,967,100
Kif. 1005 - <i>Economic and Social Infrastructure</i> ...	Sh. 724,265,100
Kif. 1006 - <i>Political , Defence and Security</i> ...	Sh. 272,165,600
Kif. 1007 - <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh. 162,483,600
Kif. 1008 - <i>Information, EDUCAT. Communication Unit</i>	Sh. 114,245,300
Kif. 1009 - <i>Management Information System</i> ...	Sh. 117,324,800
Kif. 1010 - <i>Internal Audit Unit</i> ...	Sh.144,120,000
Kif. 1011 - <i>Legal Service Unit</i> ...	Sh.119,978,700

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 97 – Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	Sh. 98,600,000
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 267,200,000
Kif. 1004 - <i>Trade, Finance and Investment</i> ...	Sh. 216,200,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya hatua hiyo, sasa nitamwita mtoa hoja atoe taarifa.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi, limeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2008/2009, kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naona leo tuna shamrashamra kidogo, maana Mheshimiwa Waziri mshahara wake umeshikwa kidogo sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutolewa hoja hiyo sasa hatuwezi kuishangilia mpaka nimalize kuwahoji. Sasa iamueni hoja iliyotolewa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu ya Wataalamu wote, hasa wale wapiga kura wetu ambao wapo hapa ndani leo, ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Bunge zima, niwapongeze sana kwa kuwa Makadirio ya Wizara yenu sasa yamepitishwa rasmi. Tunachowaomba ni kusimamia vyema mafungu hayo, yaweze kufanya kazi zilizokusudiwa kwa ajili ya kuleta maisha bora kwa Watanzania, kupitia Muungano huo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, kazi ya kupitisha bajeti ya Wizara hiyo tumeshaikamilisha. Kabla sijafikia mwisho wa shughuli zetu za leo, ninayo matangazo machache na ningombwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge.

Tangazo la kwanza, mchana nilitangaza kwamba, kuna *invitation card* kwenye *pigeon holes* zetu na a mlipopita zilikuwa bado hazijawekwa, lakini nimeletewa taarifa sasa hivi kwamba, zimewekwa na zinahusiana na shughuli ya kesho. Kama tulivyotangaza siku mbili, tatu zilizopita, kesho kutakuwa na shughuli hapa Bungeni, wenzetu wa *TBL*; kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanabaki hapa Dodoma wameandaa *entertainment session*, ambayo tutaifanya kuanzia kesho asubuhi. Saa 9.00 alasiri tutakuwa na *football match* kati ya *TBL* na Timu ya Bunge. Niseme tu kwamba, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundu, ameshatuhakikishia kwamba, ushindi utapatikana na mambo yote yapo sawa sawa kabisa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hasa wale wachezaji wetu, wasiwe na wasiwasi mambo yote yameshakwenda vizuri. (*Makofi*)

Kesho hiyo pia tutakuwa na mechini nyingine, tutakuwa na shindano la kuvuta kamba kati yetu na Timu ya *TBL*. Kwa ujumla wetu, tumeomba tusaidiane Timu ya Bunge itakuwa na wanawake na wanaume. Mheshimiwa Said Nkumba amesema kwamba, timu ilishaingia mazoezini na imefanya kazi ya kutosha na Kapteni Msaidizi Mheshimiwa Sanya, ametuhakikishia kwamba, ushindi utapatikana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, tukusanyike kwa wingi na tunaomba Wananchi wa Dodoma basi waje kushirikiana nasi katika michezo hiyo hapo Uwanja wa Jamhuri. Kadiri mnavyojua, tupo kwenye *session* nzito ya bajeti na tunahitaji kuwa na mazoezi, lakini pia kupumzisha akili zetu na mkizingatia kwamba Jumanne tunaingia kwenye bajeti ya Nishati na Madini na mfululizo wa Wizara nyingine, kwa hiyo, angalau tunapata nafasi ya kupumzika na *ku-refresh* kidogo ili tuwe tayari kwa shughuli ya wiki ijayo.

Jioni pia tutaendelea na *entertainment* hiyo, tutakuwa na shughuli nzito kwenye ukumbi wetu hapa Bungeni na tutakuwa na muziki kutoka *Diamond Musica International* na Hadija Kopa atakuwepo na kutakuwa na mashindano mbalimbali. Mshindi atakayeshinda kwenye *football match*, atapatiwa zawadi ya shilingi milioni moja. Wale wavuta kamba chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Sanya (ile timu yetu), watapata shilingi laki tano washindi wakishashinda mechini hiyo na zawadi nyingine. Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mnaobakia hapa mhudhurie sherehe hiyo.

Kwa wale ambao wangependa kusafiri kwenda Dar es Salaam kwenye Maonyesho, nimeambiwa kwamba, basi litaondoka saa 4.00 asubuhi kesho hapa hapa kwenye Viwanja vya Bunge. Kwa hiyo, nilikuwa naomba na mimi nichukue nafasi hii, niwatakies *weekend* njema; wale tunaobaki Dodoma, tutaendelea na shughuli zilizopo na wale wanaosafiri basi Mwenyezi Mungu awasafirishe salama ili waweze kurudi hapa tena tuweze kuendelea na shughuli zetu. Nawashukuru sana kwa shughuli hii ya leo na nawapongeza wenzetu wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kumaliza shughuli zao kwa siku hii ya leo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema maneno hayo, ninaomba sasa niahirishe Shughuli za Bunge na tutakutana tena Jumanne tarehe 08 Julai, 2008 saa tatu asubuhi katika Ukumbi huu wa Bunge.

*(Saa 01.35 Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 08 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*